# Nipashe

Jumanne Juni 25, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579953
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




UKURASA 13



## China yaipa Tanzania msaada wa bilioni 60/-

UKURASA 3

# Mbunge aibua tuhuma rushwa

**ADAI** wenzake kuhongwa ili kupitisha muswada, ataka Bunge lijadili jambo hilo, Naibu Spika atoa neno...

*Endelea ukurasa wa 2*



Msanii nyota wa filamu nchini, Wema Sepetu (kushoto), akitokea mlango wa nyuma katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuachiwa kwa dhamana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wema uraiani kutoka lupango

UKURASA 3

## UCHAGUZI WA MITAA: CCM yawataja Zitto, Mbowe

UKURASA 2

**MICHEZO** UGANDA MBELEKO YA CECAFA AFCON, STARS, HARAMBEE BADO UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Mbunge aibua tuhuma za rushwa

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Salome Makamba (Chadema), jana alilitaka Bunge kusitisha shughuli zake na kujadili kuhusu tuhuma za wabunge kuhongwa fedha ili kutopitisha muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali wa mwaka 2019.

Makamba alitoa hoja hiyo bungeni jijini Dodoma jana akitumia Kanuni ya 51(iv) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayoeleza kuwa mambo yanayohusu haki za Bunge, yatawasilishwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa kanuni na endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge, jambo lolote litazuka ghafla na litaonekana linahusu haki za Bunge, shughuli zitasitishwa kwa madhumuni ya kuwezesha jambo hilo kuwasilishwa na kujadiliwa isipokuwa tu kama wakati huo kura inapigwa.

Akiwasilisha hoja hiyo, mbunge huyo alisema: "Mheshimiwa Naibu Spika (Dk. Tulia Ackson), Mheshimiwa Cecil Mwambe (Mbunge wa Ndanda-Chadema), ameeleza jambo kubwa sana ambalo linahusiana na Bunge lako.

"Wabunge wako kupewa rushwa ili kushawishi abadiliko ya sheria ndogo yaliyoletwa katika Bunge lako tukufu yaweze kupitishwa kwa namna ambayo wabunge hao wataona inafaa.

"Mheshimiwa Naibu Spika, jana (Jumapili), Bunge lako liliita Wabunge wachache takribani 40 ili kupewa uelewa wa namna sheria zilizopo kwa hati ya dharura zinataka nini, ila kilichotokea na alichokieleza Mheshimiwa Mwambe, ndo kimenishitua zaidi kwa sababu inaonekana wabunge wale wamepewa rushwa...


"Jambo hilo ni aibu kubwa kwa kuwa 'social media' (mitandao ya kijamii) inazungusha habari hiyo kwamba wabunge wamepewa pesa ili kupitisha miswada hiyo."

Makamba aliliambia Bunge kuwa tuhuma za wabunge kuhongwa zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara na anaona ni busara kwa Kiti cha Spika kuchukua hatua na ikiwezekana kuwafikisha mbele ya Kamati ya Maadili wanaoeneza taarifa hizo kama hazina ukweli.

Akitoa mwongozo kwa mbunge huyo, Naibu Spika (Dk. Tulia) alisema ofisi ya Bunge haina taarifa hiyo na hakuna mtu anayepewa idhini ya kuitisha semina bungeni.

"Ukiitisha watu huko kwingine, si mkutano unaohusu Bunge, hivyo hakuna kibali cha Spika cha kuitisha mkutano uliofanyika jana (juzi) na mimi namsikia yeye (Makamba) na ofisi mimi niko hapa, hatuna hiyo taarifa ya kuita mtu yeyote

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akibadilishana nyaraka na Makamu Mwenyekiti wa Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la China, Zhou Liujun, baada ya kusaini mkataba wa msaada wa Sh. bilioni 60, zilizotolewa na nchi hiyo kwa Tanzania, bila ya masharti yoyote, katika hafla iliyofanyika, mjini Beijing, China jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Zitto Kabwe aushtukia muswada wa Azaki

**Na Romana Mallya**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema muswada wa mabadiliko ya sheria mbalimbali unaotarajiwa kusomwa bungeni Jumatatu kama hati ya dharura, usipozuiliwa unakwenda kuua asasi zisizo za kiserikali (NGO).

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Zitto, alidai kuwa kama muswada huo hautazuiliwa, wiki ijayo, inakwenda kuwa moja ya wiki nyeusi katika nchi.

"Wiki ijayo, Jumatatu kama hii tutaweka historia kwamba wastaafu wetu hawawezi kufanya shughuli zao, mtu kama Ludovick Utouh (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-CAG), taasisi yake ya Wajibu ni 'Company Ltd' inakwenda kufa kwa sababu sheria inakwenda kuondoa tafsiri ya company Ltd, sheria ya kampuni ambayo ipo duniani kote," alisema.

Zitto aliongeza: "Maana yake Mkapa, (Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa), Kikwete (Rais mstaafu wa Awamu ya Nne) wasiweze kufanya shughuli yoyote ya kijamii, kina Joseph Butiku (Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere - MNF) waende Butiama, wanataka Kituo cha Sheria cha Haki za Binadamu (LHRC), Twaweza, TGNP na mashirika mengine yafe."

Alisema hiyo ndiyo hatari ambayo wanaiona ndani ya wiki ijayo mjini Dodoma kama muswada huo utawasilishwa bungeni.

Zitto alisema wito wao kwa serikali ni kuuondoa muswada huo bungeni kwa sababu unakwenda

INAENDELEA UK. 8


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALIILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Rose/Daniel Eliewaha Mshana | T 417 DHH Brevis | Makumbusho Yard | 06/07/2019 | RAISSA A/Mart |
| Saidi Idd Lipika | Nyumba yenye Hati | Kibaha -Mlandizi | 13/07/2019 | TAVIR A/Mart |
| Adam Marwa Mwita | Nyumba | Mwanamtoti – Kijichi mbagala | 06/07/2019 | Champion A/Mart |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-**
**RAISA: 0652113262;**
**TAVIR Auctioneer:**
**CHAMPION Auctioneer:**

**TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).**
**0717495311/0718802350**
**0688056805/0742983700**

715292202


## KUELEKEA UCHAGUZI MITAA:

# CCM yawataja Mbowe, Zitto

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kina uhakika wa kushinda kwa asilimia 95 uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, huku kikitamba kuwa katika Uchaguzi Mkuu mwakani, kitachukua majimbo ya Hai na Kigoma Mjini yanayoongozwa na wabunge Freeman Mbowe na Zitto Kabwe, mtawalia.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, alipozungumza na waandishi wa habari.

Polepole alisema katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka huu katika halmashauri zote 185, chama hicho hakitakubali kumpitisha mtu yeyote kugombea kama hajafanya kazi ya kuhudumia wananchi.

Alisema viongozi wote watakaopitishwa na chama hicho kugombea katika uchaguzi huo ni wale tu wenye shughuli za kufanya kwa ajili ya kujiingizia kipato, waliofanya kazi ya kutoa huduma bora kwa wananchi na wenye sifa stahiki.

"Viongozi wote ambao hawakuwajibika kuhudumia wananchi na kushughulika na utatuzi wa kero zao, wasipewe nafasi katika uteuzi wa serikali za mitaa.

"Chama kimeshatoa mwelekeo kwamba viongozi wanaotakiwa kuchaguliwa ni wachapakazi, wenye kazi inayowaingizia kipato, waadilifu, waaminifu, wanyenyekevu, wanaochukizwa na rushwa, wanaojishusha, wazalendo kweli na wakali kwa mambo ya ovyo.

"CCM mpaka sasa ina wanachama zaidi ya milioni 15, na wapigakura wa Tanzania ni milioni 21. Kwa hiyo, tukipiga hesabu kwa wanachama pekee, tunapata kura asilimia 71 ya ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu ujao. Na tukifanya kampeni kuzunguka katika mikoa yote, tunapata kura zaidi

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# China yaipa Tanzania msaada bil. 60/-

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imetia saini mkataba wa kupatiwa fedha za msaada wa Sh. bilioni 60 za Kitanzania kutoka Serikali ya Watu wa China bila ya masharti yoyote.

Katika mkataba huo, taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa vyombo vya habari ilisema kupitia fedha hizo, Serikali ya Tanzania itaamua matumizi yake katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi wake.

Mkataba huo ulitiwa saini na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, kwa niaba ya Tanzania na Makamu Mwenyekiti wa Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la China, Zhou Liujun kwa upande wa Serikali ya China.

Taarifa hiyo ilisema mkataba huo ulitiwa saini baada ya kumalizika kwa mazungumzo kati ya Prof. Kabudi na Waziri wa Mambo ya Nje wa China na Mjumbe wa Baraza la Taifa, Wang Yi.

Mazungumzo ya mawaziri hao yalilenga kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya China na Tanzania sambamba na kuibua maeneo ya kipaumbele na kimkakati yatakayotekelezwa kwa ushirikiano baina ya pande hizo.

Maeneo hayo, kwa mujibu wa taarifa hiyo ni pamoja na upembuzi yakinifu kwa ajili ya upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ili kuwa Taasisi Mahiri ya Tiba ya Moyo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Maeneo mengine ya kimkakati ni ujenzi wa mabwawa ya kuzalisha umeme ya Ruhudji (megawati 358) na Rumakali (megawati 222) yaliyoko Iringa na Njombe ambayo yote kwa pamoja

INAENDELEA UK.8



Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike, akizungumza na viongozi waandamizi wastaafu wa Jeshi la Magereza (kulia), katika Makao Makuu ya Magereza, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Magereza, Uwesu Ngarama, akiwa na Manaibu Kamishna wa jeshi hilo, wakifuatilia mazungumzo ya maandalizi ya uzinduzi wa vitabu viwili vilivyoandikwa na wastaafu wa Magereza. **PICHA: JESHI LA MAGEREZA**.

# Wema arejea uraiani kutoka mahabusu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imemwonya msanii wa filamu nchini, Wema Sepetu, kuacha kuidharau anapokuwa na udhuru badala yake amtumie mdhamini wake kumwakilisha mahakamani.

Aidha, mahakama hiyo imesema kuanzia sasa dhamana yake inaendelea na kesi hiyo itasikilizwa ushahidi wa Jamhuri Julai 4, mwaka huu, dhidi ya tuhuma zinazomkabili za kuchapisha video ya ngono katika ukurasa wake kwenye mtandao wa Instagram.

Amri hiyo ilitolewa jana na

INAENDELEA UK.8

# Wanafunzi 65 wapewa ujauzito kwa miezi sita

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANAFUNZI 65 wa shule za msingi na sekondari mkoani Lindi, wamekatishwa masomo baada ya kupewa ujauzito kwa kipindi kisichopungua miezi sita sasa.

Wilaya ya Kilwa inatajwa kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya waathirika.

Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, ndiye aliyefichua hayo kwenye kikao maalumu cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, kujadili Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Zambi alitaja idadi hiyo kwa lengo la kuunga mkono kauli ya Katibu Tawala wa mkoa huo, Rehema Seifu Madenge, alipoeleza tatizo la watoto wa kike kupewa mimba za utotoni, na kuwa linaendelea kushamiri, hivyo kurudisha nyuma ndoto zao za baadaye.

Zambi alisema wanafunzi hao 65 wakiwamo wawili wenye umri wa miaka 13, wanaosoma darasa la tatu, walipewa ujauzito kuanzia Januari Mosi hadi Juni 20, mwaka huu.

Zambi aliitaja Wilaya ya Kilwa inayoongoza kwa kuwa na mimba 33, Liwale (13), Lindi (9), Nachingwea (6) na Ruangwa (4).

Alisema tatizo hilo linaweza kupungua ikiwa viongozi, watendaji, wazazi na walezi watakuwa tayari kushirikiana na serikali kuwabaini na kutowaficha wanaume wanaohusika na vitendo vya kuwashawishi watoto.

Zambi aliwaeleza madiwani kwamba tatizo la mimba kwa watoto wadogo lisipodhibitiwa, upo uwezekano mkubwa ndoto za watoto wa kike zikaishia njiani, hali itakayosababisha kukosa wataalamu wanaotokana na jinsia hiyo kutoka mkoani Lindi.

"Tutawapataje wataalamu wa kike, wakiwamo manesi na fani mbalimbali ikiwa mimba zinaendelea kushamiri ndani ya mkoa wetu?" Alihoji Zambi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA DODOMA

KONGAMANO LA UWEKEZAJI DODOMA
Tarehe 27 & 28 Juni 2019
UKUMBI WA DODOMA CONVENTION CENTRE (JK HALL)

"Dodoma, Fursa Mpya kwa Uchumi wa Tanzania, Wekeza Dodoma, Tukufanikishe".



Kongamano litaangazia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali za uchumi zilizopo Dodoma kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa lengo la kuwavutia kuwekeza na kufaidika na utajiri mkubwa wa rasilimali zilizopo Dodoma.

Jisajili Sasa Nafasi ni Chache
www.dodomainvestmentforum.or.tz
Email: info@dodomainvestmentforum.or.tz

Kongamano litahusisha:
Hotuba na mawasilisho ya viongozi wa serikali na sekta binafsi
Maelezo ya wawekezaji wa Dodoma kuhusu mafanikio ya miradi yao (testimonials)
Mikutano midogo ya kampuni (B2B)
Maonyesho ya bidhaa na utalii (exhibition)
Kutembelea miradi na "vivutio" ya utalii

KWAMAELEZO ZAIDI:
PIGA SIMU: 0677 300 500
@dodomaforum
dodomainvestmentforum
Tel: 0784 994 615, 0759 003 246, 0787 729 887

DODOMA INVESTMENT FORUM

UN DP
LIC
215291302

# Nchi 35 kushiriki Sabasaba

**Na Mwandishi wa MAELEZO**

NCHI 35 zimethibitisha kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu kama Sabasaba mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade), Edwin Rutageruka, nchi zilizothibitisha kushiriki ni Botswana, Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Ghana, India, Indonesia na Italia.

Alizitaja nchi nyingine zitakazoshiriki kuwa ni Iran, Japan, Kenya, Korea Kusini, Malaysia, Marekani, Misri, Morocco, Nigeria, Pakistani, Palestina, Poland na Rwanda.

Zingine ni Senegal, Singapore, Syria, Sweden, Thailand, Ufilipino, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa falme za Kiarabu (UAE) na Uturuki.

Rutageruka alisema mamlaka yake inaendelea kuhamasisha na kuwasiliana na wafanyabiashara na wawekezaji mbalimbali kuja kuwekeza na kufanya biashara nchini kwa kuwa mazingira sasa ni wezeshi na hayana urasimu.

Kwa upande wa washiriki alisema kampuni zimefikia asilimia 93.3, lengo likiwa ni kukamilisha asilimia 100 kwa kuwa Watanzania pia wanahitajika sana kutangaza biashara zao hasa katika kipindi hiki ambacho washiriki kutoka mataifa mbalimbali duniani watakuwapo.

Kaulimbiu ya Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam mwaka huu ni Usindikaji wa mazao ya kilimo kwa maendeleo endelevu ya viwanda, ambayo inaakisi maono ya serikali ya awamu ya tano ya kukuza kilimo kitakachosaidia maendeleo ya viwanda.

Maonyesho hayo yanatarajia kuanza Juni 28 hadi Julai 13, mwaka huu.

# Mkakati kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula waibuliwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) imeanza mkakati wa kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi baada ya kuanza kuzalisha mbegu za alizeti zilizothibitishwa ubora kwa ajili ya kutumiwa na wakulima na hatimaye kuzalishwa kwa wingi.

Kupitia mkakati huo tayari Kituo cha Utafiti wa Kilimio Ilonga, Kilosa mkoani Morogoro, kimepewa jukumu la kuzalisha mbegu hizo za alizeti ikiwamo ya rekodi ambayo imeanza kutumika kwa wakulima.

Akizungumza katika Siku ya Maonyesho ya Kilimo Biashara yaliyoandaliwa kwa ushirikiano wa Tari na Baraza la Nafaka la Ukanda wa Afrika Mashariki, Mtafiti wa Alizeti nchini, Frank Reuben, alisema kwa mwaka huu wameshazalisha mbegu ya alizeti aina ya Rekodi tani 37.8 ambazo zimeshasambazwa kwa wakulima.

Alisema kupitia uzalishaji mbegu hizo, ekari 18,500 zitapandwa na wakulima katika mikoa mbalimbali ya uzalishaji wa alizeti ikiwamo Singida, Dodoma na Morogoro ambayo imewekewa mkakati wa kulima zao hilo.

Mtafiti huyo alisema kupitia mkakati huo, Tari imepanga kutoa utafiti mwingine wa mbegu ya alizeti itakayokuwa na ubora kuliko mbegu yoyote iliyoko sokoni kwa sasa ili kuongeza uzalishaji wa mafuta maradufu.

"Tari inaendelea na utafiti wa mbegu zingine nne za alizeti kwa ajili ya kuhakikisha uzalishaji wa mafuta unaongezeka hapa nchini," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geoffrey Makamilo, alisema kabla ya kuanzishwa kwa Tari, Kituo cha Utafiti cha Ilonga kilikuwa kinazalisha wastani wa tani 2.3 za mbegu za alizeti lakini kwa mwaka wa kwanza baada ya kuundwa kwa taasisi hiyo, uzalishaji wa mbegu umeongezeka na kufikia tani 7.5.

Dk. Mkamilo alisema mkakati wa Tari ifikapo mwaka 2020-2022 ni kufikisha tani milioni 1.5 za alizeti ambazo zitakuwa na uwezo wa kutoa mafuta ujazo wa tani 600,000 hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa cha uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Mmoja wa wakulima wa alizeti na mzalishaji wa mafuta, Khalifan Hamad, kutoka kata ya Magomeni wilayani Kilosa, alisema mbegu ya 'Rekodi' iliyofanyiwa utafiti na Tari Ilonga imeonyesha kuzaa vizuri na ubora mkubwa utakaosaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini.

Alisema kuwapo kwa kituo cha utafiti pia kumewasaidia kupata ushauri na utaalamu wa kilimo bora cha alizeti tofauti na awali walikuwa wakipanda holela na kukosa mavuno ya kutosha.

Akifungua maonyesho hayo, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema Tari Ilonga ina wajibu wa kuendeleza utafiti katika mazao mengine ya jamii ya nafaka yakiwamo mtama, uwele, ulezi, mbaazi, kunde, choroko, soya, dengu na njugu mawe.



Mtaalamu wa masuala ya kiuchumi, Paulsen Mrina (wa pili kulia), akiwaelezea mameneja rasilimali watu kutoka kampuni mbalimbali jinsi ya kutunza fedha, katika semina ya kuwawezesha kiuchumi iliyoandaliwa na Benki ya Stanbic Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Marekani yasaidia kutungwa kanuni sheria wanyamapori

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Misaada la Marekani (Usaid), limeisaidia serikali kukamilisha kanuni za sheria ya wanyamapori ya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine, inalinda mapito ya wanyamapori maarufu kama shoroba.

Aidha, Usaid kupitia 'Usaid Project' iko kwenye mazungumzo na Mamlaka ya Utafiti wa Wanyamapori (Tawiri), ili kufanya utafiti mwingine wa hali ya shoroba baada ya utafiti wa mwaka 2009 ambao uliainisha uhai wa kila shoroba na kuonyesha ifikapo 2050 zitabaki shoroba mbili.

Shoroba ni mapito ya wanyama kutoka hifadhi moja hadi nyingine kwa ajili ya kutafuta mahitaji yao ikiwamo kwenda maeneo ya mtawanyiko kwa ajili ya kuzaliana na kupata madini muhimu kwa ajili ya miili yao.

Sheria ya Wanyamapori inayosimamia sekta hiyo ni ya mwaka 2009 na toka wakati huo hakukuwa na kanuni ambayo pamoja na mambo mengine inataja ukubwa na namna ya kutunza shoroba ambazo nyingi zimeshavamiwa na shughuli za kibinadamu.

Akizungumza hivi karibuni na Nipashe, Mtaalamu wa Usimamizi wa Maliasili na Sera wa Usaid Protect, Exper Pius, alisema mkutano wa wadau ulifanyika mwaka 2017 na walitoa maoni.

Alisema mchakato ulisimama kwa muda baada ya mabadiliko ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ambaye alitia saini kanuni hizo Machi 16, mwaka jana, ambazo zitasimamia uanzishwaji wa shoroba.

"Kanuni inatambua kuwa maeneo hayo ni ya wananchi, inabidi serikali izungumze na wananchi ili ziwapo na maeneo husika yasibadilishwe hadhi ya umiliki isipokuwa matumizi," alisema.

Alisema kwenye kanuni wananchi watatakiwa kutumia maeneo yao ambayo yanakutwa na shoroba kwa muundo wa uhifadhi endelevu kwa maana ya kuruhusu wanyama kupita wakati wakiendelea na shughuli zao.

"Kazi wanazoweza kufanya ni kama kuchunga mifugo yao na nyingine ambazo haziwezi kuleta mgongano na wanyamapori, mfano wakilima mazao ambayo wanyama watayala moja kwa moja wataingia kwenye mgogoro na wanyama," alisema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, baada ya kanuni kuwepo kuna mambo ya msingi yanatakiwa kufanyika kutokana na maoni ya wadau kuwa kuna mambo ya msingi hayakufanyika.

"Tumeamua kuisaidia serikali kuanzisha mchakato wa kuzitambua shoroba hizo kwa kutumia taratibu zilizopo kwenye kanuni ili kuona mabadiliko kabla ya kutumika rasmi maeneo yote nchini," alisema.

Pius alisema majaribio ya kanuni hizo yanafanyika kwenye shoroba ya Magombera Mwenehana inayounganisha Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa na eneo la asili la Hifadhi ya Magombera hadi Pori la Akiba la Selous, ambayo

INAENDELEA UK.5

## Hatima kesi ya Shamim yasubiri ripoti uchunguzi

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umedai mahakamani katika kesi inayomkabili mmiliki wa Blog 8020 Fashion, Shamim Mwasha (41) na mume wake, Abdul Nsembo(45) ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride unasubiri ripoti ya uchunguzi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Aidha, umedai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kwamba ripoti hiyo ikiwa tayari, Jamhuri utaijulisha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Madai hayo yalitolewa jana na Wakili wa Serikali, Wankyo Simon, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvini Mhina.

Wankyo alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake haujakamilika na bado wanasubiri ripoti ya uchunguzi kutoka kwa Mkemia Mkuu.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Charles Kisoka, alidai kuwa kesi hiyo haina dhamana, hivyo kuomba upande wa Jamhuri kuharakisha upelelezi ikiwamo kufuatilia ripoti hiyo.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa tena Julai 8, mwaka huu, na kuamuru washtakiwa warudishwe rumande.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kusafirisha dawa hizo za kulevya, Mei Mosi, mwaka huu, wakiwa eneo la Mbezi Beach, Kinondoni, jijini Dar es Salaam kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi.

## Hukumu za Tanzania ujangili zapewa tano

**Na Salome Kitomari**

TANZANIA inatajwa kuwa iko vizuri kwenye kuhukumu wanaokutwa na hatia ya kuhusika na ujangili wa maliasili na wanyamapori.

Akizungumza hivi karibuni na Nipashe, Mwanasheria wa Shirika la Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Wanyamapori Tanzania (Traffic), Linah Clifford, alisema ushirikiano wa vyombo vyote vya dola na nia ya kupambana na ujangili kumeiweka Tanzania pazuri.

Alisema kwa nchi za Afrika, Tanzania inaongoza kwa kutoa hukumu ya muda mrefu kama mtu kuhukumiwa miaka 20 au zaidi.

"Tanzania inatajwa kuwa inachukulia kwa uzito na umakini makosa ya wanyamapori maana wapo ambao wamehukumiwa miaka 20 au 30 na wengine ikiunganishwa inafika 50," alisema Clifford.

Kwa mujibu wa mwanasheria huyo, Tanzania ukikutwa na nyara ya serikali kama nyama, ngozi au meno ya wanyamapori, linachukuliwa kwa uzito na vyombo vyote vinashirikiana.

Alisema nchi nyingine kama Malawi, Msumbiji na Uganda zina sheria nzuri, lakini zina hukumu miaka mitano au 10.

"Watuhumiwa wengi wanakimbilia kwenye nchi hizo kuliko akikamatiwe Tanzania bora akakamatiwe au kutenda kosa kwingine kwa kuwa sheria zetu zina meno ya kutosha," alisema.

Aidha, alisema wana miradi zaidi ya 100 ya kupambana na ujangili wa wanyamapori, ikiwamo kutoa mafunzo kwa mahakimu na waendesha mashtaka jinsi ya kuona umuhimu wa kesi za wanyamapori na maliasili.




Baadhi ya wananchi wakiwa kwenye foleni ya kujiandikisha kwa ajili ya kupata vitambulisho vya taifa, nje ya Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), zilizopo jengo la Bima ya Taifa (NIC), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

## Sababu sekta ndogo ya haki jinai kufanyiwa maboresho

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Augustine Mahiga, amesema serikali inafanya maboresho ya sekta ndogo ya haki jinai ili kuendana na kasi kubwa ya mabadiliko duniani.

Balozi Mahiga, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa maboresho ya sekta ndogo ya haki jinai uliowajumuisha wataalama kutoka wizara na taasisi mbalimbali nchini.

Alisema serikali ina wajibu wa kufanya maboresho ya sekta ya haki jinai ili kuendana na wakati wa sasa.

"Ndugu washiriki, nchi yetu na dunia kwa ujumla zimeshuhudia kasi kubwa ya mabadiliko yatokanayo katika nyanja zote za maisha, kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kiteknolojia hali ambayo imesababisha kuwapo kwa mbinu mpya za uhalifu ambazo ushughulikiaji wake unahitaji kuendana na mabadiliko hayo," alisema.

Aidha, alisema kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, wizara na wadau waliona umuhimu wa kufanya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuboresha sekta ndogo ya haki jinai.

Alisema maboresho yanayotarajiwa yatajumuisha maeneo yote yenye changamoto yakiwamo ya kisera, kisheria na kioganaizesheni ili kuufanya mfumo huo kuakisi changamoto za maendeleo za kizazi cha sasa na vijavyo.

Alifafanua kuwa sekta hiyo ndogo ya haki jinai bado inakabiliwa na changamoto kama uchakavu wa majengo ya mahakama ambayo yalijengwa tangu wakati wa mkoloni.

"Lazima tufanye maboresho katika sekta hii, kuna wabunge nimekuwa nikukutana nao wanalalamika kuwa hata mahakama wanazotumia ni zile ambazo zilijengwa na wakoloni," alisema Balozi Mahiga.

## Marekani yasaidia kutungwa kanuni sheria wanyamapori

INATOKA UK 4

inapita kwenye eneo lililohifadhiwa kwa kuchinja.

Alisema uwepo wa maeneo ya hifadhi ya jamii yaani Wildlife Management Area (WMA), kunasaidia kuendelea kuwepo kwa shoroba na kutunza hifadhi dhidi ya uvamizi.

"Lazima tuzitambue shoroba husika kwa kuwa kuna ambazo zimeshakufa kutokana na shughuli za binadamu kwa maana ya mashamba, nyumba na kwa sasa wanyama hawawezi kupita kutoka eneo moja kwenda jingine," alisema.

Mwaka 2017, Nipashe ilifanya habari ya uchunguzi juu ya hali ya shoroba na kubaini kuwa baadhi ya hifadhi kama Hifadhi ya Taifa ya Arusha (Anapa), imebaki kisiwa kutokana na shoroba kuvamiwa na shughuli za kibinadamu na sababu kubwa ni kukosekana kwa kanuni ya sheria ya wanyamapori ya mwaka 2009.

Utafiti uliofanywa na Tawiri mwaka 2009, unaonyesha kuwa uvamizi wa shoroba umesababisha wanyama kuuawa, uwindaji haramu na kusambaa kwa magonjwa ya wanyamapori kwenda kwa wanyama wa kufugwa na kinyume chake pamoja na baadhi ya maeneo yaliyohifadhiwa kuwa kisiwa na wanyama kuzaliana aina hiyo hiyo ambayo ni rahisi kufa kwa ugonjwa au kuwa dhaifu.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Lugola usishangae, chukua hatua sasa*

**TANGU** Mbunge wa Mwibara, Kangi Lugola, ateuliwe kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, amekuwa akitoa maagizo mbalimbali kwa Jeshi la Polisi, lakini mara kadhaa baadaye amekuwa akibaini kuwa hayatekelezwi.

Maagizo yake mengi amekuwa akiyatoa kwa lengo la kumaliza kero mbalimbali za muda mrefu ambazo zinalalamikiwa na wananchi katika maeneo mengi.

Ni jambo la kumpongeza sana Waziri Lugola kwa kujitahidi kufuatilia kwa lengo la kubaini matatizo na kero za muda mrefu ambazo zimekuwa zikiwakabili wananchi.

Waziri huyo amekuwa akitumia ziara zake katika maeneo mbalimbali kwa kuandaa mikutano na kuzungumza na wananchi, huku akiwapa fursa ya kueleza kero mbalimbali, ambazo wamekuwa wakikabiliwa nazo.

Pale anapoelezwa, huwa hasiti kuwauliza maswali mbele ya wananchi wale wote wanaoshindwa kuwajibika na kuwababababisha wananchi kupata usumbufu, hivyo kutoa maagizo ili zimalizwe.

Sio hivyo tu, bali wakati mwingine Lugola amekuwa akifanya maamuzi yakiwamo ya kuwaaadhibu baadhi ya askari na maofisa wa polisi ambao wanasababisha matatizo kadhaa.

Pia amekuwa akieleza kuwa anafanya hivyo kwa kutekeleza kwa vitendo ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020, ambayo pamoja na mambo mengine, inaeleza kuwa serikali itahakikisha inalinda usalama wa raia na mali zao.

Kimsingi, Lugola ametoa maagizo mengi, lakini kubwa ambalo amekuwa akilisisitiza ni polisi kutowanyanyasa wananchi, ikiwamo kuwabambikia kesi na kuwaweka katika vituo bila kuwafikisha mahakamani.

Waziri huyo, juzi alieleza kushangazwa na kuona mahabusi 11 waliofutiwa kesi mahakamani kuwekwa katika Kituo cha Polisi Gogoni, Wilaya ya Kipolisi Kimara jijini Dar es Salaam kwa zaidi ya miezi sita kinyume cha sheria.

Lugola alieleza hayo alipofanya ziara ya kushtukiza katika kituo hicho kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya kuwapo kwa baadhi ya vituo vya polisi vinavyokaa na watuhumiwa kwa muda mrefu bila kuwafikisha mahakamani.

Alisema katika kituo hiki cha Gogoni taarifa nilizokuwa nazo kinaongoza kwa kuwashikilia watuhumiwa na kukaa nao kwa muda mrefu bila kuwafungulia mashtaka mahakamani.

Kwamba baada ya kufika katika kituo hicho, alikutana na mahabusi 32, na kuwahoji mmoja baada ya mwingine kisha mahabusi 11 waliofutiwa kesi zao.

Lugola alisema watuhumiwa hao 11 wanakabiliwa na kesi za mauaji, na kuwa miongoni mwa alivyowahoji wengine wamekaa gerezani miaka saba na baada ya muda huo sasa mahakama imewarudisha katika vituo vya polisi kufuata kesi zao.

Alisema wana miezi sita katika kituo hiki, hivyo, kama waziri, hiyo sio sawa.


Tunaona kuwa hii siyo sawa, na pengine ndio maana wakati mwingine mahabusi wanateseka na kuamua kugoma, kutokana na kuona wamenyimwa haki yao ya msingi ya kufikishwa mahakamani.

Tunamshauri Waziri Lugola asiwe analalamika anapobaini maagizo yake yamepuuzwa, bali aanzishe utaratibu mzuri wa kufuatilia utekelezaji wa maagizo anayoyatoa.

Pia aweke utaratibu wa kuwasiliana na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuhakikisha kesi za jinai zinapelekwa mahakamani kwa wakati mwafaka.

Ili kumaliza matukio haya, itakuwa vizuri jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya waziri likakabidhiwa kwa wakuu wa polisi wa wilaya na mikoa, ili wawe wa kwanza kuwajibika ikiwa mambo yatakuwa kinyume chake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

## *Serikali izungumzie kusuasua ununuzi pamba ya wakulima*

**MSIMU** mpya wa ununuzi wa pamba ulizinduliwa rasmi Mei 2, mwaka huu mkoani Katavi, huku serikali ikitangaza bei mpya ya zao hilo kuwa Sh. 1,200 kwa kilo.

Hilo ni ongezeko la Sh. 100 kwa kulinganisha na bei ya msimu uliopita ambayo ilikuwa ni Sh. 1,100 kwa kilo.

Kuzinduliwa kwa msimu huo kulifungua rasmi ununuzi wa zao hilo karibu katika maeneo yote yanayolima, ukianzia na Kanda ya Ziwa inayoundwa na mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mara, Geita, Mwanza na Kagera.

Ipo pia mikoa katika baadhi ya kanda inayolima zao hilo, kama Tabora ulio Kanda ya Magharibi na Singida ulio Kanda ya Kati.

Katika mlolongo huo unaingia mkoa wa Katavi, ambao kimsingi uko katika msimu wake wa pili wa kilimo hicho tangu kianzishwe mkoani humo.

Pamoja na changamoto mbalimbali ambazo wakulima wamekuwa wakikumbana nazo, rekodi zinaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, wakulima wamehamasika kuongeza uzalishaji.

Kwamba changamoto za upatikanaji usio wa uhakika wa pembejeo kwa wakati na huduma za ugani unaotokana na uchache wa maofisa ugani kwa kutaja baadhi, hazikukwamisha juhudi zao.

Na ndiyo maana kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba (TCB), Marko Mtunga, uzalishaji wa zao hilo kwa mwaka huu unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia zaidi ya tani 400,000 kutoka takribani tani 200, 000 za msimu uliopita.

Hii inathibitisha namna wakulima wa zao hilo la kibiashara linalotegemewa na wengi walivyohamasika kuongeza tija katika uzalishaji, japokuwa bado ekari moja ya pamba kwa wastani inatoa kilo 300 kwa sasa.

Kuna uwezekano hata hivyo wa ekari moja kutoa kilo 1000, iwapo changamoto zilizopo zitatatuliwa.

Pamoja na juhudi hizo za wakulima za kuongeza tija wakiamini watapata kipato cha kuonekana katika dhima nzima ya kupambana na umaskini kwa ujumla wake, kuna taarifa kwamba ununuzi wa zao hilo ni wa kusuasua.

Bado kuna pamba nyingi ya wakulima haijanunuliwa kabisa hadi sasa karibu miezi miwili tangu kuzinduliwa kwa msimu na kampuni za ununuzi zikionekana kutotoa kipaumbele kinachostahili.

Kwamba wakulima wa zao hilo wamebaki wameduwaa wakisikilizia kampuni za ununuzi ziinunue pamba yao!

Muungwana akiwa ni miongoni mwa watu wanaotoka Kanda ya Ziwa anadhani kuna haja ya serikali kuingilia kati suala hili sasa.

Anasema hivyo kwa sababu inaonekana kwenye kadhia hii ya pamba ni kama vile inataka kufanana na sakata lililotokea kwenye zao la korosho.

Ikumbukwe kuwa kabla ya serikali kuingilia kati suala la ununuzi wa korosho, wanunuzi wa zao hilo walitaka kuinunua korosho kwa bei ya chini ya shilingi 3,000, ambayo ilikuwa haiwalipi wakulima.

Kuna maeneo ambayo tayari baadhi ya wanunuaji wa pamba walikuwa wameshaanza kununua kwa bei ya chini ya shilingi 1,000 kwa kilo, hali iliyowafanya baadhi ya wakuu wa wilaya kuingilia kati na kupiga marufuku kitendo hicho.

Kilio cha kusuasua kwa ununuzi wa zao hili kimeibuliwa pia bungeni na Mbunge wa Sumve, Richard Ndasa ambaye ameitaka serikali iingilie kati suala hili kwani hali ya kiuchumi ya wakulima wa pamba walio wengi si nzuri.

Si nzuri katika mantiki ya kawaida tu kwamba wanategemea pamba ili waishi na kwamba pamba kwao ni siasa vilevile, sasa kama pamba yao hainunuliwi, maendeleo yao ya kimaisha yatakuwa ndiyo yanakwamishwa hivyo.

Pengine wakati umefika kwa serikali kuchukua uamuzi sasa kuhakikisha pamba ya wakulima inanunuliwa, tena kwa bei iliyotangazwa ili kuboresha maisha ya wakulima hawa.

Ieleweke kwamba wakulima hawa wametumia raslimali zao, nguvu zao na muda kuzalisha pamba wakitarajia waiuze ili watatue matatizo yao ya kiuchumi.

Sasa danadana zinapoanza kutoka kwa wanunuaji inakuwa haieleweki, hivyo ni vyema serikali ikasema katika hili.

## BARUA/MJADALA

### BARUA YA WAZI KWA MKURUGENZI MKUU WA VETA; Chuo cha Veta Oljoro kimulikwe

**Mhariri**

TUNAOMBA chuo hiki kiangaliwe mwenendo wake, kwani kuna masuala kadhaa yanayotia shaka katika utendaji wake.

Mojawapo ni matumizi mabaya ya fedha/raslimali za umma. Mfano mwaka huu wa 2019, mnamo msimu wa kilimo, chuo kilitumia fedha nyingi kulima eneo lote la mashamba ya chuo yapatayo ekari 1000 hivi.

Lakini kikapanda mazao eneo dogo tu la karibia ekari 100 hadi 150, huku eneo lingine likiachwa bila ya kupandwa chochote, wakati fedha nyingi imetumika kuliandaa.

Aidha, sehemu ya eneo hilo imekuwa ikigawanywa na kupewa wananchi walime ili kujikimu kwa chakula.

Lakini mwaka huu hawakupewa kwa madai ya kuwa chuo kimeamua kulilima eneo lake lote, lakini matokeo yake eneo kubwa likaachwa bila kupandwa zao lolote. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Tatizo jingine ni matumizi mabaya ya ofisi na utendaji usiozingatia na mifumo na taratibu zilizowekwa. Mfano, hata maamuzi ya kulima eneo lote la mashamba ya chuo, hayakuzingatia taratibu zilizowekwa.

Kwamba kamati ya shamba iliyopo kwa mujibu wa taratibu na ile ya uzalishaji mali, hazikuhusishwa kikamilifu katika kufikia uamuzi wa kulima shamba lote, badala yake watu wachache tu ndio waliamua kufanya hivyo.

Suala lingine ni ubadhirifu wa fedha za umma. Mathalani hivi karibuni mwaka huu ulifanyika ukarabati wa majengo kadhaa (bwalo la chakula pamoja na tangi la maji kwa ajili ya akiba).

Kazi hizo ambazo zote zingaliweza kufanywa kwa kutumia rasilimali watu wa ndani, badala yake mafundi waliajiriwa kutoka nje kukarabati majengo ya chuo, wakati chuo chenyewe ni chuo cha ufundi.

Kwa kutumia ujuzi wa ndani, chuo kingeliweza kutumia gharama ndogo, lakini kwa vile mafundi wa nje hutoa chochote kwa mtoa kazi, walipewa kazi hizo ambavyo hata hivyo zilifanyika chini ya kiwango.

Yaani hata miezi mitatu haijaisha, tayari sakafu iliyowekwa upya bwaloni imeshaanza kubomoka.

Aidha, tangi la maji ya akiba hadi sasa bado halina msaada wowote wa kuhifadhi maji ya akiba kwani bado linavuja, licha ya kukarabatiwa, hali ambayo huchangia shida ya maji chuoni hasa pale maji yanapokatika tu kwa muda mfupi.

Hali hii mara kadhaa imeathiri mwenendo wa mafunzo.


Ni vema mamlaka husika zikamulika taasisi hii ya mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa.

**Mzalendo Mwananchi, Arusha**

### WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Wanafunzi kumiliki simu shuleni kudhibitiwe kusiathiri masomo yao




**Na Sabato Kasika**

MOJA ya changamoto ambazo zimekuwa zikichangia kuharibu maendeleo ya kielimu kwa baadhi ya wanafunzi shuleni ni matumizi mabaya ya simu za mkononi, ambayo yanasababisha mmomonyoko wa maadili kwao.

Kutokana na hali hiyo ni vyema matumizi hayo yadhibitiwa kwa ushirikiano kati ya wamiliki wa shule, walimu na wazazi kwa kusimamia vizuri sheria zinazowabana wanafunzi kumiliki simu.

Ni wazi kwamba simu katika dunia ya leo haikwepeki, si kwa watoto, vijana na wazee, lakini ni muhimu kuweka utaratibu wa matumizi, kuhakikisha matumizi hayo hayawezi kuwaathiri watoto wakiwamo wanafunzi.

Katika kipindi hiki cha utandawazi, mawasiliano ni muhimu kwa kila mmoja, ingawa yana madhara na faida zake, na wanaopata madhara ya matumizi ya simu ni wanafunzi.

Wanafunzi wamekuwa wakidaiwa kutumia simu hizo vibaya ikiwamo kuangalia picha za ngono, ambazo huwatoa kwenye mstari na kujikuta wakiingia katika mambo ya mahusiano ya kimapenzi.

Ninajua kwamba ni vigumu kuwazuia wanafunzi kutumia simu kuwasiliana na wazazi wao, lakini ni vyema kukawekwa sheria kali zitakazowafanya watumie simu vizuri.

Kunaweza kuwekwa utaratibu wa shule kupata simu moja au mbili, ambazo zitatumiwa na wanafunzi kuwasiliana na wazazi wao mara wanapohitajika shuleni.

Hapa msingi mkubwa ni nidhamu kwa mwanafunzi, kwani ndio chachu ya mafanikio yake, hivyo ni muhimu walimu na wazazi kufuatilia kwa karibu nidhamu za wanafunzi wawapo shuleni na hata nje ya shule.

Simu inaleta madhara kwa wanafunzi kutokana na ukweli kwamba ni chanzo cha kufeli mitihani yao, kwa vile baadhi yao hutumia muda wa kujisomea kwa kuongea na simu na wapenzi wao au kuchati na rafiki zao.

Kwa wale ambao watakuwa wanakumbuka, hata Waziri Selemani Jafo aliwahi kukemea hilo alipotembelea Shule ya Sekondari Jangwani jijini Dar es Salaam na kuwaambia wanafunzi ukweli kuhusu kufanya vibaya katika mitihani yao.

Ilikuwa ni mwaka jana alipowapasha kuwa baadhi yao wanatumia simu za Whatsapp kuangalia picha zisizo na maadili na kujihusisha na mambo ya uasherati na kwamba katika mazingira hayo elimu haiwezi kuwa rafiki yao.

Kwa kauli hiyo ya waziri ni vyema ikawaamusha wazazi na walezi ili waone kwamba, kuna haja ya wao kujiongeza na kufuatilia hatua kwa hatua nyendo za watoto wao, kwani inadaiwa kuwa wapo baadhi ya wanafunzi wanaomiliki simu bila wazazi kujua.

Wapo pia wanaomiliki simu ambazo wazazi wao hawana uwezo wa kuzinunua, hawa wote wanatakiwa kuelimishwa ili kutambua faida na hasara ya kumiliki simu wakiwa bado wanafunzi.

Kama kweli mtoto anaweza kumiliki simu ambayo mzazi hana uwezo wa kuinunua, maana yake kuna swali kubwa la kujiuliza hapa kwamba ni kwanini iwe hivyo na mwisho wake ni upi?

Kumekuwapo na mjadala kuhusu matumizi ya simu shuleni huku baadhi ya watu wakidai kwamba zinachangia wanafunzi kufanya vibaya na wengine wakisema zinawasaidia kuperuzi vitu mbalimbali vinavyohusu masomo.

Lakini ukweli unabaki palepale kwamba wanazitumia vibaya na mwisho wa siku kuwaharibia malengo yao katika masomo, hivyo ipo haja ya kuangalia upya mtindo wa baadhi ya wanafunzi kwenda nazo shuleni.

Kama nilivyosema awali kwamba ni vigumu kuwazuia wanafunzi kutumia simu kuwasiliana na wazazi wao, bali kinachotakiwa ni kuweka sheria kali zitakazowafanya watumie simu vizuri.

Shule inaweza kuweka utaratibu wa kupata simu moja au mbili, ambazo zitatumiwa na wanafunzi wote kuwasiliana na wazazi wao mara wanapohitaji kufanya hivyo shuleni, kuliko kuwaacha wajifanyie kienyeji.

Ninajua sheria za elimu haziruhusu wanafunzi kuwa na simu shuleni, lakini wajanja wachache wamekuwa wakienda nazo na ndio maana hata Waziri Jafo alibaini hilo na kulikemea.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



HABARI KITAIFA

# CCM yawataja Mbowe, Zitto

INATOKA UK.2

ya asilimia 90," Polepole alisema.

Kiongozi huyo alisema Kamati Kuu ya chama hicho inatarajiwa kukutana leo na makatibu wa chama hicho kutoka mikoa yote na kesho inatarajiwa kufanya kikao chake kikiongozwa na Mwenyekiti, Dk. John Magufuli na keshokutwa itatembelea miradi mbalimbali.

**MBOWE, ZITTO**

Polepole alisema anaamini CCM mwakani itaibuka na ushindi katika majimbo mengi ambayo sasa yanaongozwa na upinzani, yakiwamo Hai na Kigoma Mjini ambayo Mbowe na Zitto wanayashikilia.

Alidai Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimekuwa kikiwaaminisha Watanzania kwamba mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ni ngome yake, lakini anaamini dhana hiyo itafutika mwakani.

Polepole alidai kufanya vizuri kwa Chadema katika mikoa hiyo kulitokana na kutoelewana kwa wanachama na viongozi wa CCM katika maeneo hayo.

Alidai kutokana na kumalizika kwa tofauti hizo kulikokwenda sambamba na kurejea kwa Waziri Mkuu mstaafu Edward Lowassa, hakuna jimbo hata moja katika uchaguzi ujao ambalo litakwenda upinzani kwenye mikoa hiyo.

Alidai Mbowe amekuwa akipiga kelele kwamba vyama vya siasa vimezuiwa kufanya mikutano ya hadhara wakati hata katika jimbo lake lenyewe haendi kufanya mikutano hiyo.

"Chama cha Mbowe kimeanza kusema kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeanza kuandikisha daftari la wapigakura katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro ili kuwanyima haki wapigakura katika mikoa hiyo kwa sababu ni ngome ya Mbowe, nani kakwambia Arusha na Kilimanjaro ni ya Mbowe?" Polepole alihoji.

"Na kinachotaka kuwaaminisha ionekane kwamba kule kulikuwa ni ngome ya Chadema, kulitokana na tofauti zilizotokea kwa baadhi ya wanachama wetu kuhama ambao hata hivyo tayari wamesharudi.

"Upinzani umeingia Kilimanjaro na Arusha kutokana na tofauti zilizotokea ambazo hata walioongoza tofauti hizo tayari wamerudi akiwamo mzee wetu mstaafu. Kwa hiyo, mikoa hiyo haijawahi kuwa ngome ya upinzani na mimi nataka kuwaambia kuwa 2020 hakuna atakayebaki huko."

Polepole pia alimtumia salamu Zitto, akidai naye ajiandae kuondoka katika jimbo lake kwa kuwa amekuwa akitoa taarifa alizodai za uongo.

"Unawezaje kusema uchumi umeporomoka wakati serikali inaendesha miradi yake na kufanya mambo makubwa ya maendeleo ikiwamo kununua ndege, kutengeneza barabara, reli na mengine kwa kutumia pesa yake ya ndani?

"Tunamtaka huyu ndugu yetu Zitto atafute kazi ya kufanya badala ya kuendelea kuwadanganya wananchi. Na tulishamwambia kwamba katika jimbo lake lile ajiande kutafuta kazi nyingine kwa sababu 2020 harudi," Polepole alitamba.



Balozi wa Tanzania nchini Kenya, Dk. Pindi Chana (kushoto) akiingia kufungua mafunzo ya kujijengea uwezo wanawake wajasiriamali toka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF), Mama Anna Mkapa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zitto Kabwe aushtukia muswada wa Azaki

INATOKA UK. 2

kuua biashara.

Zitto ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini, alidai kuwa kwa kuonyesha muswada huo unahila, umepelekwa bungeni kama hati ya dharura ili usomwe mara ya kwanza, ya pili, ya tatu ndani ya siku tano.

"Leo (jana) wabunge wanamaliza kujadili bajeti, kesho (leo) tunaipigia kura, Jumatano tunakwenda kujadili Sheria ya Fedha, Alhamisi tunajadili mgao wa fedha, Ijumaa Bunge linaahirishwa, kwa hiyo sheria hii yenye kubadili sheria zote ambazo ni Sheria ya Kampuni, Sheria ya Bodi ya Wadhamini, NG'O na pia kuna mabadiliko mengine yanakuja ya Sheria ya Filamu ili kudhibiti," alidai na kuendelea:

"Tunapitisha sheria za hatari, ambazo zitajadiliwa siku moja ili kuhakikisha kwamba wanapitisha kile ambacho wamekikusudia."

Zitto alisema akiwa Mbunge na Kiongozi wa ACT-Wazalendo anatoa wito kwa serikali iachane nazo kwa sababu hazina maana yoyote.

"Sheria hizi zitazuia uhuru wa

INAENDELEA UK. 26

# China yaipa Tanzania msaada bil. 60/-

INATOKA UK.3

yatakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa takribani megawati 580, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa na ukarabati wa reli ya Tazara.

Aidha, katika mazungumzo yao, serikali ya China imeahidi pia kuunga mkono katika ujenzi wa miundombinu muhimu katika mji mpya wa serikali katika makao makuu Dodoma.

Taarifa hiyo pia ilisema Waziri Wang alisifu uhusiano mwema na wa kirafiki baina ya Tanzania na China na kuongeza kuwa Tanzania imekuwa rafiki wa kweli wa China kwa wakati wote.

Prof. Kabudi kwa upande wake, aliishukuru serikali ya China sambamba na kueleza kuwa kipaumbele cha Tanzania ni kudumisha na kuendeleza uhusiano mzuri wa kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi uliopo baina ya nchi hizo mbili kwa manufaa ya pande zote mbili.

Pia Prof. Kabudi alipongeza serikali ya China na nchi za Afrika kwa kuandaa mpango kazi wa kimkakati ambao umeainisha maeneo 10 ya kipaumbele yakiwamo uendelezaji wa sekta ya viwanda na miundombinu ambayo kwa Afrika hususan Tanzania ndicho kipaumbele cha kwanza.

Maeneo mengine ya kipaumbele ni pamoja na uendelezaji wa biashara na uwekezaji kati ya China na Afrika pamoja na ushirikiano katika maeneo ya ulinzi na usalama.

## Wema arejea uraiani kutoka mahabusu

INATOKA UK 3

Hakimu Mkazi Maira Kasonde, wakati akitoa uamuzi wa kufutiwa dhamana au la katika hoja zilizowasilishwa na mawakili wa pande zote mbili.

Alisema baada ya kupitia hoja za Jamhuri kwamba Wema alifikishwa mahakamani hapo Juni 17, mwaka huu, akiwa chini ya ulinzi na kiapo cha utetezi, mahakama yake imejiridhisha kwamba alivunja masharti ya dhamana.

Alisema kiapo cha mshtakiwa kinaonyesha sababu za kushindwa kufika mahakamani kwamba alipata ugonjwa baada ya kufika vinunga vya mahakama hiyo.

"Swali ni kwa nini alishindwa kuijulisha mahakama wakati alikuwa eneo la mahakama? Kutokuwapo kwako mahakamani lazima umjulishe mdhamini wako ambaye ana wajibu wa kuhakikisha unafika kusikiliza kesi yako na si wakili," alisema na kuongeza kuwa:

"Mahakama yangu inakupa onyo, mdhamini wako anatakiwa kuwajibika pale unapokuwa na udhuru wa kuja kutoa taarifa. Dhamana yako inaendelea na kesi inaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Julai 4, mwaka huu," alisema Hakimu Kasonde wakati akitoa uamuzi wa kumwachia kwa dhamana huru msanii huyo.

Juni 11, mwaka huu, mahakama hiyo ilitoa hati ya kukamatwa Wema baada ya kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yake.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Silvia Mintanto, kuomba hati ya kukamatwa msanii huyo.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Reuben Semwanza, alidai kuwa mshtakiwa alifika mahakamani kusikiliza kesi yake lakini alipatwa na ugonjwa wa gafla.

Juni 17, mwaka huu, mahakama iliamuru mshtakiwa huyo kwenda mahabusu hadi jana alipoachiwa kuendelea na dhamana.

Katika kesi ya msingi, Wema (30), anadaiwa kuwa Oktoba 15, 2018 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alichapisha video ya ngono na kuisambaza katika mtandaoni wake wa kijamii wa Instagram.

## Mbunge aibua tuhuma za rushwa

INTOKA UK. 2

ya kuja kutoa uelewa kuhusu suala hilo.

"Kwa hiyo, kama kilikuwapo ama kilikuwa vipi, chochote kilichoongelewa huko, ofisi haina taarifa," Dk. Tulia alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema hakuna haki yeyote ya Bunge katika matukio hayo iliyovunjwa ambayo inaweza kusababisha chombo hicho kiache kufanya shughuli zake na tujadili jambo la dharura.

Jumamosi, asasi za kiraia Tanzania takriban 30 zilikutana na Waandishi wa habari jijini Dodoma na kutoatamko zikitahadharisha kuwa mabadiliko ya sheria yanayotarajiwa kufanywa na Bunge hivi karibuni hayatakuwa na matokeo chanya na yanakwenda kuzikandamiza asasi hizo.

Katika tamko lao, viongozi wa asasi hizo walidai mabadiliko hayo yakipitishwa, hakuna asasi hata moja itakayokuwa salama na huo utakuwa mwisho wa ajira nyingi za Watanzania na serikali kukosa kodi.

Viongozi hao waliishauri serikali itoe walau muda wa miezi sita ili kujadiliana zaidi na wadau kabla ya kupitisha kuwasilisha muswada huo bungeni, huku wakiweka wazi kuwa wamepanga kwenda mahakamani kudai haki waliyoiita ya wanyonge.

HABARI MIKOANI

# Mkapa, wenzake kutembelea shule kongwe yao ya zamani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, anatarajiwa kuungana na wahitimu wengine wa Shule kongwe ya Sekondari Ndanda ya Masasi, mkoani Mtwara kuitembelea shule yao Septemba 27, mwaka huu, kwa ajili ya siku ya wahitimu wa shule hiyo iliyoanzishwa miaka 91 iliyopita.

Mkapa aliyesoma Ndanda katika miaka ya 1950, alithibitisha kuungana na wahitimu wengine wa shule hiyo alipokutana na kuzungumza na viongozi wa Umoja wa Wahitimu wa Shule ya Sekondari Ndanda (UWAHISSENDA) waliokwenda kuutambulisha umoja wao ofisini kwake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Alisema kama mmoja wa waliobahatika kusoma Ndanda, anajiona ana wajibu wa kuungana na wana umoja wengine walioanzisha wazo la kuitembelea shule yao ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wa shule katika maisha yao.

"Hili ni wazo la kupongezwa sana. Hongereni kwa ubunifu na uthubutu wa kutambua umuhimu wa kule mlikopata elimu. Ni wachache sana wanaokumbuka mambo kama haya," alisema Mkapa huku akiahidi mwaka huu ataungana nao.

Kwa wahitimu hao, hii itakuwa mara ya pili kurejea Ndanda, kwani mwaka jana walikwenda kwa mara ya kwanza na kuzindua umoja wao wakiwa shuleni hapo na kukabidhi vitabu vyenye thamani ya takribani Sh. milioni 5, kupanda miti, kuzungumza na wanafunzi wa sasa na pia kushiriki katika shughuli mbalimbali shuleni hapo, ikiwa ni pamoja na kufyatua matofali.

Mwenyekiti wa umoja huo, Yohana Kasawala, alimshukuru Mkapa kwa kuridhia kuwa mwanachama mpya, lakini kipekee kwa kukubali kuungana na wanafunzi wengine wa zamani kwa safari ya shuleni Ndanda. Aliwataka wahitimu wengine kuona fahari ya kusoma Ndanda na hivyo wajitokeze kufanikisha Siku ya Wahitimu Ndanda.

Umoja huo uliasisiwa mwaka 2015 kupitia mtandao wa kijamii wa Whatsapp na una wanachama hao zaidi ya 150, wakiwa na malengo ya kutanua wigo wa ukaribu hata baada ya kuhitimu masomo yao, kuinuana kiuchumi na pia kushiriki katika kuijengea uwezo shule yao.

"Daima umoja ni nguvu, utengano ni dhaifu, nasi tumeona ni vyema tukatumia mshikamano huu kama fursa ya kujiimarisha kiuchumi. Tuna ndoto nyingi...ni suala la muda tu, lakini mwelekeo wetu ni mzuri na kwa sasa tunafikiria kuanzisha kampuni ya mikopo midogomidogo yaani Microfince company. Siku za usoni tunaweza kufikiria hata kuanzisha benki," alisema Kasawala.

Ndanda, shule yenye historia ndefu kielimu, iliyoanzishwa mwaka 1928 na imeshatoa wahitimu zaidi ya 15,000 waliobahatika kushika nyadhifa mbalimbali katika nchi, akiwamo Mkapa. Hawa Ghasia, mmoja wa mawaziri waandamizi katika Serikali ya Awamu ya Nne na Subira Mgalu, Naibu Waziri.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (wa tatu kushoto), akimsikiliza mmoja wa wajasiriamali waliowezeshwa na GGM kwa kupitia kampeni ya Kilimanjaro Challenge, anayefuata ni Makamu wa GGM, Simon Shayo. Zaidi ya watu 65 walishuka Mlima Kilimanjaro baada ya kuupanda Juni 15, mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali ya wilaya kujengwa Ikungi

**Na Salome Kitomari**

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida, katika mwaka wa fedha 2019/2020, itajenga hospitali ya wilaya itakayotoa huduma zote muhimu za afya.

Akizungumza jana kwa njia ya simu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema fedha za ujenzi huo zitatolewa na Serikali Kuu na halmashauri ikiwamo nguvu za wananchi.

Alisema hospitali hiyo itakuwa ya kwanza baada ya miaka yote kukosekana kwa hospitali inayomilikiwa na serikali kwa ajili ya kufikisha huduma za afya kwa bei nafuu kwa wananchi wote.

"Kwa sasa tuna hospitali mbili za wilaya zinazomilikiwa na taasisi za dini, tumeona ni muhimu sana kujenga hospitali ya serikali ambayo itatoa huduma zote muhimu," alisema.

Kwa mujibu wa Kijazi, huduma zitakazotolewa ni upasuaji mkubwa na mdogo, na huduma nyingine ambazo wananchi walikuwa hawazipati kirahisi.

Aidha, katika kuboresha huduma za afya, serikali iliipatia halmashauri hiyo fedha za ukarabati na upanuzi wa vituo viwili vya afya vya Ihanja na Sepuka kwa kutumia mafundi jamii.

Hivi karibuni, Kijazi alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 1.13 ambazo Sh. milioni 500 zilikarabati na kupanua kituo cha Ihanja ambacho kimewekewa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 230.

Kadhalika, ukarabati unaendelea katika kituo cha Sepuka na kiasi cha Sh. milioni 400 zimetolewa, ili kuweza kutoa huduma za dharura na upasuaji, na kwamba ungetumika utaratibu wa zamani gharama ingekuwa mara mbili.

Wilaya ya Ikungi ilianzishwa mwaka 2010 ina vituo vya afya 43, zahanati 38 ikiwa ni 34 za serikali na tatu za taasisi za dini pamoja na vituo vya afya vitatu.

# Burunge yarejesha uhai kwenye shoroba

**Na Salome Kitomari**

HIFADHI ya Wanyamapori ya Burunge (Wildlife Management Area (WMA), imefanikiwa kurejesha uhai kwenye mapito ya wanyama 'shoroba' inayounganisha hifadhi za taifa Tarangire na Ziwa Manyara.

Katibu Mtendaji wa Burunge WMA, Benson Mweise, aliwaambia waandishi wa habari wa Tanzania na Thailand, walio kwenye programu maalum ya kuandika habari za ujangili na uhifadhi iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Alisema idadi ya wanyama wanaopita kwenye shoroba hiyo imeongezeka kutokana na jitihada za kutunza ikiwamo kumalizika kwa ujangili wa tembo na faru.

"Zamani ilikuwa ni vigumu wanyama kupita kirahisi kutoka Tarangire hadi Ziwa Manyara, lakini kwa sasa wanapita na tunawaona wengi, hii ni habari njema kuwa shoroba ina uhai," alisema.

Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (Tawiri), mwaka 2009 ulionyesha kuwa ifikapo mwaka 2050 Tanzania itabakiwa na shoroba mbili, kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu.

Aidha, wanyama wanaozaliana kizazi hicho hicho itaongezeka, huku wakishindwa kuhama kutoka hifadhi au eneo lililohifadhiwa kwenda jingine pamoja na maeneo ya mtawanyiko.

Katibu huyo alisema tangu kuanzishwa kwa WMA hiyo mwaka 2003 ikiwa na kilomita za mraba 283 na vijiji kumi wanapata fedha ambazo hugawanywa kwenye vijiji kwa ajili ya shughuli za maendeleo na nyingine kubaki kwa ajili ya uendeshaji.

Alisema mwaka 2017/18 walipata Sh. bilioni 2 ambazo Sh. bilioni 1 ilibaki Burunge na nyingine ziligawanywa kwa kila kijiji ambavyo vilipata Sh. milioni 103 kila kimoja.

Alisema shughuli zinazofanyika kwenye eneo la hifadhi ni utalii wa picha na uwindaji, na kwamba kuna wawekezaji saba.

Naye Spika wa kwanza wa Burunge, Noah Teveli, alisema ongezeko la watu ni changamoto kubwa kwa kuwa ardhi ni ile ile na kwamba imesababisha uwepo wa migogoro baina ya WMA na wananchi.

# Athari mazingira zaathiri ufukwe Tanga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa eneo la ufukwe lililopo Jiji la Tanga linakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo athari za kimazingira kama vile utupaji holela wa taka hasa za plastiki.

Aidha, taka hizo huletwa na mifereji ya maji ya mvua inayoingia baharini kutoka maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Sima, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Konde (CUF), Khatib Said Haji.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zimesababisha uharibifu mkubwa katika Bandari ya Tanga eneo la 'Deep Sea' lango kuu la kuingia na kutokea katika bandari hiyo.

"Je, serikali inachukua hatua gani za dharura kudhibiti uharibifu huo?" Alihoji.

Naibu Waziri Sima alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zinatofautiana katika maeneo mbalimbali nchini yakiwamo maeneo ya ukanda wa Pwani ambayo ni muhimu kwa shughuli za uchumi.

"Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuchukua hatua za makusudi katika kukabiliana na athari hizo ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2007 na Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012," alisema.

Sima alisema mipango hiyo imeelekeza hatua za haraka za kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sekta muhimu zikiwamo maji, maliasili, miundombinu, afya, nishati, ukanda wa pwani na maeneo ya bahari.

Pamoja na hayo, Sima alisema hatua zilizochukuliwa na serikali na Halmashauri ya Jiji la Tanga katika kuhifadhi na kulinda eneo hilo dhidi ya uchafuzi wa mazingira ni pamoja na kufanya kampeni za usafi wa mazingira kwa kuhusisha wavuvi, wafanyabiashara na vikundi vya mazingira.

Alitaja kampeni nyingine kuwa ni kutoa elimu kwa wavuvi na wadau wengine katika eneo hilo kuhusu usafi wa mazingira na kuhifadhi miti na uoto wa asili kuzunguka fukwe hizo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akitoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngoro Malenya, wakati wa uzinduzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Ulanga mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba nchini, Stela Tulo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**.

## Ujenzi bandari kavu Inyala waiva

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), katika mwaka 2019/20 imepanga kuanza kujenga bandari kavu katika eneo la kimkakati la Inyala, Mbeya ili kuhudumia wateja wa Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Chongo (DRC).

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Atashasta Nditiye, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbeya Vijijini (CCM), Oran Njeza.

Mbunge huyo alisema katika kukabiliana na ushindani na bandari za nchi jirani, TPA ina mpango wa kuanzisha bandari kavu katika eneo hilo la kimkakati kwa Wilaya ya Mbeya.

"Je, ni lini tathmini ya fidia kwa wananchi itakamilika? Je, ni lini ujenzi wa bandari kavu ya Inyala utaanza? Na je, kuna mkakati wa ujenzi wa reli kuunganisha bandari kavu ya Inyala na bandari ya Itungi (Kyela)?"Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Nditiye alisema bandari hiyo pia itahudumia wafanyabiashara wa Tanzania kutoka Nyanda za Juu Kusini ili kukabiliana na ushindani na bandari za nchi jirani.

"Katika bajeti ya mwaka 2019/20, TPA imepanga kufanya upembuzi yakinifu katika eneo lenye ukubwa wa ekari 100, ili kubaini mahitaji halisi na eneo linalofaa kwa ajili ya kujenga bandari kavu," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kukamilisha zoezi hilo uthamini utafanyika na baada ya kukamilika taratibu za kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huo zitaanza.

Aidha, alisema ili bandari kavu itakayojengwa ilete tija, mpango wa serikali kupitia Tazara ni kufanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kutandika reli kuelekea kwenye eneo itakapojengwa bandari kavu ya Inyala.

"Mpango huu unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2020/21," alisema.

Nditiye alisema mkakati uliopo ni kuunganisha bandari kavu ya Inyala na Itungi kwa reli ya Tazara ili kuhudumia nchi jirani za DRC, Zimbabwe, Malawi na Zambia.

"Hata hivyo, mkakati huu utaanza kutekelezwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha reli ya Tazara," alisema.

# Serikali yataja sababu vifo vya watoto

SERIKALI imekiri kuwapo na idadi ya vifo vingi vya watoto katika Mkoa wa Katavi, huku ikidai kuwa havitokani na ukosekanaji wa huduma za afya kwa watoto wachanga.

Hali hiyo, inatokana na watoto wenye umri wa miaka 15-19 kubeba mimba au kuwa na watoto licha ya kuwa viungo vyao kutokuwa na ukomavu wa kutosha.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema mkoa huo unaongoza kwa vifo vya kinamama na watoto wachanga na hali hiyo inatokana na kukosekana kwa vifaa bora wakati wa kujifungua.

Kutokana na hali hiyo, alihoji serikali ina mpango gani kuhakikisha inapunguza vifo hivyo ambavyo kwa takwimu za mwaka jana watoto 501 walifariki dunia.

Akijibu swlai hilo, Dk. Ndugulile alisema mkoa huo una changamoto kubwa ya mimba za ututoni na wastani wa kitaifa sasa hivi ni asilimia 27 ya watoto kati ya miaka 15 -19 wana watoto au mimba.

"Umri wa kupata ujauzito ni mdogo sana na Katavi ni miongoni ya mikoa inayoongoza kwa kuwa bado hawajafikia ukomavu wa kubeba mimba, hivyo suala hilo linachangia kwenye vifo hivyo," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itawasaidia wananchi wa mkoa wa Katavi kifaa cha kumsaidia kupumua mtoto aliyedhaifu (Ambu bag).

Akijibu swali hilo, Dk.Ndugulile alisema pamoja na juhudi za serikali za kuongeza wataalamu wa huduma za afya wenye ujuzi, dawa na vifaa tiba kwenye vituo vya afya, kwa kipindi cha mwaka jana ilipokea na kusambaza vifaa vya kumsaidia mtoto kupumua ikiwamo ambubag na maski 3,735.

Aidha, alisema vifaa hivyo vilipelekwa katika halmashauri za wilaya 109, vituo vya kutolea huduma za afya 3,500 za mikoa 16 Tanzania Bara.

Pamoja na hayo, wizara hiyo inategemea kupokea ambu bag na maski nyingine 2,500 zitakazosambazwa kwenye vituo vya afya katika mikoa ambayo haikutoa mgawo hapo awali.

# Madini ya bil. 3.4/- yauzwa Arusha, Namanga

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

SOKO jipya la madini lililoanzishwa mwezi uliopita mpakani mwa Tanzania na Kenya, katika eneo la Namanga mkoani hapa, limewezesha kuuzwa kwa madini yenye thamani ya Sh. bilioni 1.7.

Aidha, soko la kimataifa la jijini Arusha lililoanzishwa Juni 15, mwaka huu, katika siku zake tatu za awali, madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.7 pia yameuzwa.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Arusha, Erick Robert, alipohojiwa na Nipashe mwishoni mwa wiki iliyopita.

Robert alisema katika soko la Namanga lililoanzishwa Mei 21, mwaka huu, hadi Juni 14, liliwezesha kuuzwa kwa madini yenye uzito wa kilo 171,034 na kuingiza mrabaha wa serikali wa Sh. milioni 83.1 na ada ya ukaguzi wa Sh. milioni 15.4.

Kwa upande wa soko la Arusha, alisema katika siku tatu za awali hadi Juni 18, madini yenye uzito wa kilo 22,983.77 yaliuzwa na kuiingizia serikali mrabaha wa Sh. milioni 51.7 na ada ya ukaguzi ya zaidi ya Sh. milioni 17.

Hata hivyo, Robert alisema wafanyabiashara wote wakubwa wanapaswa sasa kufanyia biashara zao katika eneo hilo kwa kuwa wana ofisi na mpaka sasa wenye ofisi tayari ni 12 tu.

Akizungumzia sekta nzima ya madini, Robert alisema Juni ya mwaka wa fedha wa 2018/2019, mkoa wa Arusha uliuza madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 21 na kuingiza mrabaha wa zaidi ya Sh. milioni 764 na ada ya ukaguzi ya zaidi ya Sh. milioni 208.

"Kwa takwimu hizi ni kwamba mapato yanayokusanywa kutokana na biashara ya madini mkoani Arusha ni asilimia 37 ya maduhuli yote," alisema.

Alisema mpaka sasa Mkoa wa Arusha umeshavuka lengo lililowekwa la kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 2.5 kwa zaidi ya Sh. milioni 102.

Sehemu kubwa ya madini yanayopatikana mkoa wa Arusha ni ya vito ambayo ni pamoja na Tanzanite, Ruby, Anyolite, Corundum, Rhodolite, Green Garnets, Red Garnets, Sperssartite, Tourmaline, Emeralds, Sunstones, Moonstones, Aventurine Quartz, Aquamarine, Kinywe na miamba chokaa.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopatikana katika ofisi ya madini, mkoa wa Arusha una wafanyabiashara wakubwa wa madini wapatao 97, huku wafanyabiashara wadogo wakiwa 291.

Aidha, mkoa wa Arusha una leseni 784 za uchimbaji mdogo, leseni nne za uchimbaji wa kati, 42 za utafiti na moja ya uchenjuaji wa madini.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, akisalimiana na wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi Loongung Kijiji cha Kitiangare, ambapo ameahidi kuchangia Sh. milioni 3 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

# Waiomba serikali kuingilia mgogoro wao na mwekezaji

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

VIJIJI 23 wilayani Longido mkoani Arusha, vimeiomba serikali kuingilia kati mgogoro wao na kampuni ya uwindaji wa kitalii ya Green Miles Ltd, baada ya kugoma kuwalipa Sh. milioni 329.

Baadhi ya viongozi wa vijiji hivyo na wananchi, waliwaambia waandishi wa habari kuwa wanaomba serikali kuingilia kati kwa kuwa kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa mgogoro huo umeshindwa kupatiwa ufumbuzi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mairowa, Lingoine Laizer, alisema wamekuwa na malalamiko na kampuni hiyo kwa muda mrefu sasa na licha ya kuwa na uhusiano mbaya na vijiji imeendelea kuwapo.

"Tumelalamika wilayani lakini nako halmashauri inaidai kampuni hii, tumekwenda mkoani bila mafanikio tukaenda kuonana na Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ameahidi kuja lakini miezi miwili sasa hajafika," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Karao, Saraoni Mollel, alisema kama kampuni hiyo imeshindwa kulipa madai yao ambayo walikubaliana miaka zaidi ya mitatu iliyopita, basi iondolewe.

"Fedha wamegoma kulipa na mwaka huu tunaona wamerudi bila hata kutoa taarifa vijijini wanataka kuendelea na kazi zao," alisema.

Namayani Laizer alisema serikali inapaswa kushughulikia mgogoro huo kwa kuitaka kampuni kulipa au kuiondoa ili kuimarisha uhifadhi.

"Kutokana na uhusiano mbaya baina ya vijiji na mwekezaji eneo la kitalu chake, vitendo vya ujangili vimeota mizizi na kusababisha twiga 16 kuuawa," alisema.

Diwani wa Engarenaibor, Peter Ndereko, alisema Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo, lilitoa msimamo wa kutohitaji tena kufanya kazi na mwekezaji huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema mgogoro baina ya vijiji na kampuni hiyo unapaswa kutatuliwa kwa kuwa ni wajibu wa mwekezaji kukaa vizuri na vijiji.

"Mwekezaji licha ya kuwa na mikataba na Wizara ya Maliasili na Utalii, anapaswa kuwa na uhusiano mzuri na vijiji alikowekeza na serikali ya wilaya tumekwishatoa taarifa ngazi za juu," alisema.

# Wafanyakazi wahamasishwa kuanzisha Saccos

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFANYAKAZI waliopo katika mashirika na kampuni mbalimbali nchini, wamehamasishwa kuanzisha vyama vya akiba na mikopo, katika maeneo yao ya kazi ili kupunguza changamoto mbalimbali za kimaisha na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Marcel Bituro, alisema jana alipokuwa akizungumza katika mkutano wa jukwaa la vyama vya kuweka na kukopa mkoani Arusha.

Bituro alisema kuna umuhimu mkubwa wa mashirika na taasisi kuanzisha vyama hivyo, kwa kuwa vinasaidia katika kujikwamua kiuchumi kwa kujiendeleza na hata kuweka akiba ya kifedha, ambayo itasaidia kutatua changamoto mbalimbali.

Alisema uwapo wa vyama hivyo pia unasaidia kuwa wabunifu katika kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo itasimamiwa na wanachama wenyewe na kuwawezesha kuwekeza kustaafu wakiwa wameshajipanga.

"Chama chetu kilianza mwaka 2002 na tuna wanachama 400 hadi sasa na tayari tumeanzisha mfuko wa elimu ambao humwezesha mwanachama kuweka akiba, kwa ajili ya ada ya watoto na ada hiyo huwa tunatuma kwenye akaunti ya shule moja kwa moja. Suala hili limesaidia wanachama wetu kulipa ada za watoto kwa wakati," alisema Bituro.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Kilombero Multipuporse, Julius Akyoo, alisema wamekuwa wakiwasaidia wanachama kujikwamua kiuchumi kwa kuwakopesha mikopo ya fedha ambayo hurejeshwa kwa riba nafuu.

Akyoo alisema wamejiwekea malengo ya kuanzisha vitega uchumi mbalimbali, ikiwamo kujenga jengo la ghorofa tano na wako katika hatua za mwisho za kuanza mradi huo.

Pia alisema wana malengo ya kujenga hoteli na kuanzisha kiwanda cha usindikaji wa vyakula kwa lengo

la kujikwamua kiuchumi.

Aidha, aliwataka viongozi mbalimbali wa vyama hivyo kufanya kazi zao kwa uwazi na kuwa na nidhamu ya matumizi mazuri ya fedha ili kuondoa migogoro mbalimbali katika vyama hivyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Wakulima wa kahawa Poli, Elirehema Maturo, wamekuwa wakiwasaidia wakulima wa kahawa kupata soko la uhakika kwa kununua kahawa yao kwa bei nzuri sambamba na kutoa elimu jinsi ya kuboresha kilimo hicho.

# Jengo la dharura lapunguza msongamano

**Na Paul Willam,** MOSHI

CHANGAMOTO ya idadi kubwa ya wagonjwa katika jengo la dharura la Hospitali Teule ya Kibosho wilayani Moshi, imepatiwa ufumbuzi baada ya kujengwa kwa jengo jipya, ambapo linaweza kuhudumia wagonjwa 24 kwa wakati mmoja lililogharimu Sh. bilioni 1.487.

Jengo hilo jipya ambalo limejengwa kwa ushirikiano kati ya Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi na ufadhili wa wahisani wa Aktionskreis Ostafrika kutoka Ujerumani, lilizinduliwa jana na mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka 2019.

Akisoma taarifa za ujenzi wa jengo hilo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali, Dk. John Materu, alisema lengo la ujezi huo ni kutokana na jengo lililokuwa likitolea huduma za dharura kuzidiwa na wagonjwa baada ya kupanuka kwa huduma za hospitali.

Dk. Materu alisema mwaka 2011 wagonjwa wa nje waliokuwa wakihudumiwa katika hospitali hiyo walikuwa 45,391 na mwaka 2014 waliongezeka hadi kufikia 75,015 hali iliyosababisha jengo la dharura kushindwa kukidhi utoaji wa huduma bora na salama.

"Kukamilika kwa awamu hii ya kwanza ya ujenzi wa jengo hili, huduma ambazo zimeanza kutolewa ni za wagonjwa ambao si wa ajali, tiba ya mifupa na awamu ya pili itakuwa ufungaji wa vifaa tiba ambavyo vimeshawasili," alisema Dk. Materu.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, alitumia nafasi hiyo kuwataka watumishi wa umma kuacha tabia ya kulalamika na badala yake wachape kazi kwa bidii na kwamba serikali inatambua madai yao ya malimbikizo ya madeni na itayalipa wakati wowote.

Mkongea aliwataka pia watumishi kuacha tabia ya kwenda nje ya nchi kupata huduma za afya na badala yake wapate ndani ya nchi kwa kuwa serikali imekuwa ikipambana kuboresha huduma hiyo.

Baadhi ya wananchi, Renatha Michael na Grace Mushi, waliipongeza Hospitali Teule ya Kibosho kwa ujenzi wa jengo hilo kwa kuwa litasaidia kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kufuata huduma za dharura katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Moshi Mjini.

# Kiongozi Mwenge aonya wala rushwa

**Na Paul William,** MOSHI

SERIKALI imejipanga kuendeleza mapambano dhidi ya wala rushwa na ufisadi nchini na kuonya kuwa wanaoendekeza vitendo hivyo, watakumbana na hatua kali za kisheria.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, alisema juzi wakati wa ukimbizaji Mwenge katika Halmashauri ya Moshi na kuzindua klabu ya wapinga rushwa katika Shule ya Sekondari ya Langasani. Klabu hiyo ina wanafunzi 98.

Mzee Mkongea alisema serikali ya awamu ya tano imeonyesha dhahiri kwa vitendo kupambana na watumishi wasio waaminifu ambao wameweka mbele maslahi binafsi na kuwataka kuachana na dhana hiyo badala yake waweke mbele kwa maslahi ya taifa.

Alisema vita dhidi ya rushwa sio kazi ya serikali pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) pekee bali huanzia na mtu mwenyewe katika kuwaibua wala rushwa.

"Wako watu ambao wamekuwa wakiendekeza rushwa ya ngono kwa wanawake. Wananchi pamoja na nyie wanafunzi mna jukumu kubwa la kuhakikisha mnawaibua watu hawa ili wachukuliwe adhabu kali na iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia hizo," alisema.

Aidha, kiongozi huyo alitumia nafasi hiyo kuipongeza Takukuru Mkoa wa Kilimanjaro kwa juhudi na kazi kubwa inayoifanya katika kupambana na watu wasio na uzalendo na nchi yao na kuwataka kuendeleza juhudi hizo kwa maslahi makubwa ya taifa.

Awali, wakisoma risala kwa kiongozi huyo, wanafunzi hao walisema lengo la kuanzishwa kwa klabu hiyo ni kuelimisha wanafunzi madhara ya rushwa na kutambua aina zake.

"Tumekuwa tukitoa elimu kwa jamii dhidi ya madhara ya rushwa pamoja na kuielimishwa kutambua umuhimu wa kupambana na wala rushwa kwa kutoa taarifa Takukuru ili wachukuliwe hatua," alisema.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Leonard Chamriho (katikati), akionyesha ripoti ya mwaka 2018 ya Shirika la Kuwezesha Usafiri kwa Usharoba wa Kati (CCTTFA), kuhusu uchunguzi wa masuala ya usafirishaji kwa wadau wa Tanzania, baada ya kuizindua, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu Mtendaji wa CCTTFA, Kapteni Dieudonne Dukundane na Mkurugenzi Mkazi wa TradeMark East Africa (TMEA) Tanzania, John Ulanga. **PICHA: JOHN BADI**

# Watangaza nia CCM waonywa

**Na Paul William,** MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewaonya makada ambao wameanza kujipitisha katika majimbo kujinadi kwa ajili ya ubunge kuwa waache mara moja tabia hiyo na watakaobainika watachukuliwa hatua za kinidhamu.

Pia kimesema wanachama hao wanapaswa kutambua kuwa chama ndicho kitakachoteua wawakilishi watakaopeperusha bendera katika nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM kupitia vijana, Japhari Kubecha, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Wilaya ya Moshi Vijijini ya Kijana iliyozinduliwa katika kata ya Mabogini.

Alisema wakati chama kimekuwa kikijikita katika kusikiliza kero na matatizo ya wananchi ili kuyatafutia ufumbuzi, wako baadhi ya wanachama ambao wamekuwa wakipita na kuwarubuni wananchi na kujinadi kugombea nafasi za ubunge. Kutokana na tabia hiyo, aliwaonya wanachama hao kuacha mara moja.

"CCM ni chama chenye kanuni na utaratibu wa demokrasia na muda utakapofika kitaleta mgombea atakayepeperusha bendera yake na hawa ambao wameshaanza kampeni mapema hawatapata nafasi," alisema.

Kubecha alisema wako pia baadhi ya viongozi na wanachama ambao wamekuwa na tabia ya kuwabeba wanaotangaza nia za kugombea na kusababisha kuzaliwa kwa makundi na kuwaonya watu hao kuacha tabia hiyo.

Mjumbe huyo pia alisema kuna baadhi ya watu wanaotaka kuliamulia taifa lifanye nini na wamekuwa wakizunguka nje ya nchi na kuanza kulichafua pamoja na viongozi wake kutokana na kutishwa na kasi ya serikali.

"Watanzania wanaodhani ni maadui wa (Rais) Dk. John Magufuli si kweli bali watambue ni maadui wa UVCCM (Umoja wa Vijana wa CCM) na taifa, hivyo hatutawafumbia macho," alisema.

Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Moshi Vijijini, Hassan Hossein, alisema changamoto zinazoikumba kata ya Mabogini zinasababishwa na viongozi waliowachagua mwaka 2015.

Alisema CCM mpya imejipanga kuhakikisha inawapitisha wagombea wenye nia ya kuwatumikia wananchi na kuwataka kuwaamini na kuwachagua kuanzia uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu mwakani.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 25, 2019
...MU • SAYANSI




Ukurasa 15

## UCHAMBUZI WA KITABU;

No Mud, No Lotus: The ART of Transforming Suffering by Thich Nhat Hanh (Sanaa ya kubadili m mateso kuwa ushindi na furaha)

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

**Aina bora za utunzaji wa sharubu**

# Mikakati yainyanyua Singida kutoka mkiani 2017 kuwa ya 14 mwaka jana



Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# WANANCHI JIEPUSHENI NA TABIA YA KUJICHUKULIA SHERIA MKONONI

DUNIA kwa hivi sasa inakumbwa na tatizo la jamii kujichukulia sheria mkononi.

Kwamba umezuka mtindo wa watu kuchukua hatua ya kumwadhibu au kumshambulia mtu ama jamii kuchukua hatua juu ya jambo fulani bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Tanzania ikiwa ni sehemu ya dunia imeshuhudia matukio kama ya wananchi kumshambulia mtu hadi kumuua au kumwacha akiwa na kilema cha kudumu kwa kisingizio kuwa ni mwizi au ametenda uhalifu fulani.

Aidha, matukio mengine ni ya mauaji yanayotendwa na baadhi ya watu kwa kisingizio cha wivu wa mapenzi au ulevi.

Matukio ya aina hii ndiyo yanatokea mara kwa mara na yanachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa matukio ya mauaji hapa nchini.

Matukio mengine ya kujichukulia sheria mkononi ni yale yanayotendwa kutokana na imani za kishirikina ambapo wana ndugu, ukoo, majirani, wanakijiji au watu wengine tu mtaani wanamtuhumu mtu kuwa ni mchawi na mara nyingi watuhumiwa wanakuwa ni wale wazee.

Matokeo yake wanawavizia na kuwaua au kuwashambulia kwa silaha mbalimbali hadi kuwaua.

Vilevile, migogoro ya wakulima na wafugaji nayo imekuwa ikisababisha wananchi kujihusisha na vitendo hivyo vya kujichukulia sheria mkononi, kwani badala ya migogoro hiyo kusuluhishwa kwa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa au katika katika vikao vya kusuluhisha, wengine wanakiuka na kujichukulia sheria mkononi kwa kutekeleza mauaji au kusababisha majeraha na vilema kwa wengine.

Wakati akihojiwa na mwandishi wa makala haya, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini Kamishna Msaidizi Mwadamizi wa Polisi SACP David Misime amesema kuwa, vitendo vya kujichukulia sheria mkononi ni ukiukwaji wa sheria za nchi na kwa wale wanaobainika hukamatwa na wanapopatikana na hatia mahakamani sheria inaelekeza kuwa adhabu yake ni kifo.

Vitendo vya kujichukulia sheria mkononi vimekatazwa na sheria mama ambayo ni Katiba ya nchi na sheria nyingine pamoja na vitabu vya dini navyo vimekataza vitendo hivyo.

Akitoa wito kwa wananchi juu ya vitendo vya kujichukulia sheria mkononi, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, SACP Misime, alieleza kuwa ili kuondokana na matukio haya ambayo yanaleta madhara makubwa kwa jamii na kwa familia kubaki yatima, kujenga chuki na uhasama na baadhi ya wanajamii kubaki vilema ni vyema wadau wote na jamii kwa ujumla kukemea vikali vitendo hivyo pamoja na kusimamia malezi na maadili kuanzia ngazi ya familia kwani ngazi hiyo ikisimamiwa vizuri matukio kama haya yatapungua kwa kiasi kikubwa.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

Matukio mengine ya kujichukulia sheria mkononi ni mauaji yanayotokana na wivu wa mapenzi.

Ni matukio ambayo hayawezi kuzuiwa na doria za askari Polisi mitaani kwani hutendeka wakati mwingine ndani ya nyumba, majumba ya starehe au mashambani.

Hivyo ni vyema jamii ikashirikiana kutoa elimu kwamba suluhisho si kujichukulia sheria mkononi, kwamba ukifanya hivyo nawe hutabaki salama, bali utakamatwa na kufikishwa mahakamani.

Na matokeo yake kuhukumiwa kunyongwa au kifungo cha maisha jambo ambalo litakutenga na familia yako na kupoteza muda wako muhimu wa kufanya kazi zako za kujiletea maendeleo.

Kama ni suala la wivu wa mapenzi kwa kugundua kuwa mwenzako ana mahusiano ya pembeni utatuzi si kuchukua sheria mkononi bali ni kufungua kesi ya madai mahakamani dhidi ya unayemtuhumu ili kudai fidia.

Jambo hilo litakufanya uendelee na uhuru wako na kazi zako za kujiletea maendeleo, badala ya kukosa vyote (Uhuru, familia na mali zako) na mshahara utakuwa kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Pia, alitoa mfano kuwa zipo nchi ambazo matukio kama hayo ni machache sana na hilo limewezeshwa na jamii kutambua thamani ya uhai, thamani ya kuishi na familia ukiwa huru, thamani ya kuwa huru na kufanya kazi zako za kujiletea maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla.

Pia wametambua dawa ya tatizo sio kulitatua kwa kutengeneza tatizo lingine na pengine kubwa zaidi.

"Dawa au ufumbuzi ni kufuata sheria, kanuni na taratibu na kutambua thamani yako kama binadamu, utu na thamani ya muda," anasema msemaji wa Jeshi la Polisi.

Wananchi kwa namna moja ama nyingine hawana budi kufuata sheria za nchi kwa kuwakamata wahalifu na kuwakabidhi kwa Jeshi la Polisi ama mamlaka zingine za kisheria ili waweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Kwamba kuwaadhibu ni jambo ambalo linaweza kusababisha majeruhi hata mauaji kwa watu wanaotuhumiwa kutenda uhalifu ndani ya jamii.

Tuachane na tabia ya kujichukulia sheria mkononi, ina hasara kubwa kwa maisha yako.

**Imetolewa na:-**

**Kitengo cha Uhusiano, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Dar es Salaam, habariphq@gmail.com**



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO** marobarnabas@yahoo.com

### Ukiambiwa kitenge wakitia moto

"UKIAMBIWA kitenge au kiepushe na moto wewe wakitia motoni" ni methali ya kutumiwa kwa mtu anayepewa ushauri fulani wa kumfaa lakini akaupuuza na kuishia kujitosa katika taabu.

Wahenga wametuachia methali nyingi za kutuzindua na kutuelimisha. Kwa mfano, "Asiyeangalia huishia ningalijua." Mtu asiyeangalia aendako huishia kusema 'laiti ningalijua' baada ya kufikwa na jambo. Twashauriwa tuwe watu wa kukanyika au tunaofuata ushauri tunaopewa na waliotutangulia kwa maarifa au ujuzi kama vile wazee.

Magazeti ya michezo hutumia maneno ya Kiingereza kana kwamba hakuna ya Kiswahili! Maneno yanayotumika mara kwa mara ni 'ishu' yaani 'issue' kwa Kiingereza ambalo maana yake kwa Kiswahili ni suala au hoja. Gazeti la Kiswahili limeandika: "Ishu ya Msuva Ulaya iko hivi buana."

Msomaji anayeitwa Mwamini aliandika yafuatayo kwenye gazeti la Mwananchi: "Kiswahili ni tunu* yetu. Kutofungamanisha Kiswahili na maendeleo ni kuukataa uzalendo wetu, utu wetu na utamaduni wetu bila sababu za msingi. Matokeo yake ni kuwa watumwa wa utamaduni wa watu wa Magharibi. Maendeleo huletwa na watu walio huru kifikra na kujituma katika kufanya kazi. Lugha inabaki kuwa chombo cha mawasiliano ambacho kikiwa peke yake bila watu walio huru kifikra, katu maendeleo ya kweli hayatoweza kufikiwa."

*Tunu ni kitu ambacho mtu humpa mwingine kuwa ishara ya upendo; hidaya, tuzo; kitu ambacho hupatikana kwa nadra, kitu cha thamani kubwa. Kongole (shukrani, asante) Mwamini kwa kuliona hilo.

Pia waandishi hupenda sana kutumia maneno tofauti na maudhui (wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema). Nimekuwa nikisahihisha Kiswahili lakini ni kama natwanga maji kwenye kinu. Kila ninavyojitahidi ndivyo wenzangu wanavyozidi kutumia maneno kinyume na maana halisi!

Baadhi ya maneno yanayotumiwa vibaya ni 'balaa', 'bana' au 'buana', 'mzuka' n.k. Uhalisi wa neno 'balaa' ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; kisirani, nuksi. Pia jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku; janga lililoenea katika jamii au kwa mtu binafsi.

Neno bwana siku hizi limepewa majina mawili: 'buana' au 'bana.' 'Buana' halimo kabisa kwenye msamiati wa Kiswahili ila limebuniwa na waandishi wa habari za michezo. 'Bana' ni kitendo cha kuweka kitu katikati ya nguvu mbili zinazoishia kwenye kitu chenyewe.

"Mkali wa Bocco mzuka kama wote" ni kichwa cha habari kinachomduwaza msomaji kwa kutojua maana yake, kikifuatiwa na maelezo yafuatayo:

"Meddie Kagere ndiye aliyeibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu baada ya kutupia kambani mabao 23, lakini straika anayemfuata na kinara kwa wazawa ni Salim Aiyee wa Mwadui, unaambiwa kwa sasa ana mzuka kama wote huko mgodini."

Nimeeleza mara nyingi kuwa maana ya 'tupia' ni kuweka kitu juu ya kingine kwa kurushia rushia mahali mbalimbali kama vile ufuta juu ya mkate. Kitendo cha kuweka nguo begani au kichwani; pia tupia macho.

'Kamba' ni nyuzinyuzi kama vile za usumba (uzi unaotokana na ganda la nnje la nazi ambalo hufaa kusokotea kamba) au katani, zinazosokotwa kwa urefu, aghalabu hutumika kufungia mizigo; ugwe. Pia ni kiumbe wa baharini mwenye miguu mingi mirefu, magamba na nyama laini.

Ingeandikwa: "Meddie Kagere ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu nchini kwa kufunga mabao 23, akifuatiwa na mzawa Salim Aiyee wa Mwadui." Hayo ya "sasa ana mzuka kama wote" anajua aliyeandika. Mwandishi anapaswa kuhakikisha wanaosoma habari/makala zake wanaelewa maana ya maneno anayoandika.

Ajabu ni kuwa hata gazeti hili ninalolitumia kukosoa maneno ya ovyo magazetini, yaelekea waandishi wake hawasomi makala za "Tujifunze Kiswahili" na ushahidi ni huu: "Aliongeza kuwa halmashauri imekinunua kifaa hicho kwa ajili ya matumizi ya kupimia kutokana na kuchukuliwa kipimo hicho, wanafanya kazi katika mazingira magumu, ikiwamo kukodisha kifaa hicho."

Sentensi imeandikwa ovyo kwani ingepaswa kuwa mbili. "Alisema Halmashauri ilinunua kifaa hicho (GPS) ili kupimia ramani. Kutokana na kifaa hicho kuchukuliwa, watu wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa kukodi kifaa hicho."

'Kukodisha' limetumiwa vibaya na kuharibu maana. Kiswahili fasaha, 'kodisha' ni pangisha kitu kama chumba/vyumba, nyumba n.k. kwa malipo fulani. Wenye nyumba hukodisha chumba/vyumba au nyumba zao na wanaokodi huitwa wapangaji. Vivyo hivyo wenye vyombo vya usafiri hukodisha vyombo vyao vya usafiri na wanaokodi, yaani watumiaji, huitwa wakodishaji.

Neno 'kodi' lina maana mbili: Kwanza ni malipo kwa ajili ya kitu kilichotumiwa kwa muda. Pili ni fedha inayotozwa na serikali kwenye pato la mtu; kitendo cha kutumia kitu cha mtu mwingine kwa muda kwa malipo.

Sisi ndiwo twatakiwa kwenda kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wenzetu. Pukachaka! (Neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa).


Methali: Kila mlango una ufunguo wake.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## UCHAMBUZI WA KITABU;

# No Mud, No Lotus: The ART of Transforming Suffering by Thich Nhat Hanh (Sanaa ya kubadili mateso kuwa ushindi na furaha)

Ukijua mateso yanasababishwa na nini na ukawa na uwepo wa akili kuwa maisha yana mateso, basi utakuwa umejua ukweli mmoja wa dhahabu utakaokutoa katika kuendelea kuteseka kwa kukosa maarifa...



Kutambua ugumu wa mtu anakoelekea ndiyo njia inayompeleka kwenye mafanikio. **PICHA: MTANDAO**




KATIKA maisha watu wengi wanateseka sababu ya kutojua namna vitu vilivyo, vinavyokuwa na namna ya kukabiliana navyo. Hapa ndipo chimbuko la mateso kwa watu wengi duniani.

Kama si mateso ya mwili moja kwa moja, basi ni mateso ya kifikra ambayo huwa hayaachi kuwaandama mpaka pale siku ambapo watajua kweli ilipo na kukubali na kasha kuchukua hatua ya kufuata au kubadilika.

Mwandishi wa kitabu hiki kaelezea kwa mapana sana namna ya kujiweka huru katika maisha pale unapojua uwepo wa kitu na kukikabili kama njia ya kubadili mateso kuwa ushindi na furaha.

Ukijua mateso yanasababishwa na nini na ukawa na uwepo wa akili (mindfulness) kuwa maisha yana mateso, basi utakuwa umejua ukweli mmoja wa dhahabu (noble truth) utakaokutoa katika kuendelea kuteseka kwa kukosa maarifa (Ujinga).

Furaha ni somo ambalo linaweza kuelezeka zaidi kwa mtu mmoja hata mwingine kwa jinsi aonavyo.

Wakati wapenzi wawili waliopanga kwenda katika matembezi kuzungumza juu ya maisha yao ya baadaye, mvua inyeshapo wanaweza kukereka sana na hata wakapoteza furaha wakati huo huo mkulima wa kule Dodoma, Mbeya, Rukwa au Morogoro kwake ni furaha kubwa sana sababu mvua ndilo lililokuwa ombi lake.

Kadri ambavyo katika maisha unajitahidi kukimbia uhalisia ulivyo, ndivyo ambavyo unajitengenezea mateso na hatari kubwa zaidi.

Licha ya kuwa si sehemu ya ua lakini kukosekana kwa mwanga wa jua, mawingu au ardhi hakuna matokeo ya mmea.

Hapa tumeona watu walioingia katika kufanya tabia hatarishi kama kunywa pombe na hata wengine kuvuta sigara pale ambapo walipokuwa wakiukwepa uhalisia wa maisha ulivyo, kumewaletea uraibu na matatizo makubwa.

Furaha si hali inayodumu ni kama vile sarafu inaweza kugeukia upande wowote na upande huo ni mateso na mateso unapoyakubali, ndivyo inavyokuwa rahisi sana kuirudisha furaha na maisha yakaendelea vizuri zaidi.

Shida ni kuwa watu wengi hawakubaliani na upande wa mateso kama ni sehemu pia ya furaha ukikubali kuwa yapo.

Kama utakuwa mdadisi mzuri sana wa mazingira utakubaliana kabisa UA ni matokeo ya vitu ambavyo si sehemu ya ua kivipi?

Mwanga wa jua, mawingu, ardhi ni mazingira ambayo yanafanya mmea utokee na kisha ua liwepo.

Licha ya kuwa si sehemu ya ua lakini kukosekana kwa mwanga wa jua, mawingu au ardhi hakuna matokeo ya mmea.

Hivi ndivyo ilivyo kwa furaha kwamba mateso kuwapo ndio chimbuko la furaha.

Tunapokuwa mbali na

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA ELISANTE JOHN, SINGIDA

# Mikakati yainyanyua Singida kutoka mkiani 2017 kuwa ya 14 mwaka jana

• Ni matokeo ya darasa la saba • Ni ushirikiano wa uongozi mkoa na wadau
• Ufuatiliaji, usimamizi, vitendo na kuacha kukaa ofisini siri iliyojificha

BAADA ya Mkoa wa Singida kushika nafasi ya mwisho kwenye matokeo ya darasa la saba kitaifa mwaka 2017, hatimaye umeondokana na aibu hiyo, baada ya kujinasua hadi nafasi ya 14, kati ya mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Mafanikio hayo yametokana na juhudi kubwa zilizochukuliwa na serikali, wadau wa elimu, viongozi, walimu, wazazi na jamii kwa ujumla, zilizowezesha kuukwamua mkoa huo kutoka nafasi hiyo ya 'mkiani'.

Mkoa una jumla ya shule za msingi 525, 21 miongoni mwao zikiwa ni za watu binafsi.

Haikuwa rahisi kuyafikia mafanikio haya bila ya juhudi za wadau wengi kujitoa kwa dhati, kufanya ufuatiliaji, kuchukua maamuzi magumu na hata kukumbushana majukumu ili kuikimbia dhihaka ya kuitwa 'Mkoa ulioshika mkia mwaka 2017'.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Singida, Mwalimu Nelesi Mulungu, anasema matokeo ya mwaka jana yanauweka mkoa kwenye nafasi nzuri zaidi siku za usoni.

Hiyo ni baada ya wanafunzi 20,617 kati ya 27,653 waliofanya mtihani Septemba mwaka jana, kufaulu na hivyo kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza.

Mwalimu Mulungu anabainisha kuwa kati ya wanafunzi hao waliofanya mtihani, wasichana 14,741 na wavulana 12,668, wasichana waliofaulu ni 11,091 na wavulana 9,526, hivyo kuwezesha ufaulu kuwa sawa na asilimia 75.21 mwaka jana.

"Ufaulu kwa mwaka jana ulipanda hadi kufikia asilimia 75.21, ikilinganishwa na asilimia 62 za mwaka 2017...huu umepanda kwa asilimia 13.21, na hili ni jambo la kujivunia, ingawa bado tuna safari ndefu kuyafikia mafaniko bora zaidi," anafafanua.



Wadau mbalimbali wa elimu wakiwa kwenye picha ya pamoja na wanafunzi, viongozi, kamati ya shule ya msingi na wazazi baada ya kukutana kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuboresha miundombinu ya shule yao.

### HALMASHAURI ZILIZOONGOZA

Ofisa elimu huyo anazitaja halmashauri tatu za wilaya zilizoongoza kwa ufaulu kimkoa, huku nafasi zao kitaifa zikiwa kwenye mabano kuwa ni Itigi iliyokuwa ya kwanza (50), Manispaa ya Singida ya pili (75) na Singida Vijijini ya tatu (82).

Anasema Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ambayo mwaka 2017 ilishika nafasi ya mwisho kimkoa na kitaifa pia, mwaka jana imeendelea kuwa ya mwisho kimkoa, lakini ikajinasua kitaifa kutoka mkiani baada ya kuwa ya 181, miongoni mwa halmashauri za Tanzania Bara (kitaifa).

Hata hivyo, Mwalimu Mulungu anaipongeza halmashauri hiyo baada ya Shule ya Msingi St Marie Eugenie iliyopo wilayani humo, kushika nafasi ya kwanza kimkoa, wakati ambapo halmashauri hiyo inaburuza mkia, kimkoa.

Anasema licha ya Wilaya ya Mkalama kuwa ya mwisho kimkoa, lakini uongozi wa mkoa unajivunia halmashauri hiyo kuongeza hali ya ufaulu hadi kufikia asilimia 57, ikilinganishwa na asilimia 37.08 za ufaulu, mwaka 2017.

Anasisitiza, kama ambavyo mkakati uliwekwa kuukwamua mkoa kutoka nafasi ya mwisho, juhudi hizo ndizo zitakazounganishwa pia kuiwezesha wilaya hiyo mwaka huu iweze kufanya vizuri zaidi, baada ya changamoto zake nyingi kutatuliwa.

Anazitaja baadhi ya changamoto zilizopo katika wilaya hiyo iliyogawanywa kutoka Iramba kuwa ni uwepo wa jamii ya wafugaji inayohamahama, uhaba wa walimu, mwamko duni wa elimu kwa baadhi ya familia, umaskini na miundombinu duni.

Anaomba wadau wa elimu kuisadia wilaya hiyo kuzikabili changamoto zake, zikichangizwa pia na uwepo wa jamii ya Wahadzabe inayoishi katika wilaya hiyo, huku ikitegemea asali, matunda pori, nyama pori na mizizi, kama chakula chao kikuu.

### KATIBU TAWALA

Akizungumzia mafanikio ya elimu kimkoa, Katibu Tawala Mkoa, Dk. Angelina Lutambi, anasema mshikamano kati ya serikali, idara ya elimu, wataalamu wabobezi, wanafunzi, walimu na wadau wa elimu, ndio uliowezesha mkoa kujinasua katika nafasi hiyo.

Dk. Angelina anasema, baada ya matokeo ya mwaka 2017 kuonyesha Singida ni mkoa wa mwisho, Sekretarieti chini ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, ilikutana mara moja kubaini tatizo na dosari zilizokuwa ndani ya uwezo wao ili kuzitatua.

Walifikia maazimio na kuandaa mikakati kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wenye nia ya kuhakikisha hakuna kosa litakalojirudia tena, ili kurejesha hadhi ya mkoa katika suala zima la sekta ya elimu ya msingi, katika ngazi zote.

Dk. Angelina anasema, ndipo wataalamu na wadau walielekeza nguvu kwa vitendo, badala ya kufanya kazi kwa mazoea ofisini, hatimaye wakafanikiwa kumaliza kero nyingi kabla hata ya kufika ofisini, kwa kushirikiana na jamii husika, pia jitihada za wanafunzi.

Anasema kati ya wadau hao ni, Mpango wa Kuboresha Elimu nchini (EQUIP-T), uliowezesha msaada wa pikipiki kwa waratibu elimu ngazi ya kata, zikiwamo pikipiki 21 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 63 kwa Halmashauri ya Wilaya Singida Vijijini.

Pikipiki hizo pia zilisambazwa kwa halmashauri nyingine sita za mkoa ikiwamo, Manispaa ya Singida, Ikungi, Mkalama, Itigi, Manyoni na Iramba, ambapo waratibu walifanya kazi zao kwa ufanisi kusimamia sekta ya elimu na maendeleo kwa ujumla.

Wakati wa makabidhiano ya pikipiki hizo kwa halmashauri zote za wilaya, Mkuu wa Mkoa Dk. Nchimbi, aliwaagiza waratibu elimu kuzitunza na kufuata maelekezo ya serikali, badala ya kuzigeuza kuwa bodaboda.

"Licha ya kuzitumia pikipiki hizi kwa kazi zenu za kila siku, hakikisheni taaluma inasonga mbele...huko mnakopita muwe mnakagua na miundombinu mbalimbali na mtoe taarifa kwa viongozi wa maeneo yenu na kwangu pia, ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa," anasisitiza.

Anawataka waratibu hao kuwajibika zaidi kwa kuwasaidia walimu waliokata tamaa ya maisha, na kuwarejesha katika hali ya upendo, badala ya kuwakaripia ili waweze kujirudi na kuipenda kazi yao, kadri walivyofundishwa vyuoni.

### CCM

Wadau wengine walioshiriki juhudi za kuunasua mkoa kutoka nafasi ya mwisho ni, Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya Jumuiya ya Umoja wa Wazazi, kutokana na kongamano kubwa la wadau wa elimu lililoitishwa katika ukumbi wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Singida.

Kongamano hilo lilipewa jina la 'Maadili na Elimu ni Mapacha wasioachana, Tutimize Wajibu wetu kwa Maendeleo ya Taifa.'

Katika kongamano hilo Jumuiya hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Manispaa na wadau, walizibainisha dosari nyingi zinazosababisha Mkoa wa Singida kuanguka vibaya katika elimu.

### WADAU WENGINE WALIOALIKWA

Waalikwa wengine walikuwa ni mashirika ya madhehebu ya dini, wajasiriamali, wataalamu, wadau, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) pamoja na mashirika ya umma na yale ya binafsi.

Baadhi ya maazimio yaliyopitishwa ni pamoja na msisitizo wa suala la nidhamu kwa wanafunzi, maadili kwa walimu, wajibu wa wazazi, pia suala la lishe (chakula cha mchana), kwa ajili ya wanafunzi wakiwa shuleni.

### CECE & DANIEL ENTERPRISE

Shirika la Cece & Daniel Enterprise la jijini Dar es Salaam nalo limetoa mchango wake kupitia shindano lililojulikana kama 'The 2018 Spelling BEE', likiwa mahsusi kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi. **PICHA ZOTE: ELISANTE JOHN, SINGIDA**

Meneja mwezeshaji wa Cece & Daniel Enterprise, Upendo Mushi, anasema, lengo la shindano hilo ni kusaidia wanafunzi kutamka kwa ufasaha maneno, likianzia na shule 14 za msingi na nyingine 14 za sekondari, huku nyingine nne zikiwa za wenye mahitaji maalumu.

Anasema wanafunzi wote watashiriki, lakini watachujwa wapatikane 10 bora kwa kila shule, tayari kushiriki kwenye shindano kubwa litakalojumuisha wanafainali 320, na wengine 10 wenye mahitaji maalumu, (walemavu wa kusikia), ili kumpata mshindi.



Wasichana wa Sekondari ya Kinambeu katika Wilaya ya Iramba wakipokea sehemu ya msaada wa ndoo kutoka kwa Mbunge Aysharose Mattembe, kwa ajili ya usafi, ili kuchochea morali ya ufaulu wa jinsia hiyo.

### TUME YA UTUMISHI

Nayo Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (TSC), ni miongoni mwa wadau waliosaidia mkoa wa Singida kuimarisha matokeo ya darasa la saba.

Hiyo ni baada ya makatibu wasaidizi wa tume hiyo ngazi za wilaya kukutana, ili kubaini changamoto zinazochangia kuporomoka kwa elimu.

TSC Taifa ilijielekeza zaidi katika taratibu za kazi, yaani kufuata sheria, kanuni na taratibu za kazi, kutoa ushauri murua kwa waajiri wao ili kupunguza malalamiko na mashauri ya kinidhamu kwa walimu katika vituo vya kazi.

Masuala ya sheria, utawala na ajira kwenye maeneo ya kazi, ni kati ya mada zilizofundishwa kwa makatibu hao wasaidizi, lengo likiwa lilelile la kuboresha sekta ya elimu hapa nchini.

Kiongozi wa timu ya mkoa wa Singida Phoibe Okeyo, kutoka asasi ya Equip-Tanzania inayosaidia kuboresha elimu nchini na mkoa wa Singida kwa ujumla, aliahidi asasi hiyo kuendeleza ushirikiano na serikali, ili kuinua sekta ya elimu katika mkoa wa Singida.

### COMMUNITY EMPOWERMENT

Shirika la Community Empowerment Project-4CCP linalomilikiwa na Hospitali ya Haydom mkoani Manyara, nalo limejitosa kuhakikisha linatoa mchango wake kwa jamii ya Wahadzabe, katika kijiji cha Munguli, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Kwa ufadhili wa Shirika la Norwegian Church Aid (NCA) la nchini Norway, shirika hilo limejenga vyumba viwili vya madarasa, kuajiri walimu na kulipa mishahara yao katika Shule ya Msingi Munguli, na kuchimba kisima cha maji ambacho kimegharimu Sh. milioni 145, kwenye kijiji hicho.

Vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu katika shule hiyo, kwa pamoja vimegharimu Sh. 65,000,000, huku shirika hilo likiahidi kuisaidia zaidi halmashauri hiyo, ili kuwezesha jamii ya Kihadzabe kuelimika na hivyo kuachana na maisha ya zama za kale.

Hatua hiyo imeleta mageuzi ya ufaulu wa darasa la saba na la nne, ambapo umepanda kutoka wanafunzi watano (2016) hadi 16 mwaka 2017 kwa darasa la saba, huku kwa darasa la nne wanafunzi wote wakifaulu katika wastani wa daraja A na B, ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

### MIKAKATI KUINUA ELIMU 2019

Ofisa Elimu Mkoa, Mwalimu Mulungu, anasema idara yake itaendelea kufuatilia na kuhakikisha walimu wanafanya maandalizi ya kutosha katika majukumu yao, ili kuzing'arisha zaidi shule zao na mkoa wa Singida kwa ujumla.

Anasema, kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya na manispaa, idara yake itaendelea kuielimisha jamii kupitia kamati za shule na kamati za maendeleo za kata, juu ya umuhimu wa mahudhurio ya wanafunzi kuwa ni ya lazima, tangu anapoandikishwa hadi anapomaliza.

Hata hivyo, Mulungu anafafanua kuwa, hivi sasa mkoa unaendelea na juhudi za kuzihimiza halmashauri za wilaya na manispaa, zihamasishe jamii kuchangia gharama za miundombinu iliyopungua katika kila shule zake.

Mwalimu Mulungu anasisitiza kuwa, kupitia mpango wa uboreshaji wa elimu (EQUIP-T), jamii imehamasishwa kuhakikisha kila shule na kwa kila darasa kunakuwapo mwakilishi ambaye atakuwa anafuatilia maendeleo ya shule. Anasema, idara yake itaendelea na vikao vya mara kwa mara na maofisa elimu ngazi ya wilaya, kata na walimu wakuu, kuhimiza uwajibikaji, kuandaa mitihani miwili ya utimilifu kwa darasa la saba na la nne kila mwezi, na kuwapo uwasilishaji wa upimaji kutoka kila halmashauri na kwa kila shule.

JIELIMISHE

## MATAIFA YALIYOENDELEA YAPOTEZA IMANI NA CHANJO

UTAFITI juu ya mienendo ya umma katika masuala ya afya duniani, umeonyesha kuwa watu wanaoishi kwenye nchi zenye uchumi mkubwa hasa barani Ulaya, wamekuwa na imani ndogo katika chanjo dhidi ya magonjwa.

Matokeo ya utafiti huo, yanahusishwa na kuibuka kwa harakati dhidi ya chanjo ambapo watu hukataa kuamini faida za chanjo ama kudai kuwa ni hatari.

Ripoti ya Shirika la Masuala ya Tiba ya Uingereza liitwalo British Medical Charity Welcome Trust, juu ya utafiti uliofanywa kati ya mwezi Aprili na Desemba mwaka uliopita, imeonyesha kuwa Ufaransa inaongoza kwa kutokuwa na imani na chanjo.

Ripoti hiyo imeonyesha kuwa asilimia 33 ya raia wa Ufaransa hawakubaliani na kauli kwamba chanjo ni salama.

Hata hivyo, asilimia 79 ya watu duniani kote imeonyesha kukubali kwamba chanjo ni salama, huku asilimia 84 wakisema kuwa chanjo zinafanya kazi kwa ufanisi.

Ripoti hiyo imeonyesha kuwa nchi za Bangladesh na Rwanda, zina imani kubwa na chanjo, huku watu katika nchi hizo wakikubali kwa asilimia 100 kwamba chanjo hizo ni salama na muhimu kwa watoto.

Nchi zilizotajwa kuwa na imani ndogo zaidi na chanjo zimetajwa kuwa ni zile za Ulaya Magharibi zikifuatiwa na Ulaya Mashariki.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa iliyotolewa mwezi Aprili mwaka huu ilionyesha kuwa takribani watoto milioni 169 walikosa dozi muhimu ya kwanza ya chanjo dhidi ya surua kati ya mwaka 2010 na 2017.

Kwa mujibu wa takwimu rasmi, kwa upande wa Marekani pekee, idadi ya visa vya ugonjwa huo kwa mwaka huu ni zaidi ya 1,000.

### NCHI MASKINI NDIZO ZENYE MAAMBUKIZI ZAIDI DUNIANI

Mmoja wa wataalamu waliohusika katika utafiti huo, Imran Khan anasema kwa nchi ambazo watu wake wana imani kubwa na chanjo kama vile Misri na Bangladesh, ndipo kwenye magonjwa ya kuambukiza zaidi.

Khan ameongeza kwamba kwa upande wa nchi zilizoendelea hata ambapo mtu hapati chanjo, bado huwa katika hatari ndogo ya kupata maambukizi na kwamba hata mtu anapoambukizwa hapati matatizo makubwa ya kiafya kwani katika nchi hizo kuna mifumo mizuri ya afya.

Shirika la British Medical Charity Welcome Trust la Uingereza lililofanya utafiti huo, limesema linatumaini kwamba utafiti wake ni msingi mzuri kwa serikali mbalimbali duniani, kufuatilia jinsi tabia za watu zinavyobadilika, hivyo kusaidia katika kutunga sera zinazolenga kutoa kinga, hasa ugonjwa wa surua ambao haustahili kufumbiwa macho.

Mbali na masuala ya chanjo, ripoti ya shirika hilo imeonyesha pia kwamba, kuna tofauti za kijinsia katika ufahamu juu ya masuala ya kisayansi duniani.

Imebainisha kwamba asilimia 49 ya wanaume wanasema wanafahamu kiasi ama sana juu ya sayansi, huku asilimia 38 pekee ya wanawake ndio waliokiri kuwa na ufahamu juu ya masuala hayo.

**DW**



Mwananchi akiwa tayari kupatiwa chanjo. **PICHA: MTANDAO**

# No Mud, No Lotus: The ART of Transforming Suffering by Thich Nhat Hanh (Sanaa y

Inatoka Uk. 15

miili yetu, ndipo tunapokosa kujua mambo yanayotuzunguka na kwa kufanya hivi akili zetu huwa zinakuwa hazitulii na kwa kuwa hazitulii basi ni rahisi sana kufanya mambo ambayo yatazidisha mateso katika maisha yetu.

Wakati mwingine watu wanaendelea kuwa katika mateso makubwa sababu ya kumbukumbu ambazo wamezipitia huko nyuma... huenda ni kufanyiwa unyama, kukataliwa, kuondokewa na wapendwa wao, ajali na mengine mengi yanayofanana nayo.

Kinachoongeza maumivu zaidi kwa mnyama aliyechomwa mkuki ni ule mkuki kuchoma tena mara ya pili hapo hapo.

Nini maana yake? Katika maisha watu wanajiongezea mateso zaidi pale wanaporuhusu tafsiri ya kitu hicho, pale wanapoweka hisia zao na hata vile hofu wanazozijenga hapo hapo inakuwa kama mkuki wa pili katika kidonda ambacho maumivu yake ni zaidi ya mkuki wa kwanza.

Njia bora ya kulitatua tatizo ni kuliona tatizo katika uhalisia wake kama lilivyo. Wengi wanapata mateso zaidi sababu hawaoni tatizo kama lilivyo.

Jifunze kuachilia yaliyopita na uanze kuishi sasa. Huwezi kubadili yaliyopita mbali na kuweza kujifunza somo kwa yaliyokwishatokea.

**MAPUMZIKO**

Unahitaji kuwa na hali ya mapumziko katika maisha yako, ili upate muda wa kufahamu mengi yanayoendelea katika maisha yako kwa ukaribu zaidi.

Maana pale unapokosa muda wa kupumzika, kuna vitu unaweza ukawa ukiendelea kuvifanya kwa makosa bila kujua.

Kila siku jifunze kufanya katika ubora, kufanya matendo ya upendo na furaha ambayo yatatia thamani kwa maisha ya watu na njia hii bora sana kulisha furaha yako kwa hatua za juu zaidi kila siku katika maisha.

Unahitaji ujue kufanya juhudi na mojawapo ni kujipa utulivu mkubwa na ukae uandike maono yako makubwa na kuangalia ulipofikia.

Maana umekuwa unakimbizana sana na maisha

## JE, WAJUA?



Aina nzuri ya mwonekano mzuri wa utunzaji wa sharubu kwa mtu mwenye kipara. **PICHA: MTANDAO**

# Aina bora za utunzaji wa sharubu

KUFUGA sharubu na sharafa ni jambo linalopendwa na wanaume wengi duniani.

Pamoja na hilo, suala la kufuga sharubu na sharafa linaonekana kuwa ni tatizo kwa wafugaji, hasa wakizingatia namna nywele hizo zitakavyotengeneza mwonekano wao.

Mathalani, kwa mujibu wa utafiti ulioendeshwa na Taasisi ya ChilliSauce ya Uingereza, imeonekana kuwa asilimia 50 ya wanaume nchini Uingereza hupata shida sana kubuni aina ya utunzaji wa sharubu na sharafa zao.

Utafiti huo ulioshirikisha wanaume 12,000, unaonyesha kuwa asilimia 60 ya wanaume wa Wales wanafurahishwa na mwonekano wa sharubu zao, wakati asilimia 70 ya wanaume wa Jiji la London, wao hukerwa na mwonekano wa sharubu zao.

Utafiti huo pia unaonyesha kuwa wanaume wengi nchini Marekani wenyewe hupenda kufuga sharubu na sharafa zao kwa namna ya kuchekesha wakiwa na mitindo mingi ya kuchangamsha nyuso zao.

Kwa kuliona hilo, nchini Uingereza yameanzishwa mashindano maalumu ya ufugaji wa sharubu na sharafa pamoja na utunzaji wa nywele kwa watu wenye vipara.

Mashindano hayo yaitwayo November, hufanyika mwezi Novemba na hujumuisha watu kutoka katika nchi zinazojenga himaya ya nchi ya Uingereza yakiwa pia yanafuatiliwa na mashabiki katika nchi nyingine za Ulaya na Marekani.

Ni kupitia mashindano hayo ndipo watu wengi hupata mfano wa chaguo bora la aina ya ufugaji wa sharubu pamoja na utunzaji wa 'mabaki' ya nywele zinazozunguka kichwani kwa watu wenye vipara kama ilivyo kwenye mifano ya picha.

# UTAFITI

## WATUMIAJI 'APPS' ZA WAPENZI HUTUMIA NJIA HATARISHI KUJENGA MWONEKANO

WANAWAKE na wanaume wanaotumia 'apps' ili kupata wapenzi wanaowataka, wako hatarini kutumia njia zisizofaa kiafya ili kudhibiti au kupunguza mwili, utafiti unaeleza.

Utafiti uliofanywa nchini Marekani kwa watu 1,700 umebaini kwamba kujitapisha, matumizi ya dawa za kupunguza mwili na kufunga kula ni njia zinazotumika kwa wingi.

Apps za kutafuta wenza zimekuwa maarufu sana kutokana na kuwepo kwa mitandao ya simu na intaneti miaka ya hivi karibuni.



Watu hutumia apps kuwapata wenzi wanaofikiri wanawafaa kwa kutazama mwonekano wa miili yao pia.

Katika utafiti huu, uliochapishwa kwenye jarida liitwalo Eating Disorders, watafiti wamefananisha tabia za watu wanaotumia apps kutafuta wenza na wasiotumia 'application' hizo.

Wakabaini kuwa watumiaji wa 'application' hizo wana namna sita za kudhibiti miili yao ili kuwa na mwonekano mzuri kwenye mitandao.

Kwamba hutumia njia ya kujitapisha, dawa za kuharisha, kufunga kula, dawa za kujikondesha na dawa za kujenga miili au misuli yao.

Kutoka kwa watu wazima waliohojiwa 1,726 wanawake na 209 wanaume wanasema wanatumia apps kupata wenza.

Kwenye kundi hilo, karibu nusu ya wanaume na wanawake wameripoti kwamba wanatumia njia ya kufunga kula, ili wasiwe na uzito mkubwa na mmoja kati ya wanawake watano na mwanaume mmoja kati ya watatu wanasema hujitapisha ili kuepuka kuwa na uzito wautakao.

Mmoja kati ya wanawake wanne na asilimia 40 ya wanaume, wanatumia dawa za kuharisha.

Dk. Alvin Tran aliyeongoza jopo la watafiti anasema utafiti umebaini kwamba kuna matumizi ya hali ya juu ya njia hizi miongoni mwa watumiaji.

**MWONEKANO WA MWILI**

Dk. Tran anasema: "Wakati hatujui kama watu kwenye utafiti huu walikuwa wakitumia njia hizi kabla ya kuanza kutumia apps za kuwatafuta wapenzi, tunahofu kwamba matumizi yake yanaweza kuzaa tabia hizo," anaongeza: "Hapa tunapaswa kutambua madhara ya kutumia apps za wapenzi na mabadiliko ya tabia katika kudhibiti mwonekano wa mwili."

Anabainisha kuwa ni muhimu kutilia maanani kwamba utafiti huu hauthibitishi mahusiano ya moja kwa moja kati ya apps na tabia zisizofaa kiafya katika kudhibiti uzito.

"Hata hivyo, ni muhimu kwa watumiaji wa apps ambao wanaweza kuwa hatarini kuingia kwenye tabia za kutokula vya kutosha, wakapata msaada kuondokana na tabia hiyo," anasema.

**BBC**

## a kubadili mateso kuwa ushindi na furaha)


kiasi kwamba umekosa hata muda wa kujisikiliza unataka ufike wapi na wapi uendako!

Na mwisho inatia moyo sana pale ambapo katika mateso tunayopitia watu kama hawa wasemao nipo kwa ajili yako, najua unapitia magumu lakini nina furaha kuwa utashinda.

Mateso yanapokuwa na mwitikio wa umoja na kuwa tayari kushughulika nayo huwa ni faraja na matumaini makubwa zaidi.

Yaelewe maisha katika pande zake zote mbili kuwa furaha na mateso ni sehemu ya maisha makamilifu.

***Na Mchambuzi wa vitabu***
***Dk. Raymond Nusura Mgeni 2019***
***+255 676 559 211***
***raymondpoet@yahoo.com***




# UTAFITI: Pesa chafu na simu za mkononi ni hatari kwa afya yako

PESA chafu na simu za mkononi zinaweza kuwa hatari kubwa kwa afya yako, watafiti wanaonya.

Wanasayansi wanasema pesa hususani zile za thamani ndogo, zinasababisha magonjwa mengi ya kuhara miongoni mwa watu wanaotumia chakula kinachoandaliwa kwenye maeneo ya hoteli, migahawa na vilabu.

**WANAOANDAA CHAKULA**

Utafiti uliofanywa miongoni mwa waandaaji 395 wa chakula katika maeneo 15 tofauti ya Jiji la Nairobi, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Jomo Kenyatta na kile cha Teknolojia nchini Kenya (JKUAT), kwa ushirikiano na Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Tiba ya Kenya (Kemri), na Kitengo cha Utafiti wa Matibabu cha Jeshi la Marekani nchini humo.

Unabainisha kwamba wanaoshughulikia chakula cha umma kwa ujumla wanapaswa kuhamasishwa juu ya hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na kugawa chakula baada ya kushika pesa au simu za mkononi.

Utafiti huo unaonyesha kuwa kwa sababu pesa na simu za mkononi huwa hazisafishwi, hugeuka kuwa maficho ya vimelea wa magonjwa ambao husababisha sumu kwenye vyakula.

Baada ya kupima sarafu kuanzia shilingi moja hadi noti ya shilingi 1,000 zinazotumiwa jijini Nairobi, ripoti ilifichua kuwa sarafu za shilingi 5, 10, 20 ndizo zilizokuwa chafu zaidi, zikifuatiwa na noti za shilingi 50, 100 na 200.

"Nyingi kati ya pesa pamoja na simu zilikuwa na bakteria wanaosababisha magonjwa."

Matokeo ya utafiti huo yaliwasilishwa kwenye mkutano wa saba wa afya na sayansi wa Afrika Mashariki, uliofanyika jijini Dar es Salaam, Tanzania mwezi Machi.

Na kibaya zaidi utafiti huo unasema ni kwa wahudumu wa vyakula, hususan wanaogawa vyakula kwa wateja pamoja na wapishi ambao ilibainika kuwa hawazingatii usafi na hasa baada ya kupokea simu zao za mkononi.

Wakati wa utafiti huo, washiriki 34 walipatikana na magonjwa tofauti kama vile kikohozi, kichomi na maumivu ya tumbo na utumbo (gastroenteritis).

Si kwamba magonjwa haya yanasababisha matatizo tu kwa wagonjwa, bali ni magonjwa yanayoweza kuambukizwa kutoka kwa mwandaaji wa chakula, anayegawa chakula au mpishi wa chakula anayeumwa.


Wapishi wakiwa kazini, wakihudumia wateja wao. **PICHA:MTANDAO**

Aidha, ilibainika kuwa asilimia 60 ya waliofanyiwa utafiti hawakuwa wamenawa mikono yao baada ya kupokea simu za mkononi.

Kwa kawaida, waandaaji wa chakula hawapaswi kupokea simu.

"Wanaoshughulikia chakula cha umma kwa ujumla hawana budi kuhamasishwa juu ya hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na kugawa chakula baada ya kushika pesa au simu za mkononi," unaonya utafiti.

Mnamo mwaka 2009, Taasisi ya Utafiti wa Tiba nchini Kenya (Kemri), ilifanya utafiti sawa na huo jijini Nairobi na kugundua kuwa simu za mkononi zina vimelea wa magonjwa kwa kiasi kikubwa, baadhi zikiwa hata na vimelea wanaopatikana kwenye kinyesi.

**MACHINJIO HATARI ZAIDI**

Nyingi kati ya pesa zilizopatikana na vimelea zilikuwa ni sarafu zilizochukuliwa kutoka kwenye machinjio, zikifuatiwa na zile zilizokusanywa kutoka kwa wauzaji wa mahindi kando ya barabara na vyakula vinavyouzwa kwenye maduka madogo (vioski).

Kwa mujibu wa Dk. Richard Korir, Ofisa wa Utafiti katika Kituo cha Kitengo cha Utafiti wa Makrobailojia na mwandishi wa utafiti huo, kutofuatwa kwa kanuni ya kuosha mikono na usafi kwa ujumla kunasababisha kuhamishwa kwa vimelea hawa wa magonjwa kwenda kwenye chakula ambacho bila shaka kinaliwa.

Utafiti huo ulifanywa na kuwasilishwa na mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kilimo (JKUAT) ambaye aliangazia aina mbalimbali za bakteria wanaopatikana katika mazingira, chakula, utumbo na ngozi kwa wanyama na binadamu.

**SIMU ZA MKONONI ZINA** MAAMBUKIZI ZAIDI

Ingawa vimelea vingi vya bakteria hawa si hatari, baadhi wanaweza kusababisha magonjwa kama vile homa ya matumbo, sumu ya chakula na maambukizi ya ngozi.

"Shilingi 1,000 ndiyo yenye maambukizi ya chini kwa sababu hutumiwa mara chache, huku sarafu ya shilingi moja ikiwa pia haina uchafu mwingi na thamani yake imeshuka kwa hiyo haitumiwi sana," anabainisha Dk. Korir.

Sarafu zenye thamani ya chini ndizo zilizokutwa na uchafu mwingi kuliko zile zenye thamani ya juu.

Vimelea waliopatikana zaidi walikuwa ni wa jamii ya staphylococcus, wanaofahamika kusababisha maambukizi ya ngozi, moyo na mifupa, sumu ya chakula, kichomi na sumu ya mwili wa binadamu.

Bakteria waliopatikana katika chakula pia ni jamii ya Escherichia Coli (E. coli), ambao hupatikana katika mazingira ya chakula, utumbo wa binadamu na wanyama.

Wengi kati ya vimelea hao si hatari, lakini wanaweza kukufanya uwe mgonjwa. La kushangaza ni kwamba, Dk. Korir anasema, zikilinganishwa na sumu za pesa, simu za mkononi ndio mbaya zaidi inapokuja katika suala la maambukizi ya magonjwa.

"Watu wengi hawadhani kuwa simu ni chafu au ni chanzo cha kuambukizwa magonjwa... kwa hiyo, mara nyingi hawazingatii usafi baada ya kuzitumia," anasema.

Simu ziligundulika kuwa na bakteria 12 baada ya kukusanywa na kuchunguzwa na zaidi bakteria aina ya Staphylococcus, ambao mara nyingi hupatikana katika nywele na ngozi.

Kutofuatwa kwa kanuni ya kuosha mikono na usafi kwa ujumla kunasababisha kuhamishwa kwa vimelea hawa wa magonjwa kwenye chakula, umebaini utafiti.

***BBC***






WADAU
## SABATO KASIKA

# KUSHUKA kwa maendeleo ya kielimu darasani kwa mtoto ni matokeo ya changamoto tofauti. Je, wazazi wachukue hatua gani? Wadau wanajadili.



**CHARITY MANOKO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWANZA kabisa ni muhimu kuelewa kwamba maendeleo ya mtoto shuleni yanategemea ukaribu wa wazazi na walezi. Hao wanapaswa kuhakikisha mtoto amefanyiwa maandalizi ya kwenda shule kuanzia sare, madaftari na vitu vingine vya muhimu awapo shuleni. Si vibaya kuwa na chakula kwa sababu akiwa na njaa hawezi kufuatilia masomo vizuri. Kikubwa zaidi ni afya njema. Kwa hiyo achunguzwe afya yake na kumjenga kisaikolojia. Awapo nyumbani ni lazima apate muda wa kulala mapema, kujisomea na pia kucheza katika mazingira hayo. Yakizingatiwa hayo ni lazima atafanya vizuri katika masomo yake. Wapo baadhi ya wazazi hawataki kuona mtoto akicheza wanataka asome tu au kumzidishia majukumu mengine. Kufanya hivyo hakuwezi kumsaidia. Lingine linalotakiwa kufanyika ni ushirikiano wa karibu kati ya walimu na wazazi. Wazazi wahudhurie vikao vinavyoitishwa shuleni, kwani kuhudhuria vikao hivyo wanaweza kujua mengi kuhusu tabia za watoto wao. Ninasema hivyo kwa sababu mtoto anaweza kuonyesha tabia fulani nyumbani, lakini akienda shuleni anabadilika na kufanya vituko. Hayo ni mambo ya msingi yanayotakiwa kuzingatiwa na wazazi wenzangu kwa ajili ya maendeleo mazuri ya watoto wao shuleni.




**ERNEST PAUL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SUALA la mtoto kushuka kielimu inategemea mazingira anayoishi pamoja na wazazi kama wanamfuatilia au wanamuacha afanye lolote atakalo. Wapo baadhi ya watoto, ambao wanajua vipindi vyote vya televisheni kuliko vya shule. Maana yake ni kwamba wameachiwa kuwa huru kupita kiasi. Sasa kama hali inakuwa hivyo mtoto hawezi kushuka kielimu? Jambo lingine ni mazingira ya shule anayosoma mtoto kama kuna walimu wa kutosha na huduma zote za msingi kwenye elimu. Kama shule itakuwa na walimu wachache na pia hawafuatilii wanafunzi wao, basi maendeleo ya mtoto yatakuwa mabovu. Jambo la msingi ambalo sisi wazazi tunapaswa kulitambua ni kwamba ufuatiliaji wa maendeleo ya mwanafunzi shuleni unaanzia nyumbani. Mwalimu ni mzazi wa pili, wote hawa wanatakiwa kushirikiana kuhakikisha kila mwanafunzi anatimiza wajibu wake vizuri awapo shuleni na nyumbani. Mimi nina uzoefu katika hili, kwani mwanangu naye aliwahi kufanya vibaya nikafuatilia, nikagundua tatizo na kulitafutia ufumbuzi, sasa maendeleo yake ni mazuri. Nilipata ushirikiano kutoka kwa walimu kwa sababu niko karibu nao. Tuwafanye walimu kuwa rafiki zetu badala ya kuwaona kama maadui, vinginevyo hawawezi kutupa ushirikiano hata kama wanaona watoto wetu wanafanya vitendo viovu.



**RAINAS MGUSI (MWALIMU MKUU S/M SIMAKITONGO, MAGU MWANZA)**

JAMBO la kwanza ambalo kila mmoja wetu anapaswa kujua ni maana ya elimu. Kimsingi elimu kwa kifupi ina maana pana ikitajwa kuwa ni tendo au uzoefu wenye athari ya kujenga akili, tabia au uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi. Katika dhana ya kiufundi, elimu ni njia, ambayo hutumiwa makusudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Ndio maana elimu imekuwa na kaulimbiu nyingi sana ikiwamo ya elimu ni ufunguo wa maisha. Kwa upande wa haki za msingi, elimu inaelezwa kuwa ni moja ya haki za msingi za mtoto. Hivyo kila mzazi anatakiwa kuhakikisha mtoto wake anapata elimu itakayomwezesha kupiga hatua kutoka sehemu moja kwenda nyingine katika maisha yake ya baadaye, kwa maana ya maendeleo. Pia suala la mtoto kushuka kielimu linaweza kuwa na sababu nyingi kama vile makundi anayoshirikiana nayo shuleni au jinsi anavyoachiwa afanye anavyotaka akiwa nyumbani. Kwa hiyo wazazi na walezi wanatakiwa kuwa karibu na watoto wao kwa kufuatilia maendeleo ya taaluma ili taifa liweze kuwa na vijana wasomi watakaoliongoza hapo baadaye. Ninasema hivyo kwasababu kujifunza ni kutaka kujua juu ya jambo fulani ambalo hukulijua kabla. Nimalizie kwa kusema kwamba jukumu la wazazi ni kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, wasisubiri hadi washuke kielimu.



**GERMANA MVUNGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

BAADHI ya wazazi hawana mwamko wa elimu hadi waone watoto wao wanashuka kielimu ndipo wanaanza kuwafuatilia shuleni. Hilo ni tatizo kwa sababu kufuatilia maendeleo ya mtoto siyo hadi afanye vibaya, hata kama anafanya vizuri, mzazi hatakiwi kubweteka na badala yake anatakiwa kufuatilia maendeleo hayo. Ni lazima mzazi ujue ni kwa nini mtoto anafanya vizuri. Je, anaibia kwa wenzake au ni uwezo alinao darasani. Lakini tukisubiri wafanye vibaya ndipo tushtuke na kuanza kufuatilia tutakuwa tumechelewa. Ukifuatilia sana utagundua kuwa wenye mtindo huo wa kufuatilia maendeleo ya watoto shuleni mara baada ya kushuka kielimu ni wale ambao hawana mwamko wa elimu na pia hawana uhusiano mzuri na walimu. Kwa hiyo jibu la swali lako kwamba mzazi, ambaye anatambua umuhimu wa elimu ni lazima atachukua hatua ikiwa ni pamoja na kumuuliza mwanaye kwa nini inakuwa hivyo na kisha atakwenda hadi shuleni kufuatilia na hatimaye atajua chanzo cha tatizo na kukifanyia kazi kutegemea na chanzo chake. Kikubwa zaidi ni kwamba wazazi wanatakiwa kufuatilia maendeleo ya watoto wao wakati wote, iwe wanafanya vizuri darasani au vibaya, kwani wanatakiwa kutiwa moyo ili waongeze bidii katika masomo badala ya kuwaacha wafanye wanavyotaka, kwani mwisho wake ndio huo, ambao unaweza kusababisha wakashuka kielimu.



**JUMA HAMIS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SHULE ya kwanza ya mtoto ni mzazi au mlezi. Hapa ninataka kuweka wazi wajibu wa mzazi au mlezi kwa mtoto, kwani ndio wanaohusika kusaidia watoto kupata elimu. Hivyo wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kabla ya makundi mengine yoyote. Watu hawa wana wajibu wa kumwandaa mtoto kwa ajili ya kupokea maarifa na kumjengea utayari wa kujifunza, kwani huo ndio wajibu muhimu na wa kwanza katika maisha ya malezi. Watu hawa wakitimiza wajibu wao vizuri wanaweza kumsaidia mtoto/watoto kufikia ndoto zao, hao ndio walimu wa kwanza kwa mtoto, wanaweza kumjenga kuwa wa aina fulani. Kwasababu ni kawaida kwa watoto kuiga tabia za wazazi au walezi wao na hata watu wengine wanaowazunguka kwenye maeneo wanayoishi. Hivyo ni muhimu wazazi na walezi kutambua wajibu wao kwenye malezi wakitambua kuwa elimu ni msingi mzuri wa kumkuza na kumwezesha mtoto kukua kwa kufuata maadili na kuwa raia mwema. Kinachotakiwa ni kwamba mzazi anapoona mtoto wake anashuka kielimu ni kuchukua hatua haraka iwezekanavyo kwa kufuatilia shuleni ili kujua kuna tatizo gani badala ya kuwaachia jukumu hilo walimu. Mzazi au mlezi ana nafasi kubwa kwa maendeleo ya mtoto kielimu kama nilivyosema awali. Yaani mzazi na mlezi wanatakiwa kushirikiana kwa karibu wakitambua kuwa kila mmoja ana sehemu yake katika maendeleo ya elimu ya mtoto.

# Waelezwa fursa kilimo cha maharage

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wadogo wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kujikita kwenye kilimo cha maharage kwa kuwa zao hilo kwa sasa lina soko kubwa duniani.

Ushauri huo ulitolewa juzi jijini Mbeya na watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Uyole, wakati wa kikao na wadau wa zao hilo kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mtafiti wa maharage, Dk. Mary Ndimbo, alisema zao la maharange mbali na kutumika kama chakula, pia ni la biashara ambalo linaweza kumwingizia mkulima kipato.

Alisema zao hilo soko lake lipo katika maeneo mbalimbali duniani, na kwamba wakulima wanatakiwa kuzalisha bila kuogopa kukosa soko kwa vile uzalishaji uliopo hautoshelezi hata soko la ndani.

"Kwa sasa tunazungumzia Tanzania ya viwanda, maharage yanaweza kusindikwa na yakauzwa yakiwa yameongezewa thamani, teknolojia ya sasa kuna teknolojia nzuri za kilimo ambazo wakulima wetu wakizitumia wanaweza wakajiongezea tija," alisema Dk. Ndimbo.

Mratibu wa zao la maharage nchini, Dk. Rose Mongi, aliwataka watafiti na wazalishaji wa mbegu kuhakikisha wakulima wanapatiwa mbegu zilizobora ili wazalishe zao hilo kwa wingi na kupata tija tofauti na ilivyo sasa.

Aliwataka pia wajasiriamali kubuni namna mbalimbali za kusindika zao hilo ili ifike mahali wamiliki viwanda vya kuchakata zao hilo kuunga mkono juhudi za serikali za uchumi wa viwanda.

Dk. Rose alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazozalisha kwa wingi mazao ya jamii ya mikunde yakiwamo maharage, lakini bado uzalishaji wake haukidhi mahitaji ya soko kutokana na mahitaji kuwa makubwa kuliko uzalishaji.

"Nategemea kuwa katika utaratibu huu wa kuanzisha viwanda nchini kimojawapo kitakuwa ni cha kuchakata maharage, serikali ipo tayari kumuunga mkono mtu yeyote atakayeanzisha kiwanda cha aina hiyo ikiwa ni pamoja na kumtafutia soko," alisema Dk. Rose.

Mmoja wa wajasiriamali kutoka mkoani Rukwa, Theresia Mkondolwa, alisema wanayatumia maharage kutengeneza sambusa kwa kuchanganya na viungo ikiwamo karoti, vitunguu na viungo vingine vya kawaida.

Vilevile alisema wanayatumia kutengeneza maandazi, biscuit, keki na unga wa lishe na kwamba ubunifu huo umewasaidia kujiongezea kipato kwenye familia zao.

Mtafiti wa kilimo kutoka Rwanda, Lyogo Jackron, alisema Tanzania ndio nchi inayoongoza kwa kuzalisha maharage bora Afrika na yeye yupo nchini kwa ajili ya kujifunza mbinu za kisasa za kilimo cha zao hilo.

Alisema atahakikisha anaenda kuzitumia mbinu atakazokuwa amejifunza nchini kwenda kuzalisha zao hilo kwao pamoja na kuwafundisha wenzake.



Baadhi ya maofisa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Uyole jijini Mbeya wakikagua moja ya mashamba darasa ya kikundi cha wakulima cha Mshebhaje kilichoko Kata ya Mshewe wilayani Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# Kijiji chajivunia afya wajawazito, watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa Kijiji cha Uturo, Kata ya Mapogoro katika Wilaya ya Mbarali, wanajivunia kijiji chao kufikisha miaka 20 bila kutokea kifo cha mjamzito wala mtoto na kuwa cha mfano nchini.

Kijiji hicho kimejizolea sifa hiyo kutokana na mikakati mbalimbali ambayo wamejiwekea kwa kushirikiana na uongozi wa zahanati ya kijiiji inayohudumia zaidi ya wananchi 12,000 wakiwamo wa kutoka vijiji jirani vya Ukwama na Ukwavila.

Wakizungumza wakati wa ziara ya makatibu wakuu wa Wizara ya Afya, Dk. Zainab Chaula wa Tanzania Bara na Asha Abdallah wa Tanzania Visiwani, wananchi hao walieleza baadhi ya mikakati iliyowafikisha katika mafanikio hayo.

Mmoja wa wananchi hao, Sadi Mwasunga alisema awali kijiji hicho kilikuwa kinakabiliwa na changamoto ya vifo vya mama na mtoto kutokana na hali ya huduma za afya kutokuwa nzuri.

Alisema wajawazito walikuwa wanakufa kutokana na kujifungulia kwa wakunga wa jadi na kwamba tangu mwaka 1999 baada ya aliyekuwa Mganga Mfawidhi wa Zahanati hiyo, Dk. Wilson Chotamganga, kuwaelimisha hakijawahi kutokea kifo tena.

Alisema moja kati ya mbinu walizopewa na Chotamganga ambazo wanazitumia mpaka sasa ni kuhakikisha wajawazito wanahudhuria kliniki kila mwezi kuanzia mwezi wa kwanza wanapobaini kuwa ni wajawazito.

Mbinu zingine ni kuhakikisha wajawazito wanahudhuria pamoja na wenza wao kwenda kupima kliniki kwa mara ya kwanza, ili wanaume pia washirikishwe kwenye zoezi hilo.

"Tunamshukuru ndugu yetu Chotamganga ambaye alitubadilisha sana, wanawake na watoto walikuwa wanafia kwa wakunga wa jadi ambao ndio tulikuwa tunawatumia tangu enzi, lakini tangu alipokuja huyu bwana na akatuelimisha tunashukuru tulibadilika na sasa tunaheshimika nchi nzima," alisema Mwasunga.

Naye Kesheni Kivambe, alisema katika kijiji hicho zimeundwa kamati maalumu za wanawake ambazo zinafuatilia maendeleo ya kila mjamzito, ili kuhakikisha wote wanahudhuria kliniki na kujifungulia hospitali badala ya ilivyokuwa awali.

# Ziara ya Magufuli yainufaisha shule

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SHULE ya Msingi Ilenge katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, imeneemeka na ziara ya Rais John Magufuli, kwa kupatiwa mashine ya kudurufu maandishi na kuunganishiwa umeme.

Akiwa ziarani wilayani humo Aprili 30, mwaka huu, Rais Magufuli alizindua kiwanda cha maparachichi cha Rungwe Avocado na ndipo uongozi wa Shule ya Msingi Ilengo ambayo ipo jirani na kiwanda hicho ukamuomba awasaidie umeme na mashine ya photocopy.

Baada ya ombi hilo, Rais Magufuli alichangia Sh. 2,000,000 kwa maelekezo kuwa Sh. 1,000,000 ni kwa ajili ya kuunganishiwa umeme na Sh. 1,000,000 ununuzi wa mashine hiyo ya kudurufu maandishi.

Kufuatia mchango huo, Mbunge wa Rungwe, Saul Amon (CCM), aliahidi kumuunga mkono Rais kununua mashine hiyo ili kuiwezesha shule hiyo kuwa na kifaa hicho muhimu kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake.

Akiwasilisha mashine hiyo kwa uongozi wa shule hiyo, juzi Mbunge wa Rungwe Saul alimshukuru Rais Magufuli kwa kusaidia upatikanaji wa mashine hiyo.

Alisema baada ya kuchangiwa fedha na Rais, aliunganisha na zake na kwenda kuinunua mashine hiyo kwa shilingi milioni 2.27 na akautaka uongozi wa shule hiyo kuitumia vizuri mashine hiyo ili idumu na kuwasaidia kwa muda mrefu.

"Nimekuja kutimiza ahadi ambayo niliahidi mbele ya Rais ya kuwanunulia mashine hii, hivyo ni jambo la kumshukuru Rais maana alipita maeneo mengi, na sisi hapa ndio tumeneemeka zaidi ya wenzetu, tuitunze vizuri mashine hii ili idumu," alisema Saul.

Akipokea mashine hiyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ilenge, David Mwaipopo, alimshukuru Rais Magufuli kwa msaada huo, na kwamba watahakikisha wanamuunga mkono ipasavyo.

Alisema baada ya Rais kuondoka mkoani Mbeya shule yake iliunganishiwa umeme baada ya siku 10, kitu ambacho walikuwa hawajawahi kukitarajia, na kwamba sasa wanafurahia matunda ya ziara ya kiongozi huyo.

"Kuletewa mashine hii ni kiashiria kuwa maombi tuliyomuomba Rais wetu yametimizwa kwa asilimia 100, tunashukuru na tunamhakikishia kuwa tutaendelea kumuunga mkono kwa kuchapa kazi kama anayosisitiza siku zote," alisema Mwalimu Mwaipopo.

Alisema tangu Rais Magufuli aingie madarakani, ameonyesha upendo kwa wanafunzi kwa kuamua kuanza kutekeleza sera ya elimu bila malipo, na sasa kila akienda kwenye ziara mkoa wowote lazima achangie maendeleo ya elimu.





# Serikali yawakumbuka wajane

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeagiza asilimia nne kati ya 10 za mikopo inayotolewa na halmashauri nchini wapewe wajane, ili kuwaepusha na mikopo yenye riba kubwa ambayo inachangia kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Aidha,serikali imeagiza wanawake ambao wana ndoa za asili wajitokeze kwenda kufunga ndoa halali ili waweze kupata cheti cha kifo na cha ndoa ambavyo vitawasaidia kudai urithi watakapofiwa na waume zao.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani yaliyofanyika jijini hapa, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema serikali imeamua kutoa agizo hilo ili kusaidia kinamama kuendesha maisha yao kupitia mikopo ya serikali ambayo ina unafuu.

Dk. Ndugulile aliziagiza halmashauri kupitia wizara husika zifanye utaratibu wa kutoa elimu kwa wajane jinsi ya kupata mikopo hiyo ambayo itachangia kupunguza ukali wa maisha baada ya kufiwa na waume zao.

"Kuanzia sasa hakuna sababu ya wajane hao kwenda kukopa mitaani wakati serikali inatoa mikopo ambayo haina riba katika halmashauri, kinachotakiwa ni asasi hizo kutoa elimu kwa wajane ili wajue jinsi gani ya kupata mikopo hiyo," alisema Dk. Ndugulile.

Akizungumzia kuhusiana na suala zima la wanawake kuwa na ndoa za asili zisizotambulika, Dk. Ndugulile alisema wanatakiwa kwenda kufunga ndoa halali ili waweze kupata cheti cha kifo, na cha ndoa ambavyo vitawasaidia kudai urithi hapo baadaye.

Alisema asasi zisizo za kiserikali zinapaswa kuwapa elimu wanawake hata kabla ya kupata matatizo ya ujane juu ya kufunga ndoa halali ikiwamo kupata cheti cha ndoa ambacho kitakuwa kinga hapo baadaye ya kumsaidia kupata cha kifo ambavyo vyote vitakuwa ni vielelezo tosha vya yeye kupata haki yake ya msingi.

"Tunaziomba asasi zisizo za kiserikali zishirikiane na wizara kuhakikisha wanatoa elimu kwa kinamama kuhusu kuwa na ndoa halali," alisema Dk. Ndugulile.

Alisema wakifanya hivyo watakuwa wamesaidia kupunguza manyanyaso dhidi ya wanawake kutokana na mila potofu ambazo ni kandamizi kwa wanawake ambazo hupelekea kupokonywa baadhi ya mali ambazo hazihamishiki kipindi wanapofiwa na waume zao.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. John Jingu, alisema Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), inakadiria kuwa idadi ya wajane Tanzania ni 400,000 sawa na asilimia 3.1 ya wanawake wote nchini ambao wanakadiriwa kuwa ni milioni 28.5 kwa mwaka 2019.

Dk. Jingu alisema serikali inatambua kuwa wajane ni kundi muhimu katika jamii, ndio maana inaadhimisha siku hiyo pamoja na nchi nyingine duniani, ili kujua kuweza kujua changamoto zinazowakabili wajane na kuzitafutia ufumbuzi.



Mwezeshaji wa kongamano la lugha ya alama, Mchungaji Kelebi Mhawi, akitoa elimu ya semina kwa watoa maamuzi kutoka sekta mbalimbali iliyofanyika Wilaya ya Kondoa kwa ajili ya kuboresha mawasiliano ya lugha. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Ushauri uchakataji wa majitaka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuanzisha miradi ya pamoja ya uchakataji wa majitaka ili kusaidia kupunguza gharama za utengenezaji wa mifumo inayohitajika kwa wananchi mmoja mmoja.

Wito huo ulitolewa na Mhandisi Abdul-Nassir Rizeg

kutoka kampuni ya uchakataji majitaka ya Wastewater Solution kupitia mfumo wa Oswams, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Mhandisi Rizeg, alisema mradi wa uchakataji majitaka unaweza kuiepusha jamii na magonjwa ya milipuko kama kipindupindu pamoja na kuzuia upotevu wa maji bila sababu na kupunguza kasi ya uchafuzi wa mazingira, vyanzo vya maji na mabadiliko ya tabianchi.

"Mtu akitumia majisafi lita 1,000 kwa siku anazalisha majitaka lita 800 sawa na asilimia 80 kwa siku ambayo huingia ardhini, lakini mengine huenda kwenye vyanzo vya maji kwa wale wanaoishi kandokando ya sehemu hizo na kuvichafua hali ambayo inasababisha maji yale kuwa siyo salama na wakati mwingine kukauka kabisa," alisema Mhandisi Rizeg.

Alifafanua uchakataji wa majitaka unaweza kuisaidia jamii kutumia kiasi hicho cha majitaka yanayopotea kila siku kwa kuyatumia tena katika shughuli za umwagiliaji, ufugaji wa samaki, uoshaji magari, kuflashia vyoo, upendezeshaji miji kwa kumwagilia bustani na shughuli za ujenzi.

Alisema pia mfumo huo unaepusha kabisa zoezi la usafirishaji wa majitaka kiholela kwa kuwa hatua zote za uchakataji zifanyika sehemu husika majitaka yalipozalishiwa.

Aidha, alibainisha kuwa sehemu za machinjio zinachangia zaidi uchafuzi wa mazingira kwa kuwa uzalisha majitaka kwa wingi na hawajui namna ya kuyadhibiti, hivyo mfumo huo unahitajika zaidi ili kudhibiti changamoto hiyo.

Mhandisi huyo alisema viwanda vya maziwa navyo vinazalisha majitaka kwa wingi na kuchangia uchafuzi wa mazingira, na kwamba uzalishaji wa lita moja ya maziwa unazalisha majitaka lita tatu.

# Shule iliyokarabatiwa kwa mil. 900/- yakabidhiwa serikalini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imeikabidhi serikali majengo ya Shule ya Sekondari Dodoma baada ya kukamilika kwa ukarabati uliogharimu Sh. milioni 900.

Akikabidhi majengo hayo, Mkurugenzi wa mradi huo, Waziri Salum, alisema kukamilika kwa ukarabati huo kutawezesha shule hiyo kuwa na miundombinu ya kisasa.

Katika hatua nyingine, alisema serikali imetenga Sh. billioni 2, kwa ajili ya ukarabati wa shule tano za msingi jijini Dodoma ili kuboresha sekta ya elimu.

"Agosti kazi inaanza, serikali imetenga Sh. bilioni 2, tunaenda kukarabati shule tano, ambapo kwa shule moja tunapeleka Sh. milioni 400, ni kiasi kingi sana cha fedha kwa ajili ya ukarabati na upanauzi wa shule hizi," alieleza Salum.

Akiyapokea majengo hayo Mkuu wa Shule hiyo, Amani Mfaume, alishukuru hatua ya serikali kwa kuweka bajeti kubwa kwenye sekta ya elimu, ambayo imelenga zaidi kuhakikisha inakarabati shule zote kongwe nchini.

"Hatunabudi kuishukuru sana serikali yetu chini ya Rais John Magufuli, kwa kuiwekea bajeti kubwa sekta ya elimu, hivyo kuifanya sekta ya kimkakati," alisema Mfaume.

Mfaume alisema kukamilika kwa majengo hayo kutachangia kuleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya elimu ukilinganisha na hapo awali, ambapo walikuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi kutokana na uchakavu wa baadhi ya miundombinu.

"Kwa sasa tunaelekea sehemu nzuri changamoto zimekwisha, madarasa mazuri, madawati yapo, waalimu wapo wa kutosha... kila kitu kipo tunachodaiwa sasa kwa upande wa serikali na wazazi wetu ni matokeo mazuri ya wanafunzi wetu tu," alisema.





Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, Ramadhan Chande (kulia), akizungumnza na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, jana.**PICHA: RAHMA SULEIMAN**.

# KMKM yataka kusaidia wazee, wenye mahitaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASKARI wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) wametakiwa kuwasaidia wazee pamoja na watu wenye mahitaji maalum.

Hayo yalielezwa na Katibu wa Kamati ya Sherehe na Mapambo wa KMKM, Luteni Kamanda Zuleikha Khamis Juma, wakati wa shughuli ya usafi wa mazingira uliofanywa na kikosi hicho katika hospitali ya walemavu wa akili Kidongo Chekundu na maeneo mengine katika Wilaya ya Mjini pamoja na Hospitali ya KMKM Kibweni, nyumba za wazee sebleni na nyumba za wazee Welezo.

Alisema Kikosi cha KMKM ni miongoni mwa jamii ya Wazanzibar na kinathamini sana uwapo wa wazee na watu wengine wote wenye mahitaji maalumu na kimepanga zoezi hilo kwa kuwa wanawajali sana wazee hao ambao ndio walioweza kujitolea na kulisaidia taifa kufika hapa lilipo.

Lamanda Juma alisema kwamba wazee wametoa mchango mkubwa katika kulijenga taifa, hivyo wanapaswa kuenziwa.

Naye katibu wa hospitali hiyo, Bhai Ibrahim Khamis, alikishukuru kikosi cha KMKM kwa kujitolea na kuweza kuwasaidia kufanya usafi katika maeneo ya hospitali hiyo ambayo yalikuwa machafu sana hasa kwa kipindi hiki cha magonjwa mbalimbali ya mlipuko.

Alisema wazee wameshatumia nguvu zao katika kuleta maendeleo hivyo kwa sasa wanahitaji kupumzika.

# Sababu za miti ya asili kutoweka zatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imesema kuwa miti mingi ya asili imetoweka katika maeneo tofauti kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo ujenzi katika maeneo ambayo hayakuwa ya makazi.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Makame Ussi, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Chakechake, aliyetaka kujua kama serikali inafahamu kuwa miti ya asili inatoweka.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa kuongezeka kwa mahitaji ya nishati ya kuni ambayo imepelekea miti mingi kukatwa.

Alieleza kuwa utaratibu uliokuwa ukitumika zamani kwa kilimo cha kuhama pia uliathiri miti mingi ya asili.

"Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia idara ya misitu na maliasili zisizorejesheka imeanza utaratibu wa kuotesha miche ya asili katika vitalu vyake pamoja na kuhamasisha watu binafsi kuotesha miti hiyo kupitia vitalu vyao," alisema.

Alisema kwa mwaka wa 2018/2019 serikali imeanza utaratibu wa kuotesha na kuipanda miti ya asili katika mashamba ya serikali na maeneo ya kuotesha na kuipanda miti ya asili katika mashamba ya serikali na maeneo mengine ya wananchi.

Alisema jumla ya miche 20,000 ya miti asili imeoteshwa katika vitalu vya serikali ikiwamo mibuyu, mipilipili, doriani, mizambarau, mikungu, miharita pamoja na mifuu inayotarajiwa kupandwa katika msimu wa mvua za masika.

Aidha, alisema kwa mujibu wa sensa ya miti ya wood biomass, minazi imepungua kutoka 5,205,600 mwaka 1997 hadi kufikia 3,332,000.

Alisema idadi ya miembe imeongezeka kwa Unguja kutoka 643,800 kwa mwaka 1997 hadi 1,255,000 kwa mwaka 2013 tofauti na Pemba ambapo idadi ya miembe imepungua katika kipindi hicho kutoka 920,000 hadi 527,000.

**Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia idara ya misitu na maliasili zisizorejesheka imeanza utaratibu wa kuotesha miche ya asili katika vitalu vyake pamoja na kuhamasisha watu binafsi kuotesha miti hiyo kupitia vitalu vyao**

# SMZ, Costech waibua maeneo ya utafiti

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis, alisema wizara yake kwa mwaka wa fedha 2018/19 ilishirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (Costech) kuibua maeneo 14 yanayohitaji kufanyiwa utafiti.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Konde, Omar Seif Abeid, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, akitaka kujua hadi sasa utafiti mbalimbali ulioratibiwa umefanyika.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2017/2019 ofisi yake ilianza kuyafanyia utafiti baadhi ya maeneo hayo ukiwamo utafiti wa kuangalia namna bora ya vijana kupatiwa mafunzo ya uzalishaji mali.

Alisema utafiti mwingine ni wa kubaini changamoto zinazopelekea wananchi kutofanya usajili wa matukio ya kijamii kwa wakati.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema utafiti wa aina mbili umeratibiwa ambao ni uwezo wa serikali za mitaa katika utekelezaji wa majukumu yake na tathmini ya utekelezaji wa ugatuzi kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID).

Alisema hadi sasa utafiti huo ulioratibiwa ambao ulihusu uwezo wa serikali za mitaa katika utekelezaji wa majukumu na tathmini ya utekelezaji wa ugatuzi zimeshakamilika.

Hata hivyo, alisema serikali imeanza kuzifanyia mapitio sheria za sekta zilizogatuliwa ili ziendane na dhana ya ugatuzi.

# NEMC kufungua ofisi eneo la Stiegler's Gorge

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linajiandaa kufungua ofisi katika eneo la ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme katika bonde la Mto Rufiji la Stiegler's Gorge, kwa lengo la kuhakikisha ujenzi wa mradi huo hausababishi athari zozote za kimazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara katika eneo hilo la mradi mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnat Chaggu, alisema ni muhimu kuwapo kwa wataalamu wa mazingira katika eneo hilo, ili kutoa huduma za haraka pale itapohitajika na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa hatua za maendeleo ya mradi na hali ya mazingira kwa ujumla.

"Tumetembelea eneo hili la mradi mkubwa wa uzalishaji umeme unaojengwa ili kujionea namna mradi huu unavyotekelezwa na lengo letu ni kutoa huduma pale inapohitajika na kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha mradi unakamilika pasipo kukutana na vikwazo vyovyote vya kimazingira na katika muda uliopangwa," alisema Prof. Chaggu.

Aliongeza kuwa mradi huu unakusudia kuleta faida kubwa kwa Watanzania mara baada ya kukamilika, na kwamba ipo haja ya kufanya ufuatiliaji wa hatua kwa hatua katika mradi huo ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa pasipo vikwazo.

"Tumeshaleta wataalamu katika eneo hili la mradi tukisubiri kufungua rasmi ofisi zetu hapa Stiegler's Gorge, lengo ni kuhakikisha ujenzi wa mradi huu unakuwa rafiki wa mazingira na kuhakikisha pia shughuli zinazofanywa katika eneo lote hili hazileti athari zozote za kimazingira," alisema.

Prof. Chaggu aliongeza kuwa mradi huo utaleta ajira zaidi ya 8,000, na kuwataka vijana kuchangamkia fursa zitolewazo ili kujipatia kipato na kuacha kuwa tegemezi kwa jamii inayowazunguka.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema katika kuhakikisha kuwa wanafikia lengo la serikali la kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025, ni lazima NEMC ishirikiane na Tanesco kuhakikisha mambo yote yanayohusiana na mazingira yanatekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa, ili kuepusha changamoto zitakazoweza kuchelewesha ujenzi wa mradi huo muhimu kwa taifa.

Aliongeza kuwa mradi utaleta ustawi mkubwa si kwa upande wa uzalishaji umeme pekee, bali pia kuboresha sekta ya utalii ambapo kutaanzishwa safari za kitalii kutembelea eneo la mradi kwa kutumia boti maalum kwa upande wa kaskazini mwa mradi huo, eneo ambalo lina urefu wa kilomita 100.

Mradi wa Stiegler's Gorge unaotegemewa kuzalisha kiasi cha megawati 2,115 za umeme mara baada ya kukamilika kwake, upo katikati ya pori la akiba la Selous, ambapo pamoja na kuondoa tatizo la umeme Tanzania, mradi huo unalenga kuharakisha kutimia kwa azma ya serikali ya kutengeneza Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.




Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Barclays Tanzania, Aron Luhanga (katikati), na Mkuu wa Wateja Binafsi, Oscar Mwamfwagasi (kulia), wakifanya mawasiliano na mshindi wa kampeni ya 'Ishi Maisha ya Kifahari na Kadi Yako' ya Barclays Visa Credit Card' iliyokuwa na lengo la kuhamasisha matumizi ya kadi hizo katika kufanya manunuzi kwa wateja wapya na wa zamani. Mkazi wa Dar es Salaam, Yusufu Fadhili Mavura, alishinda. Wa tatu kulia ni Mkaguzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Abdallah Hemed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maofisa kilimo walalamikiwa kutowatembelea wakulima

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKULIMA katika kijiji cha Buchama Kata ya Tinde Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, wamelalamikia kutotembelewa na maofisa kilimo kwa ajili ya kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa.

Pia kuwaelimisha kulima mazao ambayo yanaendana na hali ya mazingira, ambapo wamekuwa wakilima kwa mazoea na kupata mavuno kidogo.

Wananchi walipaza kilio hicho juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kijijini humo wa kusikiliza na kutatua kero zao, kuwa ni miaka mingi sasa wamekuwa wakilima kwa mazoea bila kupatiwa elimu ya kilimo cha kisasa, na kujikuta wakiendelea kupata mavuno kidogo.

Mmoja wa wananchi hao, Charles Kashinje, alisema wamekuwa wakisikia kwenye kata hiyo kuna ofisa kilimo, lakini cha ajabu kwenye kijiji chao hawajawahi kumuona wala kuwatembelea, kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa ili waweze kupata mavuno mengi na kuinuka kiuchumi.

"Mkuu wa wilaya, kero yetu sisi wanakijiji, maofisa kilimo hawatutembelei kutupatia elimu ya kilimo cha kisasa, wala ushauri wa kulima katika mazao ambayo yanaendana na hali ya hewa, hivyo tumekuwa tukilima kimazoea na kupata mavuno kidogo, na msimu mwingine hukosa kabisa," alisema Kashinje.

"Hivyo, tunaomba katika msimu wa kilimo wa mwaka huu maofisa kilimo watutembelee hapa kijijini kwetu na sisi tupatiwe elimu hii ya kilimo cha kisasa.

Naye Ofisa Kilimo wa Kata hiyo, Hajra Omary, alitolea ufafanuzi suala hilo kuwa yeye ni mgeni kwenye kata hiyo, lakini aliahidi katika msimu wa kilimo wa mwaka huu ataanza kuwatembelea wakulima wote kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa kikiwamo kijiji hicho cha Buchama.

Kwa upande wake DC Mboneko, alikemea tabia ya maofisa kilimo kukaa ofisini, na kuwataka washinde mashambani kwa wakulima, ili kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa na kulima mazao rafiki, ili wapate kuinuka kiuchumi na kuiongezea nchi mapato.

# TIB yaboresha huduma wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo TIB imezindua mkataba wa huduma kwa wateja, ukiwa na lengo la kutoa huduma bora kwa wateja na wadau wa benki hiyo, kuelewa mahitaji yao pamoja na kujenga uhusiano wa kudumu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Maria Mashingo, alisema kuwa mkataba huo unawapa wateja haki ya kuelewa kiwango cha huduma kinachotolewa na benki hiyo wakati wote na pale benki itakaposhindwa kutimiza matarajio ya wateja, na kukiuka viwango ilivyojiwekea basi itakuwa tayari kupokea maoni.

"Benki imejipanga kutoa haki kwa wateja kwa kiwango ambacho itakidhi mahitaji ya wateja wake na pale itakaposhindwa kufanya hivyo basi itakuwa tayari kupokea maoni kutoka kwa wadau kwa lengo la kurekebisha na kuboresha zaidi huduma zake," alisema.

Aliongeza kuwa benki hiyo imejipanga kusimamia kwa dhati utekelezaji wa mkataba huo katika kufanikisha azma ya serikali ya kuwa na taasisi za umma zinazowahudumia wadau wake na kuchangia ukuaji wa uchumi.

"Mpaka kufikia Machi 30, 2019 benki ilikuwa na mali zinazofikia shilingi bilioni 614 na tumejipanga kusimamia mali hizo ili ziweze kuleta manufaa kwa Watanzania kwa kuzingatia sheria, sera, kanuni, miongozo na taratibu," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa wateja kuwa kama kioo cha benki hiyo katika utekelezaji wa mkataba huo ili kuendelea kuifanya benki hiyo kuwa mfano wa kuigwa katika kusaidia na kuwa kichocheo muhimu cha kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Charles Singili, amesema TIB ni mhimili muhimu katika kuunganisha serikali na sekta binafsi.

Singili ametoa wito kwa vijana ili kujua ni taasisi zipi zinaweza kuwakwamua ili waweze kuinua vipato vyao na taifa kwa ujumla.

"TIB imejikita katika kuwasaidia vijana waweze kusimamia misingi ya utawala bora, lakini pia kuangalia kwa namna ambavyo wanaweza kuzalisha mazao mbalimbali hali inayoweza kuwasaidia kutimia malengo yao binafsi na ya serikali ya viwanda," alifafanua.

Joseph Kidaha ambaye ni mteja, alisema mkataba huo una maana kubwa kwa wateja wa benki hiyo, huku akisisitiza kuwa, ukisimamiwa vizuri utaleta manufaa makubwa kwa wateja wake na Watanzania kwa ujumla.

ITV
JARIDA LA WANAWAKE
SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA WANAKIKUNDI TOKA GOBA JIJINI D`SALAAM KATIKA MAONYESHO YA KUSAIDIA WANAWAKE NA MATUMIZI YA KIKAPU BAADA YA KATAZO LA MATUMIZI YA MIFUKO YA PLASTIKI. "KAMPENI YAO INAITWA "KIKAPU CHANGU FAHARI".

## Rwanda yafunga tena mpaka wake na Uganda

**KIGALI, Rwanda**

SERIKALI ya Rwanda imefunga tena mpaka wake wa Katuna ulipo jirani na Uganda.

Hatua hiyo imekuja baada ya serikali ya Rwanda hapo awali kukubali kufungua mpaka huo kwa muda wa siku 12, ili kuruhusu malori yenye mizigo yaliyokuwa yamekwama kupita.

Hatua hiyo ilionekana ingemaliza uhusiano mbaya na serikali ya Uganda ambao umekuwa ukitokota tangu Februari.

Nchi za Rwanda na Uganda zinashuhudia mvutano wa kidiplomasia wakati Rwanda inaishutumu Uganda kwa kuwaficha maadui wa serikali yake, suala ambalo Uganda inakanusha vikali.

Hivi karibuni Rais wa Rwanda, Paul Kagame alielezea kuwa chimbuko la mgogoro baina ya nchi yake na nchi ya Uganda ni la tangu miaka 20 iliyopita, akilaumu nchi ya Uganda kutaka kuangusha utawala wake.

Rais Kagame alisema mgogoro huo ulishika kasi mnamo miaka ya hivi karibuni kutokana na serikali ya Uganda kuunga mkono kundi la RNC linalopinga utawala wa Kagame na ambalo linatumiwa na Uganda kuwanyanyasa raia wa Rwanda wanaotembelea au wanaoishi nchini Uganda.

"RNC wanafanya kazi kwa ushirikiano na vyombo vya usalama vya Uganda. Kilicho wazi ni kwamba wanachokifanya ni kunyanyasa Wanyarwanda ambao hawataki kuungana nao, huku wakiwasingizia kwamba wametumwa na utawala wa Kigali kuhujumu usalama wa Uganda na kuuwa Wanyarwanda wa upinzani. Ni madai yasiyo na msingi, lakini haya yote yanaonyesha ushirikiano wa dhati uliyopo baina ya serikali ya Uganda na kundi la RNC," alisema Rais Kagame.

Rais Kagame alisisitiza kwamba mara kadhaa mwenyewe aliwasilisha malalamiko hayo kwa mwenzake Rais Yoweri Museveni na kwamba hakuonyesha utashi wowote wa kuyatatua.

Hata hivyo Uganda imekuwa ikiishutumu Rwanda kuwatuma majasusi na kufanyia vitendo vya ujasusi kwenye ardhi yake, shutuma ambazo Rwanda inakanusha.

**RFI**

**Nchi za Rwanda na Uganda zinashuhudia mvutano wa kidiplomasia wakati Rwanda inaishutumu Uganda kwa kuwaficha maadui wa serikali yake, suala ambalo Uganda inakanusha vikali.**

# Wahusika jaribio mapinduzi Ethiopia wasakwa

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

VIKOSI vya usalama Ethiopia vinaendelea kuwasaka wahusika wakuu wa mauaji ya wanasiasa nchini humo.

Watu wanne waliuawa, ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Majeshi na Rais wa Jimbo la Amhara, kaskazini-magharibi mwa nchi.

Taarifa iliyotolewa na serikali ya Ethiopia ilieleza kuwa katika msako huo, watu kadhaa wameshakamatwa lakini operesheni bado inaendelea.

Serikali ya Ethiopia inamshutumu Mkuu wa Usalama wa Amhara, Jenerali Asaminew Tsige, kuongoza jaribio hilo la mapinduzi.

Jenerali Asaminew Tsige ambaye alikamatwa kwa njama ya madai ya kuhusika katika jaribio la mapinduzi la mwaka 2009 na kupewa msamaha wa rais mwaka 2018, amekimbilia mafichoni.

Asaminew Tsige amekuwa akishikilia wadhifa muhimu katika mkoa huu unaokabiliwa na mgawanyiko mkubwa.

Katika taarifa yake, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, alisema Mkuu wa Majeshi, Jenerali Seare Monnen, aliuawa nyumbani kwake kwa kupigwa risasi na mmoja wa walinzi wake, huku Rais wa Jimbo la Amhara, Ambachew Mekonnen akiuawa pamoja na mshauri wake.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Ethiopia, Ahmed Abiy ilieleza kuwa Jenerali Seare aliuawa sambamba na Jenerali Gezai Abera, na mlinzi aliyetekeleza tukio hilo amekamatwa.

Mauaji hayo yamezidisha shinikizo zaidi kwa Waziri Mkuu, Abiy, ambaye ameendelea kutekeleza mabadiliko katika idara za usalama na kuwaachia wafungwa wa kisiasa.

Waziri Mkuu, Abiy alikwenda kwenye kituo cha televisheni akiwa amevalia mavazi ya kijeshi kukemea mashambulizi hayo.

Hata hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu imemshutumu Mkuu wa Usalama wa Mji wa Amhara, Asaminew Tsige, kwa kupanga mapinduzi, lakini haijafahamika kama amekamatwa.

Mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yameikumba Amhara na miji mingine miaka ya hivi karibuni.

Tangu kufanyika kwa uchaguzi wa mwaka jana, Abiy amekua akipambana kumaliza mvutano wa kisiasa kwa kuwaachia huru wafungwa wa kisiasa, kuondoa makatazo dhidi ya vyama vya kisiasa na kuwashtaki maofisa wanaoshutumiwa kukiuka haki za binadamu.

Ubalozi wa Marekani mjini Addis Ababa umewatahadharisha wafanyakazi wake mjini humo kutotoka nje, ikisema ina taarifa kuhusu kutokea kwa mashambulizi ya risasi siku ya Jumamosi.

***RFI***



Viongozi wa nchi wanachama 28 wa Umoja wa Ulaya (EU) wakiwa katika mkutano mjini Brussels, Ubelgiji kwa mazungumzo ya faragha kuhusu nani wa kuongoza umoja huo. **PICHA: ALLIANCE**

# Upinzani washinda umeya Jiji la Istanbul

**INSTANBUL, Uturuki**

MGOMBEA wa upinzani, Ekrem Imamoglu, ameshinda katika uchaguzi wa marudio wa Meya katika Jiji la Istanbul nchini Uturuki.

Ushindi huo umemaliza mvutano wa kisiasa na kubadilisha mazoea ya chama tawala kuuongoza mji huo.

Imamoglu alipata asilimia 54.21 ya kura zilizopigwa, huku mpinzani wake, Waziri Mkuu wa zamani, Binali Yildrim kutoka chama cha AKP akiwa amepata asilimia 45.1 baada ya asilimia 99 ya kura zote zilizopigwa kuhesabiwa.

Jana maelfu ya wafuasi wa Imamoglu walisherehekea katika barabara za mji wa Istanbul baada ya mfanyabiashara huyo wa zamani kumshinda mgombea aliyechaguliwa na Rais Recep Tayyip Erdogan kwa karibu kura 800,000.

Imamoglu, ambaye ni mwanachama wa chama cha upinzani cha Republican People's Party (CHP), alisema ushindi wake utaleta mwanzo mpya kwa wananchi wa Uturuki.

"Ninamuomba Mungu atujaalie matokeo haya yalete bahati nzuri kwa taifa letu na Istanbul. Kama wananchi, mmefanikiwa kulinda miaka 100 ya demokrasia katika nchi yetu. Asanteni wananchi wenzangu! Matokeo haya hayamaanishi tu ukurasa mpya, bali yanamaanisha mwanzo mpya kwa Istanbul," alisema Imamoglu.

Matokeo ya awali yalibatilishwa kufuatia malalamiko kutoka chama tawala cha Rais Erdogan (AKP) kuwa kulifanyika makosa mengi wakati wa kupiga kura.

Uamuzi wa marudio ulikosolewa vikali na washirika wa Uturuki wa mataifa ya Magharibi na kuzua mzozo mkubwa kutoka kwa wapinzani wa ndani ya nchi waliosema demokrasia ya Uturuki inakabiliwa na kitisho.

Baraza Kuu la Uchaguzi Uturuki bado halikutangaza matokeo rasmi, lakini Yildirim alikubali kushindwa katika uchaguzi huo mara tu baada ya matokeo ya kwanza kutangazwa.

Erdogan pia alimpongeza mgombea huyo wa upinzani kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

Wakati Jiji la Istanbul likisherehekea ushindi wa Imamoglu, wachambuzi wanasema kuwa huu sio tu ushindi wa kimanispaa bali ni ushindi mkubwa zaidi kwani hata Erdogan aliwahi kusema yoyote atakayeshinda Istanbul, anakuwa ameshinda Uturuki.

Ni ushindi uliokuja wakati ambapo uchumi wa Uturuki umeshuka na bei za bidhaa zimepanda, hali iliyoharibu sifa ya Erdogan kama kiongozi imara katika suala la uchumi.

***DW***

# JPM afanya ziara ya kushtukiza daraja la Dar

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli, jana alifanya ziara ya kushtukiza katika mradi wa ujenzi wa daraja linalokatiza baharini kwa kuunganisha maeneo ya Aga Khan na Coco Beach jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, lengo la ziara hiyo lilikuwa kujionea maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo.

Rais Magufuli alishuhudia shughuli za ujenzi zikiendelea vizuri, ambapo mkandarasi ambaye ni kampuni ya GS Engineering ya Korea anakamilisha kuunganisha daraja la muda litakalomwezesha kuanza ujenzi wa nguzo za daraja, na kwamba kwa ujumla kazi imefikia asilimia 10.12.

Akiwa katika mradi huo Rais Magufuli alikutana na Mhandisi Mshauri kutoka Kampuni ya Yooshin Engineering, Suk-Joo Lee, na kumwelezea kufurahishwa kwake na maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo ambalo linatarajiwa kusaidia kupunguza msongamano wa magari kutoka na kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Naye Suk-Joo Lee alielezea kufurahishwa kwake kufanya kazi Tanzania na aliahidi kuwa kazi hiyo itakwenda vizuri.

Daraja hilo litakuwa na urefu wa kilometa 1.03 na barabara za kuunganisha zenye urefu wa kilometa 6.23. Ujenzi wake unahusisha ujenzi wa nguzo za msingi zenye urefu wa kati ya meta 14 na 65 na utagharimu takribani Sh. bilioni 255.

Daraja hilo limependekezwa kuitwa Tanzanite Bridge na litakamilika Oktoba 2021.



Baadhi ya wafanyakazi wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), wakishiriki katika kufanya usafi, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kama sehemu ya kuadhimisha kilele cha Wiki ya Utumishi wa Umma. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kortini kwa tuhuma za kughushi mil. 25/-

Na Hellen Mwango

WAKAZI wawili wa Tegeta jijini Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka saba ikiwamo kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. milioni 25.

Washtakiwa hao ni Veronica Tembe (45) na Lilian Kisamo (41), wote wakazi wa Tegeta.

Jana mahakamani hapo Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, aliwasomea washtakiwa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile.

Nguka alidai kuwa katika siku tofauti na mahali pasipojulikana washtakiwa wote wawili walikula njama ya kupata mkopo kwa njia ya udanganyifu.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kuwa siku na mahali pasipojulikana mshtakiwa Veronika peke yake akiwa na nia ovu alighushi kadi ya gari aina ya Toyota Rav 4 yenye namba za usajili T.504 BBT kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa kadi hiyo ni halisi na imetolewa na Mamlala ya Mapato Tanzania (TRA).

Pia mshtakiwa Veronika alidaiwa kuwa Novemba 27, 2012 katika benki ya EFC Microfinance, iliyopo Victoria ndani ya Wilaya ya Kinondoni, aliwasilisha kadi hiyo ya kughushi ya gari kwa maofisa wa EFC. Katika shtaka la nne mshtakiwa Veronica alighushi leseni ya biashara. Kwa madhumini ya kuonyesha kuwa leseni hiyo imetolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala.

Aidha, mshtakiwa Veronika anadaiwa Novemba 27, 2012 huko EFC Tanzania Microfinance Ltd., iliyoko eneo la Victoria mshtakiwa aliwasilisha leseni ya biashara ya kughushi kwa ofisa wa benki ya EFC kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa leseni hiyo imetolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala huku akijua kuwa siyo kweli.

Upande waJamhuri ulidai kuwa, siku na tarehe isiyofahamika, mshtakiwa Veronika akiwa na nia ovu alijipatia mkopo wa Sh. milioni 25 kupitia akaunti yake iliyopo katika benki hiyo kwa njia ya udanganyifu akijifanya kuwa yeye ndiye mmiliki wa leseni ya biashara na leseni hiyo ya gari ambavyo vilikuwa kama dhamana ya mkopo huo, huku akijua kuwa siyo kweli.

Katika shtaka la saba mshtakiwa Veronika anadaiwa kutakatisha Sh. milioni 25, huku akijua kuwa pesa hizo ni zao la makosa ya kughushi.

Hata hivyo, washtakiwa wamekana makosa hayo na mshtakiwa Lilian ameachiwa kwa dhamana huku Veronika akirudishwa rumande kwa kuwa shtaka la utakatishaji halina dhamana. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 2, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

# Zitto Kabwe aushtukia muswada wa Azaki

Inatoka uk 8

watu kufanya shughuli zao, kujumuika kwenye taasisi na kujiendesha kwa mujibu wa sheria, na pia ni sheria inayokwenda kuua biashara hasa kifungu cha 400 (a) cha sheria namba 10 kinachokwenda bungeni," alidai.

Akizungumzia Sheria ya Takwimu alisema walilalamika, lakini hawakusikilizwa na nje nako walifanya hivyo, na sasa serikali inafanya marekebisho yake.

"Ni kweli sheria zinatungwa, zinapita kwa hati ya dharura kwa sababu ya wingi ya watu wa CCM ndani ya Bunge, lakini msukumo ukiwa mkubwa wanarudi bungeni, mfano mzuri ni Sheria ya Takwimu ambayo ipo hati ya dharura."

Zitto alidai wanahitaji Watanzania wote kuunganika kwa sababu zimekuwa zikija sheria za kuwashughulikia mmoja mmoja kwa kuwa hawaunganiki zinapita kirahisi.

"Sheria ya vyombo vya habari ilivyokuja, tulisema inawahusu waandishi, baadhi tulisema wakasema wewe siyo mwandishi inakuhusu nini, hata waandishi walitushangaa wakasema wanasiasa tunawaingilia, Sheria ya Vyama vya Siasa ilivyokuja hivyo hivyo tukasema wanasiasa wenyewe na sasa wanashughulikia NGO," alisema.

Alisema ni wakati mwafaka wa Watanzania kuungana kwa pamoja kupinga, wasione zinahusu NGO peke yao.

**MADAI YA KUTUMIKA**

Kuhusu kutumika, Zitto alisema anaona ni viroja na vichekesho, na kwamba wataendelea kuelimisha na kuueleza umma ukweli.

"Kuingia kwenye malumbano kati yangu na Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally, nashangazwa sana nimeingia chuoni (UDSM) 1999 nimemkuta yupo mwaka wa tatu na alikuwa amegombea urais Daruso (Chama cha Wanafunzi) akawa ameshindwa, akawa rafiki yangu ninamuona kama ndugu zaidi ya rafiki," alisema.

Zitto alisema Dk. Bashiru anayemjua yeye ni mtu anayejadili hoja, masuala, siyo anayejadili nani anavaa nini, analishwa nini au analishwa na nani.

Zitto alimtaka Dk. Bashiru arudi kwenye kujadili hoja.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## MCHANGANYIKO

**MASHINE INAUZWA,** Profesional Floor Mashine cleaning inauzwa. Model namba: A005, Speed 154/min. Rated Power 1100W mpya kabisa. Ukihitaji Mawasiliano: 0715 942255


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



## KUPOTEA KWA VYETI



**Moses Cyril Masami** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0806-0186** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2001 katika shule ya Sekondari City, Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0731-0789** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2004 katika Shule ya Sekondari Makongo na Cheti cha Shahada chenye namba **S/N 426**2 kikichotolewa na Mzumbe University. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KJN/RB/7040/2019**

115292302

## GARI INAUZWA



Gari inauzwa aina ya
**TOYOTA HILUX 2.4, engine 2L.**
Ukitaka kuiona inapatikana Upanga Mtaa wa Undali nyumba namba 185, iko kwenye hali nzuri, full AC haina shida yoyote.

**Mawasiliani piga simu namba: 0711506758/0652316880 0686 316880**

115292402

## KUPOTEA KWA CHETI



Yusufu S. Majani anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1071-507** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari St. Mathew"s mjini Dar es Salaam. Yeyote atakaekiona taoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MBW/5300/19**

115292302

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAIRUNI MAULID DADU** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari KIUSA chenye **Index No S-3372-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2015 Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **MOS/RB/4625/19**

215292802

## KUPOTEA KWA CHETI



**Yese Modestus Kindimba** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0426-0092 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Wangin'gombe. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KW/RB/7040/18**

115291602

## KUPOTEA KWA CHETI



**Christina Joseph** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0302/0020** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1995, katika shule ya Sekondari Arusha. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **AR/RB/17128/06**

115291702

## KADI YA BAJAJI IMEPOTEA

**SALUMU HAJI BANZI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 151 ADS,** aina ya rangi yake nyekundu. Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,

Taarifa ya Polisi:
**MOR/MOR/RB/80951/2019.**

115292102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 87/2019**

**Ombi la JULIUS ELITWAMKAZA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu ELIAKUNDA ATHUMANI**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 11/7/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 21/6/2019



215292902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI,Wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 36/2019**

**MDAI:............................GRACE BAGAILE**

**MDAIWA;................DAUDI MWAIKO KESYA**


**Kwa : MWENYEKITI WA MTAA DDC KALOBE**

**KWA kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba TALAKA,MATUNZO YA WATOTO MGAWANYO WA MALI**

Kwahiyo Unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 4/7/ mwaka 2019 saa 2:30 asubuhi /alasiri kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zilizohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21/06/2019.



215293002

**IN THE DELEGATE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.37 OF 2019**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LEONARD ERASTO SATIMA -PETITIONER**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION SELEMANI LEONARD SATIMA GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are here by invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of probate for letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 26th day of JUNE, 2019.

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 24th This day of April,2019.



115291802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Stella Mafuru**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya harrier yenye namba za usajili **DKH 426**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .

Taarifa ya polisi
**KHM/RB/214/2019**

115293402


*KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO*
*Tupigie*
*0767 223311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767 223 311**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## NEYMAR: BARCA TULIENI, NAKUJA

**LONDON, England**

NEYMAR ameripotiwa amekiambia kikosi cha Barcelona watulie kwani anarudi hapo Nou Camp kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail, nyota huyo wa Paris Saint-Germain amekiambia kikosi hicho kinachonolewa na kocha Ernesto Valverde kwamba: "Tulieni, nitakuja tu."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliweka rekodi ya dunia kwenye usajili wakati akihamia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kutoka pale Catalunya mwaka 2017.

Majadiliano kati ya timu hizo mbili yapo kwenye hatua ya awali, lakini Neymar anajiamini kwamba atacheza Barcelona msimu ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anaamini kwamba mazungumzo kati ya Barcelona na PSG yatakuwa na matunda mazuri.

Tayari ameiambia PSG uamuzi wake wa kurudi pale Camp Nou na kwa mabingwa hao wa La Liga wanalijua hilo fika.


Neymar anajulikana kwamba bado ana urafiki wa karibu mno na Lionel Messi na Luis Suarez na wameanzisha kundi la kwenye mtandao wa kijamii wa WhatsApp wameliita 'los tres sudacas' ikiwa na maana 'watatu wa Amerika Kusini'.

Mshambuliaji huyo wa Brazil atalazimika kupunguza kiasi chake cha mshahara ili kulazimisha kurudi katika klabu yake hiyo ya zamani ya Barcelona.

Baada ya kuhamia kwa miamba hao wa Jiji la Paris na kuwa mchezaji ghali zaidi katika historia ya soka, Neymar alipewa mkataba ambao mshahara wake ni kiasi cha pauni milioni 32 kwa mwaka na uliongezeka kwa pauni 12.5 kutoka ule aliokuwa akilipwa pale Barca.

Neymar kwa sasa hayupo kwenye michuano ya Copa America kwa sababu anauguza majeruhi ya kifundo cha mguu.





# MAGUIRE

## AITOSA UNITED KUSAINI KWA REKODI CITY

**LONDON, England**

HARRY Maguire anakaribia kuthibitishwa kuweka rekodi ya kuhama kwa pauni milioni 80 wakati huu akitarajiwa kutua Manchester City na amekataa kujiunga na wapinzani wao, Manchester United, kwa mujibu wa Gazeti la The Mirror.

Beki huyo wa Leicester ameripotiwa kwamba amekubaliana na Man City na atalipwa pauni 280,000 kwa wiki pale kwenye dimba la Etihad.

Kama usajili huo utakamilika maana yake ni kwamba, Maguire ataivunja rekodi ya beki wa Liverpool, Virgin van Dijk na kuwa beki ghali zaidi duniani.

Maguire alisaini mkataba wa miaka mitano na Leicester Septemba mwaka jana na amebainisha kwamba, mpango wake wa kutua Man City ni mzuri zaidi kwake na asingeweza kuukataa.

Hilo litakuwa pigo kwa kocha, Ole Gunnar Solskjaer katika mipango yake ya kujenga Manchester United, kwani Maguire alidhaniwa kwamba angekuwa mmoja wa wachezaji wake msimu ujao.

# Eriksen sasa azifikiria Man United, Juventus

**LONDON, England**

NYOTA wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Christian Eriksen sasa anakaribia kujiunga ama na Manchester United au Juventus, huku Real Madrid wakiweka mguu sawa kama wakishindwa kumsajili Paul Pogba.

Mchezaji huyo wa Denmark amekuwa akitajwa kwamba anataka kuondoka katika klabu hiyo kipindi hiki cha majira ya joto, huku Real Madrid ndio ilikuwa ikitajwa kupewa nafasi kubwa.

Hata hivyo, baada ya kutumia fedha nyingi kipindi hiki, Los Blancos sasa hawataki tena kusaini mchezaji kwa fedha kubwa na mtu pekee wanayemsubiri kwa hamu ni Pogba.

Kwa mujibu wa Gazeti la The Mirror, Eriksen anajua kwamba hayupo kwenye mipango ya Real Madrid kipindi hiki, hivyo ameamua kuangalia upande mwingine.

Manchester United wanaona kwamba Eriksen anaweza kuwa mbadala wa Pogba kama ataondoka, huku Juventus pia wakimlia rada mchezaji huyo.



Real Madrid hadi sasa tayari wamewasajili Eden Hazard, Luka Jovic, Ferland Mendy, Eder Militao na Rodrygo Goes na maana yake ni kwamba hawana fedha za kutosha za kuipata saini ya wote wawili Eriksen na Pogba. Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane chaguo lake ni Pogba, na hivyo ni wazi kwamba nafasi ya Eriksen haipo.

## KOULIBALY: AFCON KWANZA, MAN UNITED, CITY BAADAYE

**CAIRO, Misri**

Kalidou Koulibaly anahisi anaweza kubaki Napoli msimu ujao licha ya tetesi kumhusisha na klabu kubwa za Ulaya, ingawa pia hana uhakika kwa asilimia 100.

Koulibaly, 28, alijunga na Napoli akitokea KRC Genk mwaka 2014 na ameweza kujiendeleza mwenyewe kama mmoja wa mabeki bora wa kati duniani.

Manchester United, Manchester City na wapinzani wakubwa wa Napoli, Juventus, wote wanasemekana kuhitaji huduma yake, ingawa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Aurelio De Laurentiis hajafanya suala hilo kuwa rahisi kutokana na kuhitaji euro milioni 120 ili kumwachia.

Koulibaly anaonekana kutokuwa na mchecheto kuhusu mustakabali wake wa baadaye wakati huu akiwa kwenye majukumu yake na timu ya Taifa ya Senegal kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 na juzi walishinda 2-0 dhidi ya Tanzania.

"Sijui [kama nitaendelea kubaki Napoli], ninadhani hivyo, lakini ninapaswa kucheza michuano ya Mataifa ya Afrika na kisha baada ya hapo nitarudi Napoli," Koulibaly aliiambia Goal.

"Kila mmoja anazungumza kuhusu mimi, lakini ninazungumza tu kuhusu Senegal, kwa sababu hilo ni lengo langu na ninataka kupata kitu fulani kikubwa na Senegal.

"Sitaki kuzungumza mustakabali wangu wa baadaye kwa sasa, ninapendelea kuzungumza kuhusu Senegal. Senegal imevuna kitu fulani kikubwa [Jumapili dhidi ya Taifa Stars]. Mimi ni asilimia 200 na Senegal asilimia 200 na watu milioni 15 wa Senegal.

"Sina mchecheto, ninataka kuangalia zaidi Afcon na kisha baada ya hapo nitarudi Napoli na tutaona nini kitatokea. Kitu muhimu sasa ni kushinda na Senegal."

Katika Kundi lake la C, Senegal imebakiza mechi mbili dhidi ya Algeria na Kenya.





# ETO'O: WE MO SALAH NENDA BARCELONA

**LONDON, England**

SAMUEL Eto'o amemshauri nyota wa Liverpool, Mohamed Salah kujiunga na Barcelona kama akipata nafasi, kwa mujibu wa BBC Sport.

Real Madrid imekuwa ikiwania kumsajili mshambuliaji huyo, hata hivyo, Eto'o amesema kwamba Barcelona ndiyo itakuwa sehemu sahihi kwa Salah.

"Real walinipa nafasi ya kuondoka Afrika, lakini najua staili ya uchezaji ya Barcelona na naona itamfiti zaidi yeye kuliko timu nyingine."

Eto'o alitumia miaka mitano akiwa Barcelona, na pia alianzia Real Madrid, lakini kwa muda wote aliokaa hapo alikuwa akipelekwa kucheza kwa mkopo.

Alienda Italia na Urusi kabla ya kutua Ligi Kuu ya England. Na sasa katika umri wake wa miaka 38, anacheza katika Klabu ya Qatar SC.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea, ambaye alionyesha kuhudhunishwa wakati Cameroon ikitolewa na England kwenye Kombe la Dunia la Wanawake juzi Jumapili, anaamini Salah anaweza kuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa duniani.

"Kama akipata nafasi ya kucheza kwenye ligi bora duniani, ambayo ni Hispania, anatakiwa kusaini Barcelona.

"Mo ana kila kitu kinachoweza kumfanya kuwa mchezaji bora duniani."

Mohamed Salah kwa sasa yupo kwenye majukumu ya timu ya taifa akiwa na Misri kwenye michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, yanayofanyika kwenye ardhi ya nchi yake.

Mchezo wao wa kwanza walishinda bao 1-0 dhidi ya Zimbabwe na kesho Jumatano watacheza na DR Congo, kabla ya kuwavaa Uganda Jumapili.

# Emery aitaka Arsenal imvunjie benki Zaha

**LONDON, England**

UNAI Emery anapanga kuhakikisha anaipata huduma ya Wilfried Zaha na ameiomba Arsenal kuvunja benki yake ili kuipata saini ya mchezaji huyo, kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail.

Arsenal ipo kwenye harakati za kusaka winga mpya katika kipindi hiki cha majira ya joto na sasa wanamuona nyota huyo wa Klabu ya Crystal Palace kuwa ndio chaguo lao, lakini kushindwa kwao kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kunaweza kusimshawishi mchezaji huyo.

Emery ameona kwamba, bajeti ya Arsenal ya pauni milioni 45 haitoshi baada ya kufungwa na wapinzani wao wa jiji la moja la London, Chelsea kwenye fainali ya Ligi ya Europa, ikiwa na maana kwamba watacheza msimu wa tatu mfululizo bila kuwapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.



Lakini kwa mujibu wa Gazeti la The Sun, Mhispania huyo ameitaka bodi ya Arsenal kutoa fedha zaidi hadi kufikia pauni milioni 55 kwa ajili ya kumpata winga huyo wa Palace.

Palace yenyewe imepanga kuweka ngumu au kumuuza kwa bei kubwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ivory Coast, ambaye tangu utoto wake ni shabiki wa Arsenal.


Thamani ya Zaha ilipanda zaidi msimu uliopita baada ya kufunga mabao 10 kwenye Ligi Kuu ya England na kutengeneza pasi za mwisho nyingi kwa klabu yake hiyo.

Emery pia atamshawishi Zaha kucheza kwenye Ligi ya Europa msimu ujao baada ya mchezaji mwenyewe kubainisha kwamba, anataka kucheza kwenye mashindano ya Ulaya msimu ujao.

Lakini Emery na Arsenal pia walionyesha nia ya kutaka kumsainisha nyota wa Celtic, Kieran Tierney, hata hivyo ofa yao ya pauni milioni 15 kwa ajili ya beki huyo wa kushoto ilikataliwa.

Celtic walikuwa wanataka angalau pauni milioni 25 ili kuweza kumuachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI: SASA TUMEANZA COPA AMERICA UPYA

Tulihitaji mchezo kama huu, kurudisha kujiamini, ni kama hatuna kitu, sasa tunahitaji...

**SAO PAULO, Brazil**

NAHODHA Lionel Messi anaamini ushindi wa Argentina dhidi ya Qatar utaisaidia timu hiyo kujiamini zaidi wakati huu wakiwa wamefanikiwa kutinga robo fainali ya michuano ya Copa America.

Miamba hao wa Amerika Kusini walijivuta nafasi ya pili kwenye Kundi lao la B baada ya ushindi wa 2-0 dhidi ya Qatar usiku wa kuamkia jana, shukrani kwa mabao ya Lautaro Martinez na Sergio Aguero.

Ulikuwa ni ushindi wa lazima kwa Argentina ili kutinga nafasi hiyo, kwani katika michezo yake miwili ya mwanzo ilipata ponti moja tu.

Akinukuliwa na tovuti ya timu hiyo, Messi alisema: "Tulikuwa na mchezo mzuri na tulishinda, kitu ambacho kilikuwa cha muhimu zaidi.

**"Tulihitaji mchezo kama huu, kurudisha kuji amini kwenye mchezo na kutulia. Wakati mechi zikiendelea, timu ilihitaji kuwa na mechi kama hii na ilikuwa maalumu kwa ajili ya sisi kuendelea kukua na malengo yetu kutimia."**

Aliongeza: "Sasa tunaanza michuano upya, michuano ya Copa Amerika. Sasa tunaanza kila kitu upya ni kama hatuna chochote."

Mshambuliaji wa Klabu ya Inter Milan, Martinez alianza kuifungia Argentina katika dakika ya nne, akitumia udhaifu wa mabeki wa Qatar na kuujaza mpira wavuni.

Aguero mshambuliaji wa Manchester City aliihakikishia Argentina ushindi huo kwa kufunga bao dakika ya 82 na kuwawezesha kumaliza wakiwa nafasi ya pili kwenye msimamo.

Hata hivyo, Messi alikosa nafasi kadhaa za wazi kuweza kuongeza mabao kwa Argentina kwenye mchezo huo.

Ushindi huo unamaanisha kwamba Argentina sasa itacheza na Venezuela kwenye hatua ya robo fainali Ijumaa jijini Rio de Janeiro.

Vinara wa kundi hilo la B, Colombia waliifunga Paraguay bao 1-0 kwenye dimba la Fonte Nova, mfungaji akiwa ni Gustavo Cuellar katika dakika ya 31.

## KWA UFUPI

### LIVER, UNITED VITANI KWA FIRPO

LIVERPOOL na Manchester United zitaingia vitani kuwania saini ya beki wa kushoto wa Real Betis, Mhispania Junior Firpo, 22. ***(Marca)***

### PEPE AZIGONGANISHA INTER, LIVER

LIVERPOOL inataka kuipiku Inter kwa dau la pauni milioni 80 ili kumnasa Nicolas Pepe, 24, lakini miamba hiyo ya Serie A ni kati ya klabu nyingi zinazovutiwa kuipata saini ya winga huyo wa Lille na Ivory Coast. ***(L'Equipe - in French)***

### ARSENAL YATAJIWA DAU LA NKUNKU

PARIS St-Germain inataka pauni milioni 13.5 kwa Christopher Nkunku, wakati huu Arsenal na RB Leipzig zote zikivutiwa na huduma ya kiungo huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 21. (L'Equipe - in French)

### MADRID YATAJA BEI YA VARANE

MANCHESTER United imeelezwa kwamba itawagharimu pauni milioni 430 kama inataka kuipata saini ya beki wa kati Mfaransa Raphael Varane, 26, kutoka Real Madrid. ***(Star)***

### INTER YATESEKA KWA LUKAKU

INTER Milan bado inaupungufu wa pauni milioni 22.3 katika thamani pendekezwa kwa mshambuliaji wa Manchester United, Mbelgiji Romelu Lukaku, 26. (La Gazzetta dello Sport, via Football Italia)

### EMERY AMTAKA ZAHA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery ameitaka 'Gunners' kuvunja benki yao ili kuipata saini ya mshambuliaji wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26. ***(Sun)***

### RASHFORD AIPASUA KICHWA UNITED

MANCHESTER United itatazama mbadala wao wa kuongeza Marcus Rashford mkataba wa miezi 12 licha ya kuwapo kwa hofu ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kuondoka wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika majira ya joto yajayo. ***(Sun)***

### BENITEZ, NEWCASTLE KUJADILI MKATABA

NEWCASTLE United inajiandaa kufanya mazungumzo kwa mara ya mwisho na kocha wao, Rafael Benitez kuhusu uwezekano wa kuongeza mkataba wa kuinoa klabu hiyo. Kocha huyo mwenye umri wa miaka 59, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa Juni, ameripotiwa kupewa ofa ya kwenda kufanya kazi China. ***(Chronicle)***

### ALMIRON AWINDWA NA MADRID

KIUNGO wa Newcastle na Paraguay, Miguel Almiron, 25, anawindwa na Real Madrid. ***(TYC Sports - in Spanish)***

### ABRAHAM KUNUFAIKA KIUNGO CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa England U-21, Tammy Abraham, 21, anataka kutumia faida ya Chelsea kufungiwa kusainisha wachezaji kwa kuwa chaguo la kikosi cha kwanza cha 'Blues'. ***(Mail)***

### SOLSKJAER AMTAKA FERNANDES MAPEMA

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ametuma ombi lake binafsi kwa Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Ed Woodward kuhakikisha wanafanikisha mapema kuipata saini ya kiungo wa Sporting Lisbon na Ureno, Bruno Fernandes, 24. ***(Record - in Portuguese)***

### TORRIERA ANUKIA KUUZIWA MILAN

Arsenal inafikiria kumuuza Lucas Torriera, 23, baada ya AC Milan kuwasilisha ofa kwa kiungo huyo wa kimataifa wa Uruguay. ***(Sport Mediaset - in Italian)***

### RODGERS ABANIWA KWA MCGREGOR

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers ameambiwa ni sawa na kupoteza muda wake katika mchakato wa kujaribu kuipata saini ya kiungo Mscotland Callum McGregor, 26, kutoka klabu yake ya zamani ya Celtic. ***(Scottish Daily Mail)***

## HABARI MICHEZO

# UGANDA MBELEKO YA CECAFA AFCON, STARS, HARAMBEE BADO

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

TIMU ya Taifa ya Uganda (The Cranes), imeendelea kuwa wawakilishi wazuri wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, ambazo zinaendelea katika viwanja mbalimbali nchini Misri baada ya Tanzania (Taifa Stars), Kenya (Harambee Stars) kuungana na Burundi kwa kuanza vibaya.

Mwaka huu katika fainali hizo, Cecafa inawakilishwa na timu nne ambazo ni Uganda, Tanzania, Burundi na mabingwa wa Kombe la Chalenji, Kenya.

Katika mechi yake ya kwanza Uganda ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kukaa kileleni katika Kundi A ambalo linaundwa pia na mwenyeji Misri na Zimbabwe.

Mabao ya Uganda katika mchezo huo yalifungwa na Farouk Miya pamoja na mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi.

Burundi yenyewe inayoshiriki mashindano hayo kwa mara ya kwanza ilianza vibaya kwa kufungwa bao 1-0 na mabingwa wa zamani wa michuano hiyo, Nigeria, wakati Taifa Stars inayonolewa na Emmanuel Amunike ilifungwa 2-0 na Senegal.

Nyota waliyoipa pointi tatu Senegal katika mchezo huo wa Kundi C ni winga Keita Balde anayeichezea Inter Milan kwa mkopo akitokea Monaco na Krepiri Diatta anayekipiga Club Brugge ya Ubelgiji.

Uganda itashuka tena dimbani kesho kuivaa Zimbabwe, huku Burundi ikimenyana na Madagascar wakati Kenya na Tanzania zikitarajiwa kutoa jasho keshokutwa.

Stars ilifungwa mabao hayo katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa June 30 na kuhudhuriwa na mashabiki wake kutoka sehemu mbalimbali, wakiwamo wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao waliongozwa na Mwenyekiti wa Bunge FC, William Ngeleja.



Mshambuliaji na Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta (kulia, akipata upinzani wakati akijaribu kumtoka beki wa Senegal kwenye mechi ya michuano ya Afcon 2019 iliyopigwa Uwanja wa June 30, juzi jijini Cairo, Misri na Senegal kushinda 2-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Burundi yaipania Madagascar kesho

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Burundi, Olivier Niyungeko, amesema anaamini kikosi chake kitafanya vizuri katika mchezo wao wa pili dhidi ya Madagascar kutokana na kiwango cha juu walichokionyesha walipocheza na Nigeria.

Burundi ambayo inashiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 kwa mara ya kwanza, ilifungwa bao 1-0 na Nigeria, lakini ilionyesha kiwango kizuri na kuwashangaza vigogo hao wa Afrika.

Mechi ya pili ya Kundi B kati ya Burundi dhidi ya Madagascar itachezwa keshokutwa mjini Alexandria.

Akizungumza na gazeti hili jana, Niyungeko alisema kuwa amewaandaa wachezaji wake kuongeza umakini na kutoidharau Madagascar ambayo ilianza kwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Guinea.

Niyungeko alisema mechi zote za mashindano hayo ni ngumu, lakini hakuna timu yenye kushuka uwanjani ikiamini itaondoka na pointi tatu.

"Soka limebadilika, hakuna mwenye uhakika wa kupata ushindi, ndio maana hakuna timu ambayo imefungwa mabao zaidi ya manne kama ilivyokuwa tukishuhudia mechi za fainali zilizopita, wachezaji wa Afrika Mashariki sasa wamepata uzoefu," alisema kocha huyo.

Alimtaja mchezaji wake chipukizi, Mohammed Amissi ambaye ana umri wa miaka 18, aliyekuwa anasumbuliwa na homa, amepona na atakuwapo katika mchezo unaofuata.

Naye Rais wa Shirikisho la Soka Burundi ( BFF), Reverien Ndikuriyo, aliliambia gazeti hili kuwa, timu yao imeimarika na wanaamini watafanya vema mechi mbili zilizobakia.

"Mechi zetu za kirafiki dhidi ya Tunisia na Algeria zilitusaidia sana, wachezaji wamekuwa na uwezo mzuri, mmeona hata Nigeria tumewapa tabu sana, kuna vitu vidogo tukivirekebisha, tutafika mbali," alisema Ndikuriyo. Kiongozi huyo alisema pia, shirikisho lake linawataka wachezaji wote kuwa na nidhamu na halitamtetea mchezaji ambaye ataondolewa kikosini na kocha mkuu wa timu hiyo.

## Tatu Z'bar zapata leseni ya kimataifa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya utoaji leseni kwa klabu za Ligi Kuu Zanzibar (FIB), imetoa leseni ya Kimataifa kwa klabu tatu, huku klabu nane zikipewa leseni ya ligi ya ndani.

Klabu zilizopewa leseni ya Kimataifa ni Malindi, KMKM na JKU, huku leseni ya ligi za ndani zikitolewa kwa Selem View, Zimamoto, Chipukizi, Jamhuri, Kipanga, KVZ, Mafunzo na Polisi.

Akizungumza katika hafla hiyo ya utoaji leseni, Meneja wa Leseni kwa Klabu, Suleiman Shabani, alisema katika mchakato huo jumla ya klabu 14 ziliomba leseni lakini klabu 11 ndizo zilimefanikiwa kukaguliwa katika mchakato huo ulioanza mapema mwa mwaka huu.

Akitaja upande wa klabu ambazo hazijakaguliwa na zinacheza Lgi Kuu alisema ni Klabu ya Jang'ombe Boys, Chuoni, Mwenge, Mlandege pamoja na timu moja kutoka kisiwani Pemba ambayo itapanda daraja kucheza Ligi Kuu.

Alisema kwa klabu ambazo hazijakaguliwa hadi mwisho wa mchakato huo hazishiriki Ligi Kuu hivyo akazitaka kuharakisha kuhakikisha zinakaguliwa kabla kuanza kwa msimu wa ligi.

## Chirwa apania kuipa Azam Kagame Cup

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Azam FC ikiendelea kujifua kuelekea michuano ya Kombe la Kagame, mshambuliaji aliyeongezewa mkataba wa mwaka mmoja wiki iliyopita, Obrey Chirwa amesema amedhamiria kuhakikisha timu yake hiyo inatetea ubingwa huo nchini Rwanda mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Chirwa alisema ameshukuru uongozi wa Azam FC kumpa mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo na kilichobaki sasa ni yeye kuonyesha thamini yake.

"Nimejipanga vizuri kwa ajili ya Kagame Cup, naahidi kujituma ili niifikishe mahali pazuri timu yangu," alisema Chirwa.

Aidha, alisema ataendeleza ushirikiano mzuri na wachezaji wenzake pamoja na kumsikiliza mwalimu wao kwa makini ili waendelee kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Julai 7 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.


"Kikubwa ni kumsikiliza mwalimu kwa makini anapokuwa anatufundisha ili tuweze kuipa mafanikio timu yetu," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Yanga.

Chirwa alitia saini wiki iliyopita mkataba wa mwaka mmoja kuendelea kuitumikia klabu hiyo msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wakati huo timu hiyo ikiwa chini ya Etienne Ndayiragije aliyeinoa KMC msimu uliomalizika na kuiwezesha kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

# Michezo

Jumanne Juni 25, 2019

Nipashe

## Messi: Sasa tumeanza Copa America upya

HABARI UK 30




Sergio Aguero (katikati) akiwa katika harakati za kufunga kwenye mechi ya michuano ya Copa America ambayo alitupia bao moja wakati Argentina ikishinda 2-0 dhidi ya Qatar. Kwa matokeo hayo ya mechi hiyo iliyopigwa Porto Alegre nchini Brazil juzi, yameipeleka Argentina robo fainali. **HABARI UK. 30**

# AMUNIKE AICHAMBUA STARS KIPIGO SENEGAL

●●●Asema bado wananafasi Afcon, Nyoni sasa fiti kuivaa Harambee Stars Alhamisi, kazi kwa kocha...

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

LICHA ya kuanza vibaya fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, Kocha Mkuu wa Timu ya Tanzania (Taifa Stars), Mnigeria Emmanuel Amunike, amesema bado anakiamini kikosi chake kinachoshiriki mashindano hayo baada ya kuikosa michuano hiyo kwa miaka 39.

Taifa Stars ilipoteza mechi yake ya kwanza ya Kundi C kwa kufungwa mabao 2-0 na Senegal ambayo ilitumia wachezaji wote wanaocheza soka la kulipwa barani Ulaya.

Amunike aliliambia gazeti hili kuwa mchezo dhidi ya Senegal ulikuwa ni mgumu kwa timu yake, lakini anawapongeza wachezaji wake kwa namna walivyopambana kuhakikisha wanawabana vigogo hao kutoka Afrika Magharibi.

Alisema hata wapinzani wao pia walipata tabu katika kufanya mashambulizi katika mchezo huo, na changamoto hiyo iliwafanya wabadilishe mfumo kila wakati ili kuwafanya Senegal washindwe kutawala mchezo kwa kipindi kikubwa.

"Mechi ilikuwa ngumu, na hata kwao pia, naamini watakuwa wanasema wamekutana na timu tofauti na ile ambayo waliifikiria kabla ya mchezo kuanza, wachezaji wangu wanaendelea kujifunza mbinu, kutokana na kila wanachokiona baada ya kumaliza mchezo mmoja," alisema Amunike.

Kocha huyo aliongeza kuwa bado nafasi ya kusonga mbele katika mashindano hayo ipo, kwa sababu kila timu imebakiza michezo miwili ya hatua hiyo ya makundi ambayo itamalizika Julai Mosi.

"Wachezaji wangu wanasonga mbele, ugumu na changamoto wanazokutana nazo, huwasaidia kuwajenga, wanaimarika na nina matumaini watafanya vema mchezo wa pili dhidi ya Kenya, najua wanajuana lakini sasa wanakutana katika mashindano ya ngazi ya juu Afrika," Amunike aliongeza.

Naye beki wa pembeni wa Stars, Hassan Kessy, alisema kuwa makosa mawili waliyofanya ndiyo yaliwapa wapinzani wao Senegal nafasi za kufunga katika mchezo huo.

Hata hivyo beki huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar, Simba na Yanga alisema kwamba watarekebisha makosa hayo na kuingia wakiwa makini zaidi katika mchezo dhidi ya Harambee Stars ya Kenya ili wapate ushindi na kuweka matumaini ya kusonga mbele kwenye fainali hizi zinazofanyika kwa mara ya 13.

**NYONI AREJEA**

Katika hatua nyingine beki wa kati mkongwe wa Taifa Stars, Erasto Nyoni, amesema kuwa afya yake imeimarika na anaamini atakuwa tayari kucheza mechi ya pili ya Kundi C ya Harambee Stars keshokutwa.

Nyoni alikosa mchezo wa kwanza wa fainali hizo dhidi ya Senegal, ambapo Taifa Stars ilifungwa mabao 2-0, kutokana na maumivu ya nyama za paja.

Beki huyo kiraka alipata maumivu hayo katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Misri iliyochezwa Juni 13, mwaka huu, ambayo pia ilimpa majeraha ya goti, beki mwingine wa timu hiyo, Aggrey Moris ambaye anasubiri kufanyiwa upasuaji nchini Afrika Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nyoni, alisema kwa sasa afya yake imeimarika na ameanza mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake kwa kushiriki programu zote zinazotolewa na benchi la ufundi.

"Nimepona, msiwe na wasiwasi, mechi ijayo nitacheza, labda kocha aamue vingine," alisema kwa kifupi beki huyo wa zamani wa mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC ya jijini Dar es Salaam.

## Simba yaiwahi TP Mazembe kwa Tshabalala

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ikielezwa vigogo wa soka wa TP Mazembe ya DR Congo wapo jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Simba kuhusu uwezekano wa kumnasa beki wao wa pembeni, Mohammed Hussein 'Tshabalala' ama ukipenda mwite 'Zimbwe Junior', nahodha huyo msaidizi amesaini mkataba mpya wa miaka miwili kuendelea kuwatumikia mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

**Tshabalala ambaye yupo na kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania ('Taifa Stars') kilichopo Cairo, Misri kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), ameelezwa alitia saini mkataba huo kabla ya kuondoka nchini Juni 7, mwaka huu, lakini jana ndiyo klabu yake ya Simba imeuanika rasmi.**

Kwa mantiki hiyo, Tshabalala sasa anaungana na nahodha mkuu, John Bocco, kipa Aishi Manula, mabeki Erasto Nyoni, Shomari Kapombe, kiungo Jonas Mkude na mshambuliaji Meddie Kagere raia wa Rwanda kwenye orodha ya wachezaji ambao wameongeza mikataba yao na Simba.

Aidha, Tshabalala ambaye ni miongoni mwa wachezaji walioonyesha uwezo mkubwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuiwezesha klabu hiyo kufika robo fainali kabla ya kutolewa na TP Mazembe msimu uliomalizika, imefahamika kwamba kwa sasa anawindwa na miamba hiyo ya DR Congo.

"Ni kweli wanamhitaji Tshabalala pamoja na Fei Toto (Feisal Salum wa Yanga) na straika Kinda wa Serengeti Boys, Kelvin John 'Mbappe'," kilieleza chanzo chetu jana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042